SILSILA YA HOTUBA ZA AL-MASJID AN-NABAWI 1

# TAWHIDI

## KATIKA HOTUBA ZA AL-MASJID AN-NABAWI



UTUNZI WA
DKT. ABDUL-MUHSIN IBNU MUHAMMAD AL-QAASIM
IMAMU NA HATIBU WA AL-MASJID AN-NABAWI SH-SHARIIF

مترجم بالسواحلية

# TAWHIDI

## KATIKA HOTUBA ZA
## AL-MASJID AN-NABAWI

**KODI KWA KUTEREMSHA KITABU HICHI PANGUSA**

a-alqasim.com

# Tawhidi
## katika Hotuba za Al-Masjid An-Nabawi

Utunzi Wa
**Dkt. Abdul-Muhsin ibn Muhammad Al-Qaasim**
Imamu na khatibu wa Al-Masjid An-Nabawi Ash-Shariif

بسم الله الرحمن الرحيم

**Naanza kwa kutaka usaidizi na baraka kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.**

# UTANGULIZI

Sifa njema zote anastahiki Allah Mola mlezi wa viumbe vyote, na swala na salamu zimshukie Nabii wetu Muhammad, watu wake na masahaba wake kwa jumla.

**Ama baada ya himdi hii**

Kwa hakika Tawhidi ndio wajibu wa kwanza juu ya waja, na kwa ajili yake Allah ameumba majini na binadamu, na kwa ajili yake ametumiliza Mitume na ameteremsha Vitabu, na akajaalia Pepo kuwa malipo ya watu wake [Tawhidi], na kwa utukufu wa shani yake imekuwa ndio jambo kubwa zaidi wanaolinganiwa kwalo waja.

Na kwa ajili ya umuhimu wa msingi huu [wa Tawhidi] ndio nilitoa hotuba zinazouhusu katika Msikiti wa Nabii, kisha nikazipangilia katika kitabu hiki, na nikakiita: «**Tawhidi; katika Hotuba za Al-Masjid An-Nabawi**», na zimetimu hotuba kumi na nne.

Namuomba Allah anufaishe [watu] nacho, na akijaaliye [ni amali] iliotakaswa kwa ajili ya Uso wake mkarimu.

Na swala na salamu za Allah zimshukie Nabii wetu Muhammad, watu wake na masahaba wake kwa jumla.

**Dkt. Abdul-Muhsin ibn Muhammad Al-Qaasim**
Imamu na khatibu wa Al-Masjid An-Nabawi Ash-Shariif.

# UMUHIMU WA TAWHIDI[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi enyi waja wa Allah mcheni Allah haki ya kumcha; kwani kwa uchamngu akili na nyoyo zinapata nuru, na makosa na madhambi yanafutwa.

**Enyi Waisilamu:**

Hakika Allah ametuneemesha na Dini inayoafikiana na maumbile yalionyooka, na akili zilizosalimika, yenye kusilihi kwa kila zama na sehemu, yenye kukusanya baina ya elimu na ibada, na baina ya kauli, amali, na itikadi. Allah hakubali kutoka kwa waja Dini isiyokuwa hiyo:

﴿وَمَن يَبۡتَغِ غَيۡرَ ٱلۡإِسۡلَٰمِ دِينٗا فَلَن يُقۡبَلَ مِنۡهُ وَهُوَ فِي ٱلۡأٓخِرَةِ مِنَ ٱلۡخَٰسِرِينَ﴾

{Na anaye tafuta Dini isiyo kuwa Uislamu haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye kukhasiri} [Aalu-Imran: 85].

Mnao ndani ya Dini hii, Neno ambalo atakayelisema hali ya kuwa mkweli ndani ya moyo wake, na akatenda kwa mujibu wake, akitaka na kukusudia kwa hilo Uso wa Allah, ataingia

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe ishirini na nne, mwezi wa Dhul-hijjah, mwaka elfu moja mia nne na ishirini na mbili hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

Peponi bila ya hesabu wala adhabu: «Laa ilaaha illa llaah». Hilo [Neno] ndilo neno zuri zaidi, amali bora zaidi, na tagaa la Imani la juu zaidi, atakayelisema ki haki atanyanyuka hadi daraja ya juu zaidi katika daraja za Dini. Kulitamka pekee hakutoshi kuingia katika Uisilamu au kubaki juu yake, bali ni wajibu pamoja na huko [kulisema] awe Muisilamu anajua maana yake, mwenye kutenda kwa mujibu wake; miongoni mwa kukanusha Shirki na kuthibitisha Upweke [Tawhidi] kwa Allah, akiitakidi usahihi wa yaliyokusanywa na kuwajibishwa nalo.

Na Muisilamu ni mkweli katika Imani yake na Itikadi yake, ni mwenye kujisalimisha kwa Allah katika hukumu, amri, sheria na kadari, hateremshi mahitaji yake ila kwa Allah, wala haombi kuondoshewa majanga yake na yeyote ila kutoka kwake aliyetakasika, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَإِن يَمْسَسْكَ ٱللَّهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهُۥٓ إِلَّا هُوَ ۖ

وَإِن يَمْسَسْكَ بِخَيْرٍ فَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ قَدِيرٌ﴾

{Na ikiwa Allah atakugusisha madhara, basi hapana wa kukuondolea hayo ila Yeye [Allah]. Na ikiwa atakugusisha heri, basi Yeye ndiye Mwenye uweza wa kila kitu} [Al-an`aam: 17].

Na kumuomba yeye pekee aliyetakasika ni ibada tukufu miongoni mwa ibada bora zaidi, [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Hakuna kitu kikarimu zaidi kwa Allah kuliko Dua**», imepokewa na Ahmad,

Na ibnu Abbaas Allah amridhie amesema: «Ibada bora zaidi ni Dua».

Na pindi zinapokushukia ajali na majanga, na njia zikafungwa mbele ya uso wako, muite Mtukufu; kwani Yeye humpatia anayemuomba, na humlinda mwenye kujikinga naye, [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema kumwambia ibnu Abbaas Allah amridhie yeye na babake:

«**Pindi unapoomba basi muombe Allah, na pindi**

**unapotaka msaada basi taka kutoka kwa Allah, na jua kuwa lau umma mzima utakusanyika ili wakunufaishe na kitu, basi hawawezi kukunufaisha na chochote ila na kile alichokuandikia Allah, na lau watakusanyika ili wakudhuru na kitu, basi hawawezi kukudhuru na chochote ila na kile alichokuandikia Allah**», imepokewa na Tirmidhi.

Wala usiache kwa kiburi kumuomba Mola wako Mlezi mambo yaliyo madogo; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Muombeni Allah kila kitu, hata kamba ya kiatu; kwani kama Allah hajaisahilisha haitakuwa sahali**», imepokewa na Abu Ya'laa,

Ama maiti au aliye ughaibuni basi kwa hakika hajimilikii nafsi yake manufaa wala madhara seuze kumnufaisha mwengine, na maiti [mwenyewe] anahitajia wa kumuombea, kama alivyotuamuru Nabii wetu swala na salamu za Allah zimshukie pindi tunapozuru makaburi ya Waislamu tuwaombee rehema na tuwaombee, na tusiwaombe uokozi.

Na Mola wetu Mlezi aliyetakasika amesifika na usikizi na uoni, na miongoni mwa kuufanyia kasoro Ulezi wake ni kutia dosari ibada zake: ukafanya ukati baina yako na baina yake katika maombi, na hali Yeye ndiye aliyesema:

﴿ٱدۡعُونِيٓ أَسۡتَجِبۡ لَكُمۡ﴾

{Niombeni nitakuitikieni}, [Ghaafir: 60]

Na ni katika yenye kuvunja Neno la Ikhlasi kumwaga damu [kuchinja] kwa ajili ya asiyekuwa Allah:

﴿قُلۡ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحۡيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ ٱلۡعَٰلَمِينَ ۞
لَا شَرِيكَ لَهُۥۖ وَبِذَٰلِكَ أُمِرۡتُ وَأَنَا۠ أَوَّلُ ٱلۡمُسۡلِمِينَ﴾

{Sema: Hakika Swala yangu, na kuchinja kwangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Allah, Mola Mlezi wa viumbe vyote * Hana mshirika wake. Na hayo ndiyo niliyo amrishwa, na mimi ni wa kwanza wa Waislamu [katika umma

huu]} [Al-an`aam: 162-163].

Na kutufu Nyumba ya kale ni ibada inayokusanya udhalilifu na unyonge kwa ajili ya Mola Mlezi wa Nyumba [Kaaba]:

﴿وَلۡيَطَّوَّفُواْ بِٱلۡبَيۡتِ ٱلۡعَتِيقِ﴾

{na watufu Nyumba ya Kale} [Al-Hajj: 29].

Na kutufu kwa asiyekuwa Allah, miongoni mwa kutufu madhabahu na makaburi, [hayo] yanawajibisha kunyimwa Pepo.

Na kuapa kwa Allah hali ya kuwa mkweli tena katika sehemu za kuhitajia hilo; ni katika kumuadhimisha Mola Mlezi wa walimwengu, na kuapa kwa asiyekuwa Yeye ni kudharau utukufu wa Muumba Mtukufu na aliye juu; kwa ajili ya hilo Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**aliye apa kwa asiyekuwa Allah, basi amekufuru au amefanya ushirikina**», imepokewa na Tirmidhi.

Na aliyechukua hirizi kwa ajili ya kujikinga na jicho, au kujivutia manufaa, basi huyo [Mtume] mteule amemuapiza; Allah asimtekelezee malengo yake, na asijibiwe na apate kinyume cha makusudio yake, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Atakaye funga hirizi basi Allah asimtimizie**», imepokewa na Ahmad.

Na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikataa kuchukua 'bai-ah' [ahadi ya kuinusuru dini] kutoka kwa aliyekuwa amefunga hirizi; Uqbah ibnu A'mir Al-Juhani Allah amridhie anasema:

«**Lilikuja kundi la watu kumi kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie, akachukua 'bai-ah' kutoka kwa tisa na akakataa kutoka kwa mmoja wao, basi wakasema: Ewe Mtume wa Allah, umechukua 'bai-ah' kutoka kwa tisa na ukamwacha huyu? [Mtume] akasema: yuko na hirizi; basi [yule bwana] akaingiza mkono wake [ndani ya nguo] na akaikata, hapo [Mtume] akachukua 'bai-ah' yake, na**

**akasema: Atakayefunga hirizi basi hakika amefanya ushirikina**», imepokewa na Ahmad.

Basi wakati wa mazito na huzuni kimbilia kwa [Allah] Mmoja Mwenye kuhesabu na kulipa, kwani Yeye ni mzuri wa kuitikia, na yule itakayo fungamana nafsi yake na amri yake yote akaikabidhi kwake; basi atamtosheleza mahitaji yote, na atamsahilishia kila zito, na atakaye fungamana na mwengine asiyekuwa Yeye, au akapata utulivu kwa elimu yake [mwenyewe], akili yake na hirizi zake, na akategemea uwezo wake na nguvu zake; basi Allah humtegemeza kwa hizo na humkosesha taufiki, alisema [sheikh Suleiman ibnu Abdillah ibni Muhammad ibni Abdil-Wahhaab] katika [kitabu chake] 'Taysiir Al-Aziiz Al-Hamiid' : "Na hili linajulikana kupitia dalili na majaribio".

Na ni miongoni mwa masururu ya kubomoa Dini: Kuwaendea wachawi na waganga, na kuwauliza makuhani na mpiga ramli; [Allah] mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنۡ أَحَدٍ حَتَّىٰ يَقُولَآ إِنَّمَا نَحۡنُ فِتۡنَةٞ فَلَا تَكۡفُرۡ﴾

{Wala hao hawakumfundisha yeyote mpaka wamwambie: Hakika sisi ni mtihani; basi usikufuru}, [Al-Baqarah: 102],

Na [imekuja] katika hadithi:

«**Atakayemwendea kuhani au mtazamiaji, na akamsadikisha kwa anayoyasema; basi hakika [kwa hilo] ameyakufuru aliyo teremshiwa Muhammad**», imepokewa na Ahmad.

Na atakayemtaka mchawi kuwafanyia vitimbi wengine, uharibifu wa vitimbi vyake utamrudia mwenyewe, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَلَا يَحِيقُ ٱلۡمَكۡرُ ٱلسَّيِّئُ إِلَّا بِأَهۡلِهِۦ﴾

{Na vitimbi viovu havimsibu ila mwenyewe aliyevifanya}, [Faatwir: 43].

Na dhuluma haikingwi kwa dhuluma, na giza la uchawi

linakingwa na nuru ya Qur-ani, wala si uchawi mfano wake,

﴿وَنُنَزِّلُ مِنَ ٱلْقُرْءَانِ مَا هُوَ شِفَآءٌ وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ﴾

{Na tunateremsha katika Qur'ani yaliyo ni matibabu na rehema kwa Waumini} [Al-Israa: 82].

Basi ewe Muisilamu ihifadhi itikadi yako; kwani hiyo ndiyo kitu cha thamani zaidi unacho kimiliki, na cha ghali zaidi unacho jichumia, na ushirikina unazima nuru ya umbile, nayo ndio sababu ya uovu, na kutawaliwa na maadui.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim '***

﴿فَٱسْتَمْسِكْ بِٱلَّذِىٓ أُوحِىَ إِلَيْكَ ۖ إِنَّكَ عَلَىٰ صِرَٰطٍ مُّسْتَقِيمٍ * وَإِنَّهُۥ لَذِكْرٌ لَّكَ وَلِقَوْمِكَ ۖ وَسَوْفَ تُسْـَٔلُونَ﴾

{Basi yashike yaliyo funuliwa kwako. Hakika wewe uko kwenye Njia Iliyo Nyooka * Na hakika haya ni ukumbusho kwako na kwa kaumu yako. Na mtakuja ulizwa}. [Az-zukhruf: 43-44].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur’ani tukufu…

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii, enyi Waislamu:**

Nguzo ya pili baada ya Shahada mbili ni: Swala nayo ndio ya kwanza atakayo hesabiwa kwayo mja siku ya Kiyama, basi usidharau kuitekeleza pamoja na jamaa ya Waislamu, wala usiutangulize uvivu mbele ya kumtii Mola Mlezi wa walimwengu, wala usipatie mgongo yale Allah kawaandalia wenye kuihifadhi miongoni mwa vipawa vingi, na kadri ya mafungamano ya mja na Mola wake Mlezi ndio milango ya heri itamfungukia, na epuka madhambi na maasi, kwani hayo yanakufanyia utiifu kuwa mzito.

Na kulingania kwa Allah kuna kuipa Dini ushindi, na kuwaiga Manabii na Mitume, nao [ulinganizi] ndio kauli njema zaidi na karimu zaidi, na [katika ulinganizi] chunguza ugonjwa, na uwekee dawa inayo nasibiana nao, na zijue hali za walinganiwa na wanayo yahitaji, na himili hamu za watu, wala usiwabebeshe watu hamu zako.

Na kithirisha toba na istighfari, kwani mazingatio ni ukamilifu wa mwishoni, wala si upungufu wa mwanzoni, na alama ya kukubaliwa kwa jema: ni kufuatisha jema jema lengine, Qatada Allah amrehemu amesema: "Hakika hii Qur-ani inawajulisha ugonjwa wenu na dawa yenu, ama ugonjwa wenu ni madhambi, na ama dawa yenu ni istighfari", nayo ni sababu ya kuingia Peponi, na kuzidi kwa nguvu na maandalizi mema, na kukinga

balaa, Abu Al-Minhaal Allah amrehemu amesema: "Mja hajawa na jirani kaburini mwake anayependeza zaidi kuliko istighfari."

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wenu…

# KUSHIKAMANA NA TAWHIDI[1]

Sifa njema zote anastahiki Allah aliyepwekeka na ukamilifu, kubaki, ushindi na kiburi, aliyesifika na Sifa njema zaidi na Majina mazuri zaidi, aliyetakasika kutokana na mifano na washirika, namhimidi Yeye aliyetakasika kwa [neema] alizotoa.

Na nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika naye, Mjuzi wa siri na minong'ono.

Na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, aliyetumilizwa na njia nyeupe na Sheria ya kuheshimika, swala na salamu za Allah zimshukie yeye, jamaa zake na Masahaba wake wachamngu, swala na salamu za kudumu zenye kuambatana hadi siku ya kufufulia na Malipo.

**Ama baada ya himdi hii:**

Mcheni Allah - enyi waja wa Allah - haki ya kumcha, na tendeni amali kwa ajili ya siku ambayo zitadhiri ndani yake siri, na yatadhihiri ndani yake yaliyofichwa na vifua na dhamiri.

**Enyi Waislamu:**

Hakika watu walikuwa umma mmoja wakiwa juu ya haki, kwa ajili ya umbile la Uisilamu ambalo Allah aliingiza ndani yao, na kwa aliyowausia katika uongofu na ubainifu, na pindi mda ulipokuwa mrefu kwao athari za Al-Haniifiyyah [mila ya Tawhidi] zilifutika, na yakawaingilia michangamanyiko iliochafua itikadi, na kuharibu usafi wake, basi wakaingia katika ushirikina, na wakapeleka aina mbali mbali za ibada kwa wasiokuwa Allah, ukapasuka umoja wao, na zikatofautiana kauli zao.

Basi Allah akatumiliza Manabii, wakiwa wenye kubashiria [watiifu] na kuonya [wahalifu]; ili watu wasiwe na hoja kwa

1 Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe ishirini na nne, mwezi wa Dhul-Qa'adah, mwaka elfu moja mia nne na kumi na tisa hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

Allah baada ya [kuja kwa] Mitume, na akatumilizwa Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie, kwa umma uliokuwa ukiishi ndani ya ujahilia ulionoga, na upotevu wa kichongo; ukiwa ushirikina ndio msingi wa Dini yao, na masanamu ndio miungu yao na mabwana wao, basi akawalingania katika Dini ya Tawhidi, iliokwisha simama dalili zake, iliowekwa wazi na aya na ikathibitishwa na hoja.

Na [Suala zima la] Itikadi wanahotubiwa nalo Waumini; ili wazidi Imani pamoja na Imani yao, kama alivyosema aliyetukuka:

﴿يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ ءَامِنُواْ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ
وَٱلْكِتَـٰبِ ٱلَّذِى نَزَّلَ عَلَىٰ رَسُولِهِۦ وَٱلْكِتَـٰبِ ٱلَّذِىٓ أَنزَلَ مِن قَبْلُ﴾

{Enyi mlio amini! Muaminini Allah, na Mtume wake, na Kitabu alicho kiteremsha juu ya Mtume wake, na Kitabu alicho kiteremsha kabla yake}, [An-Nisa`: 136]

Na ili wapate utulivu katika kuitekeleza Dini yao, na watahadhari upungufu au kasoro ndani yake; bali Allah amewaamrisha Manabii na Mitume wake kuutema na kuukana ushirikina na watu wake - na hasha wao kufanya hilo-;

[Allah] aliyetukuka na aliye juu amesema:

﴿وَإِذْ بَوَّأْنَا لِإِبْرَٰهِيمَ مَكَانَ ٱلْبَيْتِ أَن لَّا تُشْرِكْ بِى شَيْـًٔا
وَطَهِّرْ بَيْتِىَ لِلطَّآئِفِينَ وَٱلْقَآئِمِينَ وَٱلرُّكَّعِ ٱلسُّجُودِ﴾

{Na pale tulipomweka Ibrahim pahala penye ile Nyumba tukamwambia: Usinishirikishe na chochote; na isafishe Nyumba yangu kwa ajili ya wanao izunguka kwa kutufu, na wanaokaa hapo kwa ibada, na wanaorukuu, na wanaosujudu}, [Al-Hajj: 26].

Na [Allah] mwenye ushindi na utukufu alisema kumwambia mteule wa viumbe vyake Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie:

﴿وَٱدْعُ إِلَىٰ رَبِّكَ ۖ وَلَا تَكُونَنَّ مِنَ ٱلْمُشْرِكِينَ﴾

{Na lingania kwa Mola wako Mlezi, wala usiwe miongoni mwa washirikina} [Al-qaswas: 87].

Na akasema tena kumwambia:

﴿فَلَا تَدۡعُ مَعَ ٱللَّهِ إِلَٰهًا ءَاخَرَ فَتَكُونَ مِنَ ٱلۡمُعَذَّبِينَ﴾

{Basi usimwombe muabudiwa mwingine pamoja na Allah ukawa miongoni mwa watakao adhibiwa} [Ash-shuaraa`: 213].

Na wamehutubiwa nayo [Tawhidi] watu wa upotevu ili wafuate njia ya uongofu, akasema [Allah] aliye mtukufu wa shani:

﴿قُلۡ يَٰٓأَهۡلَ ٱلۡكِتَٰبِ تَعَالَوۡاْ إِلَىٰ كَلِمَةٍ سَوَآءِۭ بَيۡنَنَا وَبَيۡنَكُمۡ أَلَّا نَعۡبُدَ إِلَّا ٱللَّهَ وَلَا نُشۡرِكَ بِهِۦ شَيۡـٔٗا وَلَا يَتَّخِذَ بَعۡضُنَا بَعۡضًا أَرۡبَابٗا مِّن دُونِ ٱللَّهِۚ فَإِن تَوَلَّوۡاْ فَقُولُواْ ٱشۡهَدُواْ بِأَنَّا مُسۡلِمُونَ﴾

{Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Njooni kwenye Neno lilio sawa baina yetu na nyinyi: Ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Allah, wala tusimshirikishe na chochote; wala tusifanyane sisi kwa sisi kuwa Waola Walezi badala ya Allah. Na wakigeuka basi semeni: Shuhudieni ya kwamba sisi ni Waislamu} [Aalu-Imran: 64].

Wala hakuna ajabu ya hilo - enyi Waisilamu -; kwani kumpwekesha Allah kwa ibada ndio msingi wa Dini na miliki ya amri yote, juu yake [ya kuitekeleza] ndio kimewekwa kibula, na imeasisiwa mila [ya Uisilamu], hiyo ndio amri ya kwanza katika kitabu cha Allah, na kukataza ushirikina ndio katazo la kwanza katika Kitabu chake;

[Allah] aliyetukuka amesema:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ ٱعۡبُدُواْ رَبَّكُمُ ٱلَّذِي خَلَقَكُمۡ وَٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِكُمۡ لَعَلَّكُمۡ تَتَّقُونَ ۞ ٱلَّذِي جَعَلَ لَكُمُ ٱلۡأَرۡضَ فِرَٰشٗا وَٱلسَّمَآءَ بِنَآءٗ وَأَنزَلَ مِنَ ٱلسَّمَآءِ مَآءٗ فَأَخۡرَجَ بِهِۦ مِنَ ٱلثَّمَرَٰتِ رِزۡقٗا لَّكُمۡۖ فَلَا تَجۡعَلُواْ لِلَّهِ أَندَادٗا وَأَنتُمۡ تَعۡلَمُونَ﴾

{Enyi watu! Muabuduni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni nyinyi na wale wa kabla yenu, ili mpate kuokoka * (Allah) ambaye amekufanyieni hii ardhi kuwa tandiko, na mbingu kuwa

paa, na akateremsha maji kutoka mbinguni, na kwayo akatoa matunda yawe riziki zenu. Basi msimfanyizie Allah washirika, na hali nyinyi mnajua} [Al-Baqarah: 21-22]

Na kuingia katika Dini ya Allah hakusihi ila kwa kutangaza kupwekeka kwa Allah, nalo ndilo jambo la mwisho anatoka nalo Muisilamu duniani; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema:

«**walakinisheni maiti wenu 'laa ilaaha illa llaah'**», imepokewa na Muslim.

Kuingia katika kinyume chake [Tawhidi] ni dhambi kubwa kuliko hata kuuwa watoto, ibnu Mas-uud Allah amridhie anasema:

«**nilimuuliza Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie: Ni dhambi gani kubwa zaidi mbele ya Allah? Akasema: Ni kumfanyia Allah mshirika hali Yeye ndiye aliyekuumba. Nikasema: Kisha ni gani? Akasema: Ni umuuwe mwanako kwa kuhofia asije kula nawe**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea;

Kwa sababu hiyo ndio makatazo ya ushirikina yanasisitizwa katika Qur-ani, na maamrisho ya Tawhidi yamekaririwa, Allah amelidhihirisha hilo na amelirudia rudia, na akalipigia mifano.

Na amri ya kumuabudu Allah ndio mwanzo wa ulinganizi wa Mitume; Kipenzi cha Allah [Nabii Ibrahim] alianza kumlingania babake na hilo:

﴿إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ يَـٰٓأَبَتِ لِمَ تَعْبُدُ مَا لَا يَسْمَعُ وَلَا يُبْصِرُ وَلَا يُغْنِي عَنكَ شَيْـًٔا﴾

{Ewe baba yangu! Kwa nini unaabudu visivyosikia, na visivyoona, na visivyokufaa chochote?} [Maryam: 42],

Na Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie aliwalingania watu katika Tawhidi kwa miaka kumi kabla ya kufaradhishiwa ya faradhi, ili kuiadhimisha shani yake [Tawhidi].

[Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie aliwapa mwongozo walinganizi ya kuwa jambo la Tawhidi liwe mwanzo

wa ulinganizi wao, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema kumwambia Muadh Allah amridhie alipomtuma Yemen:

«**Hakika wewe unaiendea kaumu miongoni mwa watu wa Kitabu [kutoka mbinguni]; basi walinganie kushuhudia ya kwamba hapana anayepasa kuabudiwa ila Allah, na kwamba mimi ni Mtume wa Allah**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Kiongozi wa watu wa Tawhidi Ibrahim salamu zimahukie alimuomba Mola wake Mlezi kwa kauli yake:

﴿وَٱجۡنُبۡنِي وَبَنِيَّ أَن نَّعۡبُدَ ٱلۡأَصۡنَامَ﴾

{na uniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu} [Ibrahim: 35],

Ibrahim At-Taymii alisema: "basi ni nani atahisi kusalimika kutokana na balaa [ya ushirikina] baada ya Ibrahim?!"

Manabii waliwausia watoto wao kukita juu ya Dini sahihi na itikadi safi [iliyosalimika na uchafu wa ushirikina] hadi kufikia kifo:

﴿وَوَصَّىٰ بِهَآ إِبۡرَٰهِـۧمُ بَنِيهِ وَيَعۡقُوبُ يَٰبَنِيَّ إِنَّ ٱللَّهَ ٱصۡطَفَىٰ لَكُمُ ٱلدِّينَ
فَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنتُم مُّسۡلِمُونَ﴾

{Na Ibrahim akawausia wanawe, na pia Yaaqub: Enyi wanangu! Hakika Allah amekuteulieni Dini hii; basi msife ila nanyi mmekuwa Waislamu, wanyenyekevu}, na Manabii waliwauliza watoto wao kulihusu hali wao wamo katika tandiko la mauti [katika ya kufariki]: [Al-Baqarah: 132],

﴿أَمۡ كُنتُمۡ شُهَدَآءَ إِذۡ حَضَرَ يَعۡقُوبَ ٱلۡمَوۡتُ إِذۡ قَالَ لِبَنِيهِ مَا تَعۡبُدُونَ مِنۢ بَعۡدِيۖ
قَالُواْ نَعۡبُدُ إِلَٰهَكَ وَإِلَٰهَ ءَابَآئِكَ إِبۡرَٰهِـۧمَ وَإِسۡمَٰعِيلَ وَإِسۡحَٰقَ إِلَٰهٗا وَٰحِدٗا وَنَحۡنُ لَهُۥ مُسۡلِمُونَ﴾

{Je! Mlikuwapo yalipomfikia Yaaqub mauti, akawaambia wanawe: Mtamuabudu nani baada yangu? Wakasema: Tutamuabudu Muabudiwa wako na Muabudiwa wa baba zako, Ibrahim na Ismail na Is- hak, Muabudiwa Mmoja tu,} [Al-Baqarah: 133],

**Enyi Waislamu**:

Uongofu ndio lengo kubwa zaidi, na kuupata ndio kipawa kitukufu zaidi, na kusalimika kwa itikadi ndio ngome ya amani wakati wa mazito:

﴿ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَلَمۡ يَلۡبِسُوٓاْ إِيمَٰنَهُم بِظُلۡمٍ أُوْلَٰٓئِكَ لَهُمُ ٱلۡأَمۡنُ وَهُم مُّهۡتَدُونَ﴾

{Wale ambao wameamini, na hawakuchanganya imani yao na dhulma - hao ndio watakaopata amani na wao ndio walioongoka}, [Al-an`aam: 82],

Na kuelekea kwa Allah peke yake ndio njia [ya kuokoka] wakati wa mafuriko ya fitina, mitihani na majanga; Allah mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿وَذَا ٱلنُّونِ إِذ ذَّهَبَ مُغَٰضِبٗا فَظَنَّ أَن لَّن نَّقۡدِرَ عَلَيۡهِ فَنَادَىٰ فِي ٱلظُّلُمَٰتِ

أَن لَّآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنتَ سُبۡحَٰنَكَ إِنِّي كُنتُ مِنَ ٱلظَّٰلِمِينَ * 

فَٱسۡتَجَبۡنَا لَهُۥ وَنَجَّيۡنَٰهُ مِنَ ٱلۡغَمِّۚ وَكَذَٰلِكَ نُـۨجِي ٱلۡمُؤۡمِنِينَ﴾

{Na Dhun-Nun alipoondoka hali ameghadhibika, na akadhani ya kwamba hatutakuwa na uwezo juu yake. Basi aliita katika giza: Hapana muabudiwa wa haki isipokuwa Wewe, Uliye takasika [na kila aibu na kasoro]. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu * Basi tukamwitikia na tukamwokoa kutokana na dhiki. Na hivyo ndivyo tunavyo waokoa Waumini} [Al-Anbiya`: 87-88].

Usafi wa itikadi unasahihisha nia, na unayafunga matamanio hatamu, unaibarikisha amali, na unadumisha utajo [mwema], basi ni wapi na wapi sera ya Abu Jahli na sera ya Abu Bakr?! Na ni wapi na wapi nasaba ya Bilali na Abu Lahab?! Katika hasara ya Dini haichukuliwi fidiya hata lau ni ya dhahabu:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ وَمَاتُواْ وَهُمۡ كُفَّارٞ

فَلَن يُقۡبَلَ مِنۡ أَحَدِهِم مِّلۡءُ ٱلۡأَرۡضِ ذَهَبٗا وَلَوِ ٱفۡتَدَىٰ بِهِۦٓ﴾

{Hakika wale walio kufuru, na wakafa hali ni makafiri haitakubaliwa kutoka kwa yeyote wao fidia ya dhahabu ya kujaza dunia nzima lau wangeli itoa} [Aalu-Imran: 91].

**Enyi Waisilamu:**

Nyumba ya Allah ya kale imejengwa kwa ajili ya kusimamisha Tawhidi, vizazi vinafuatana katika kuihiji, na Waisilamu wanashindana katika kufika kwenye kumbi zake, kingizoni mwake mna Imani, na ndani ya kumbi zake mna amani na utulivu

﴿وَإِذۡ بَوَّأۡنَا لِإِبۡرَٰهِيمَ مَكَانَ ٱلۡبَيۡتِ أَن لَّا تُشۡرِكۡ بِي شَيۡـٔٗا﴾

{Na pale tulipomweka Ibrahim pahala penye ile Nyumba tukamwambia: Usinishirikishe na chochote} [Al-Hajj: 26],

Na mnao katika alama ya Hija kumkanushia Allah Ushirika: "Labbayka laa shariika lak" [nakuitikia, hauna mshirika nawe", na Dua bora zaidi ni Dua ya siku ya Arafa; ambayo ni kunyanyua Tawhidi; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Dua bora zaidi ni Dua ya siku ya Arafa, na bora zaidi niliyoyasema mimi na Manabii kabla yangu: *'Laa ilaaha illa llaahu wahadahuu laa shariika lah, lahul mulku, walahul hamd, wa huwa alaa kulli shay-in qadiir'***», imepokewa na Tirmidhi.

Na Tawhidi iliyotakaswa ndio msingi wa jumbe zote zilizotoka mbinguni, na msingi wa Mila [ya Uisilamu], nayo ndiyo hakika ambayo ni juu yetu tuwe na ghera nayo na tuilinde kutokana na kila lenye kuichafua; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَلَقَدۡ بَعَثۡنَا فِي كُلِّ أُمَّةٖ رَّسُولًا أَنِ ٱعۡبُدُواْ ٱللَّهَ وَٱجۡتَنِبُواْ ٱلطَّٰغُوتَ﴾

{Na kwa hakika kwa kila umma tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Allah, na muepukeni Shetani} [An-Nahl: 36].

**Enyi waja wa Allah:**

[Mtume] Mteule swala na salamu za Allah zimshukie alisimamisha ulinganizi wake juu ya Neno la Ikhlasi, na Ibrahim salamu zimshukie alilifanya [Neno hili] kuwa ni lenye kubaki katika kizazi chake, na hawajawahi kutamka wenye kutamka [Neno] zuri zaidi kuliko *'laa ilaaha illa llaah'*; kulitendea kazi

ndio thamani ya Pepo, lau litapimwa na mbingu na ardhi basi litazishinda, ibnu Uyeina Allah amrehemu amesema: "Allah hajawahi kumneemesha mja kati ya waja na neema kubwa zaidi kuliko Yeye kuwatambulisha: laa ilaaha illa llaah."

**Haya yaliotangulia,**

Na hakika kulitamka [Neno la Tawhidi] kwa ulimi haifaidishi ila kwa aliyejua maana yake ya kukanusha na kuthibitisha, na akatekeleza masharti yake: elimu na yakini ya maana yake, na ikhlasi na ukweli katika kuitendea kazi, na kupenda, kuandama na kukubali yaliojulishwa nalo, na kukufuru yenye kuabudiwa kinyume na Allah.

**Enyi Waisilamu:**

Tawhidi na Shirki ni kitu na kinyumeche, hazikutani pamoja - ni kama usiku na mchana -, basi pindi itapatikana shirki imani inaondoka, na hakika Allah amekutukuza na amekulinda na jambo la kuudhalilisha moyo wako na uso wako kwa asiyekuwa Yeye, naye [Allah] anakuita katika kumuelekea Yeye; basi uelekeze uso wako kwake peke yake, wala usiangushe jicho lako chini, wala usimuabudu asiyekuwa Mola Mlezi wa ardhi na mbingu, ni wapi na wapi baina ya anayemuomba aliye hai ambaye hafi, na yule anayemuomba maiti na kufungamana na mifupa iliyokuwa mchanga na iliyochakaa ndani ya makaburi?!

**Enyi Waisilamu:**

Ole wako na kumchinjia asiyekuwa Allah, kwani kuchinja ni ibada anayostahili kufanyiwa Allah peke yake, na kumchinjia asiyekuwa Allah ni ushirikina; kwani Allah ndiye Mola wako Mlezi aliyekuumba, naye ndiye aliyekuruzuku mnyama unayemchinja; basi usimchinje ila kwa ajili ya yule aliyekuumba wewe na yeye:

﴿فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَٱنۡحَرۡ﴾

{Basi swali na uchinje kwa ajili ya Mola wako Mlezi} [Al-kauthar: 2].

Na usiape ila na Allah mwenye ushindi na utukufu; kwani Allah ndiye aliye kutamsha, basi mshukuru Yeye pekee na usiape na asiye kuwa Yeye; basi usiape na Nabii, wala walii, wala neema, wala uhai wa kiumbe; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Atakaye apa na asiyekuwa Allah, basi kwa hakika amekufuru au ameshirikisha**», imepokewa na Tirmidhi.

Na vikuku, nyuzi na hirizi ni viumbe visivyo na uhai, na wewe ni kiumbe chenye uhai, basi ihurumie nafsi yako, usidunishe hadhi yako baada ya Allah kukupa ushindi na kukunyanyua, usikusudie kisicho uhai ukakibeba katika kifua chako au mkono wako, kwa madai ya kukinga na shari au kuvuta heri au kukinga na jicho, na Allah aliyetukuka anasema:

﴿وَإِن يَمْسَسْكَ ٱللَّهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهُۥٓ إِلَّا هُوَ ۖ وَإِن يُرِدْكَ بِخَيْرٍ فَلَا رَآدَّ لِفَضْلِهِۦ﴾

{Na Allah akikugusisha madhara, basi hapana wa kukuondolea ila Yeye. Na akikutakia heri, basi hapana awezaye kurudisha fadhila yake}, [Yunus: 107],

Na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie amesema:

«**Atakaye funga hirizi basi ameshirikisha**», imepokewa na Ahmad, na jifunge na Yeye [Allah] peke yake, na mtegemezee mambo yako yote.

**Enyi Waislamu:**

Baadhi ya watu wamekosa kujua hekima ya wao kuumbwa, basi wakapepetwa na uzushi, na wakatawaliwa na fitina na maradhi, baadhi yao wakafitinika na wachawi, wapiga ramli na wazushi wakubwa, kwa madai ya kujua ghaibu na kuangalia mustakbali, na hawakuvuna kutokana na hayo ila upotevu na kusambaratisha mali katika batili, na Allah kasha bainisha haki katika hilo kwa kauli yake:

﴿قُل لَّا يَعْلَمُ مَن فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ٱلْغَيْبَ إِلَّا ٱللَّهُ﴾

{Sema: Hapana katika mbingu na ardhi ajuaye ya ghaibu isipokuwa Allah} [An-Naml: 65], na Nabii swala na salamu za

Allah zimshukie anasema:

«**Atakayemwendea kuhani au mcheza ramli, na akamsadikisha kwa anayoyasema; basi hakika [kwa hilo] ameyakufuru aliyoteremshiwa Muhammad**», imepokewa na Ahmad.

Na baadhi ya watu wakafitinika na wanayo yaita 'Twali'a' [nyota], 'Abraaj' [mapito ya nyota], hadhi, kuhudhurisha roho, na kusoma kiganja cha mkono; basi wakasibiwa na mafuriko ya mawazo yasio na uhakika, na kutoridhia kadari, [Allah] mweye ushindi na utukufu amesema:

﴿أَمۡ عِندَهُمُ ٱلۡغَيۡبُ فَهُمۡ يَكۡتُبُونَ﴾

{Au iko kwao ghaibu, basi wao wanaiandika [kwa watu na kuwapa habari yake]?!} [At-Tuur: 41].

**Enyi waja wa Allah:**

Ikhlasi ndio taji la amali; na atakaye mshirikisha Allah pamoja na wengine basi Allah ni Mkwasi wa wakwasi asiyehitajia shirika, wala haridhii kwa waja wake ukafiri, basi ole wao wenye kujionyesha [na amali zao]! Si dunia wameichuma wala si akhera wameitendea, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema:

«**mwenye kujidhihirisha kuwa amejaa jambo ambalo hajapewa [hanalo] ni kama aliyevaa nguo mbili za uongo**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Hakika yamepotea matarajio ya wenye kujionyesha, na zimeambulia patupu mbio zao, wamefedheheshwa duniani, wala hawakupata malipo mema akhera, basi tahadharini tena tahadharini kujionyesha [na amali] na kutaka kuskika [nayo], kwani wa kwanza atakaye chomwa na Moto siku ya Kiyama ni wenye kujionyesha na amali zao.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿وَمَآ أُمِرُوٓاْ إِلَّا لِيَعۡبُدُواْ ٱللَّهَ مُخۡلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ حُنَفَآءَ

وَيُقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَيُؤۡتُواْ ٱلزَّكَوٰةَۚ وَذَٰلِكَ دِينُ ٱلۡقَيِّمَةِ﴾

{Nao hawakuamrishwa kitu ila wamuabudu Allah kwa kumtakasia Dini, wawe waongofu, na wasimamishe Swala na hiyo ndio Dini Madhubuti} [Al-Bayyinah: 5].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anazistahiki Allah, ambaye kwa neema yake wameongoka walioongoka, na kwa uadilifu wake wamepotea waliopotea, namhimidi Yeye aliyetakasika himdi kutoka kwa mja aliyemtakasa Mola wake Mlezi kutokana wanayomsemea madhalimu.

Na nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika naye, na ametakasika Allah Mola Mlezi wa Arshi kutokana na wanayomsifu nayo [wapotevu].

Na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake na kipenzi chake, mkweli muaminifu, ewe Allah mswalie na msalimie yeye na jamaa zake na masahaba wake, ambao wameshikamana na uongofu wake, na wanatembea juu ya njia yake.

**Ama baada ya himdi hii, enyi Waisilamu:**

Imani si bidhaa ndogo, au madai tu na majina, hakika si mengine Imani ya haki ni: Itikadi iliosalimika, amali iliyo sahihi, kupenda na kunusuru kwa ajili yake na kuchukia na kupiga vita kwa ajili yake, mandhari ya dhahiri na uhakika wa batini, kutoa msaada na kuzuilia udhia.

Na kuitekeleza Tawhidi inahitajia uangalifu wa moyo wenye kufululiza na kudumu, unaoiondolea nafsi kila fikra inayotia dosari katika ibada ya Allah.

Na aliye ingia katika mashimo ya shirki kubwa; akataka kutoka kwa wafu kuondoshewa ufakiri au maradhi, au akataka kutoka kwao manufaa - kama kupata mali au mtoto -, au akataka msaada kutoka kwa walio makaburini [wafu], au akayatufu, au akayachinjia au akayatilia nadhiri; basi atakuwa amevunja heshima ya Ulezi wa Allah, na ametia kasoro haki Yake ya ibada, na amekuwa na dhana mbovu kwa Mola Mlezi wa viumbe, na ameparaga dhambi kubwa zaidi mbele ya Allah, na

ataharamishiwa Pepo na atatiwa milele Motoni:

﴿إِنَّهُۥ مَن يُشۡرِكۡ بِٱللَّهِ فَقَدۡ حَرَّمَ ٱللَّهُ عَلَيۡهِ ٱلۡجَنَّةَ وَمَأۡوَىٰهُ ٱلنَّارُۖ وَمَا لِلظَّٰلِمِينَ مِنۡ أَنصَارٖ﴾

{Kwani anaye mshirikisha Allah, hakika Allah atamharimishia Pepo, na mahala pake ni Motoni. Na walio dhulumu hawatakuwa na wa kuwanusuru} [Al-Maaidah: 72].

Basi fuata njia ya haki, na andama mfumo wa uongofu, na fanya bidii kuihifadhi itikadi yako; kuwa hakuna mwenye kuokoa na adhabu ya Allah ila Allah, wala hayapatikani [mazuri] yalio kwake ila kwa kumfanyia ikhlasi peke yake, na kwa kutenda aliyowaamrisha waja wake wajikurubishe nayo kwake.

Na Tawhidi ni mlango wa matarajio pindi maisha yamekuwa giza, wala hutapata matakwa yako hadi umpwekeshe Mmoja wa pekee [Allah] katika kauli zako zote na matendo yako yote:

﴿أَلَآ إِلَى ٱللَّهِ تَصِيرُ ٱلۡأُمُورُ﴾

{Jueni kuwa mambo yote yanarudi kwa Allah}, [Ash-shuraa: 53],

Na watu wote watarudi kwa Mola wao.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wenu...

# MATUNDA YA TAWHIDI[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakaye mpoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Basi mcheni Allah - enyi waja wa Allah - hakika ya uchamngu; kwani uchaji Allah ndio njia ya uongofu, na kuihalifu ndio njia ya uovu.

**Enyi Waisilamu:**

Allah amepwekeka na Tawhidi, na ameitakasa nafsi yake kutokana na kuwa na mshirika na mfano, na amewaamrisha waja wake wamuabudu Yeye pekee, na akawaekea ibada aina tofauti, na akajaalia kumpwekesha Yeye kwa ibada ndio asili ya Dini na msingi wake, na nguzo yake ya kwanza, nayo ni yenye kukusanya heri, wala halikubaliwi jema lolote ila kwayo [inapofanywa kwa Tawhidi], na amali chache inapokuwa nayo inazidishwa maradufu, na inapokosekana basi amali njema zinaporomoshwa hata kama ni kubwa mfano wa majabali.

Nayo ndio mwanzo wa ulinganizi wa Mitume na uhalisi wake, na kwa ajili yake ndio wametumilizwa; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَمَآ أَرۡسَلۡنَا مِن قَبۡلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِيٓ إِلَيۡهِ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنَا۠ فَٱعۡبُدُونِ﴾

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe tisa, mwezi wa Jumaada Al-Akhir, mwaka elfu moja mia nne na thalathini na nne hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

{Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu}. [Al-Anbiya: 25].

Kila aya katika Kitabu cha Allah iko wazi kabisa katika kuibainisha [Tawhidi], au inaijulisha, au inabainisha yenye kuwajibishwa nayo, au thawabu zake, au kinyume chake. Amri ya kwanza katika Kitabu cha Allah: Ni kuiamrisha hiyo; [Allah] mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿يَـٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ ٱعۡبُدُواْ رَبَّكُمُ﴾

{Enyi watu! Muabuduni Mola wenu Mlezi}, [Al-Baqarah: 21]. yaani: Mpwekesheni.

Muisilamu katika kila swala anamuahidi Mola wake Mlezi kusimama nayo [kuitekeleza]:

﴿إِيَّاكَ نَعۡبُدُ وَإِيَّاكَ نَسۡتَعِينُ﴾

{Wewe peke yako tunakuabudu}, yaani: hatumwabudu asiyekuwa Wewe, {na kutoka kwako peke yako tunataka msaada}. [Al-Fatiha: 5].

Nayo [Tawhidi] ni haki ya Allah juu ya waja wake, na ndiyo wajibu wa kwanza miongoni mwa majukumu ya Dini; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema kumwambia Muadh Allah amridhie:

«**basi liwe la kwanza utakalo walingania kwalo ni: Kumwabudu Allah**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, na la kwanza atakaloulizwa mja ndani ya kaburi lake ni:

«**Ni nani Mola wako Mlezi?** - yaani: Ni nani muabudiwa wako? -».

Na kwa ajili ya umuhimu wake, na kuwa hakuna njia ya kumridhisha Mola Mlezi ila hiyo, kiongozi wa watu wa Tawhidi [Ibrahim] alijiobea nafsi yake na kizazi chake kupata kukita juu ya Tawhidi, akasema:

﴿رَبَّنَا وَٱجۡعَلۡنَا مُسۡلِمَيۡنِ لَكَ وَمِن ذُرِّيَّتِنَآ أُمَّةٗ مُّسۡلِمَةٗ لَّكَ﴾

{Ewe Mola Mlezi wetu! Tujaalie tuwe ni wenye kusilimu kwako}, [Al-Baqarah: 128], na Yusuf salamu zimshukie alimuomba Mola wake Mlezi akasema:

﴿تَوَفَّنِي مُسۡلِمٗا وَأَلۡحِقۡنِي بِٱلصَّٰلِحِينَ﴾

{Nifishe hali ya kuwa ni Muislamu na nichanganyishe na watendao mema}. [Yusuf: 101].

Na ni katika Dua za Nabii wetu swala na salamu za Allah zimshukie:

«**Ewe mwenye kuzigeuza geuza nyoyo! Ukitishe moyo wangu juu ya Dini yako**», imepokewa na Ahmad.

Nayo ndio wasia wa Mitume:

﴿وَوَصَّىٰ بِهَآ إِبۡرَٰهِـۧمُ بَنِيهِ وَيَعۡقُوبُ يَٰبَنِيَّ إِنَّ ٱللَّهَ ٱصۡطَفَىٰ لَكُمُ ٱلدِّينَ فَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنتُم مُّسۡلِمُونَ﴾

{Na Ibrahim akawausia wanawe, na pia Yaaqub: Enyi wanangu! Hakika Allah amekuteulieni Dini hii; basi msife ila nanyi mmekuwa Waislamu, wanyenyekevu}. [Al-Baqarah: 132].

Mfumo wa Mitume ni kuifundisha [Tawhidi] kwa watoto wao, na kuwauliza kuihusu wakiwa katika mauti; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿أَمۡ كُنتُمۡ شُهَدَآءَ إِذۡ حَضَرَ يَعۡقُوبَ ٱلۡمَوۡتُ إِذۡ قَالَ لِبَنِيهِ مَا تَعۡبُدُونَ مِنۢ بَعۡدِيۖ قَالُواْ نَعۡبُدُ إِلَٰهَكَ وَإِلَٰهَ ءَابَآئِكَ إِبۡرَٰهِـۧمَ وَإِسۡمَٰعِيلَ وَإِسۡحَٰقَ إِلَٰهٗا وَٰحِدٗا وَنَحۡنُ لَهُۥ مُسۡلِمُونَ﴾

{Je! Mlikuwapo yalipomfikia Yaaqub mauti, akawaambia wanawe: Mtamuabudu nani baada yangu? Wakasema: Tutamuabudu Muabudiwa wako na Muabudiwa wa baba zako, Ibrahim na Ismail na Is- hak, Muabudiwa Mmoja tu, na sisi tunasilimu kwake}. [Al-Baqarah: 133].

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akiwafundisha watoto wa masahaba kufungamana na Allah peke yake pasina wengineo; alisema kumwambia ibni Abbaas Allah amridhie yeye na babake:

«**Ewe kijana! Mimi nakufundisha maneno; mhifadhi Allah**

**naye atakuhifadhi, mhifadhi Allah utamkuta mbele yako, pindi unapoomba basi muombe Allah, na pindi unapotaka msaada basi taka kutoka Allah**», imepokewa na Tirmidhi.

Allah alituamrisha tusife ila [tukiwa] juu yake:

﴿يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱتَّقُواْ ٱللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِۦ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنتُم مُّسۡلِمُونَ﴾

{Enyi mlio amini! Mcheni Allah kama ipasavyo kumcha; wala msife ila nanyi ni Waislamu} [Aalu-Imran: 102].

Kwa kumpwekesha Allah kwa ibada, kifua kinapata ukunjufu, moyo unapata utulivu, na mja anajikomboa na utumwa wa viumbe:

﴿فَمَن يُرِدِ ٱللَّهُ أَن يَهۡدِيَهُۥ يَشۡرَحۡ صَدۡرَهُۥ لِلۡإِسۡلَٰمِ﴾

{Basi yule ambaye Allah anataka kumhidi humfungulia kifua chake kwa Uislamu}. [Al-an`aam: 125]

Na kwayo hamu zinapata faraja majanga yanaondoka:

﴿فَنَادَىٰ فِي ٱلظُّلُمَٰتِ أَن لَّآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنتَ سُبۡحَٰنَكَ إِنِّي كُنتُ مِنَ ٱلظَّٰلِمِينَ﴾

{Basi aliita katika giza: Hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Wewe Uliyetakasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu}, [Al-Anbiya : 87],

Ibnu Qayyim Allah amrehemu amesema: "Mazito hayajawahi kukingwa na mfano wa Tawhidi".

Inaondosha vifundo vya moyo na inausilihisha moyo; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Mambo matatu moyo ukiwa juu yake haubebi usaliti wala ghushi: kumtakasia Allah amali, kuwanasihi viongozi na kushikamana na jamaa, kwani dua yao [ya Jamaa] inawazunguka [kama ngome]**», imepokewa na Ahmad.

Nayo ni sababu ya maisha mazuri; bali haipatikani saada duniani ila kwayo; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿مَنۡ عَمِلَ صَٰلِحٗا مِّن ذَكَرٍ أَوۡ أُنثَىٰ وَهُوَ مُؤۡمِنٞ فَلَنُحۡيِيَنَّهُۥ حَيَوٰةٗ طَيِّبَةٗ﴾

{Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema}. [An-Nahl: 97].

Nayo ndio tegemeo la maisha inayotafutwa na nafsi:

﴿فَمَنِ ٱتَّبَعَ هُدَاىَ فَلَا يَضِلُّ وَلَا يَشْقَىٰ﴾

{basi atakaye ufuata uwongofu wangu, hatapotea wala hatataabika}. [Twaaha: 123]

Nayo ndiyo yenye kuleta umoja kwa Waisilamu - waarabu na wasiokuwa waarabu, wa mashariki na wamagharibi –

﴿إِنَّ هَٰذِهِۦٓ أُمَّتُكُمۡ أُمَّةً وَٰحِدَةً وَأَنَا۠ رَبُّكُمۡ فَٱعۡبُدُونِ﴾

{Kwa hakika huu umma wenu ni umma mmoja, na Mimi ni Mola wenu Mlezi. Kwa hivyo niabuduni Mimi}. [Al-anbiya: 92].

Ni Neno la Tawhidi Neno jema tukufu, msingi wake umekita na tagaa lake limeenda juu, nayo ni Neno la Allah liliojuu kabisa, na Allah alimzungumzisha nalo Musa moja kwa moja bila ya ukati:

﴿إِنَّنِيٓ أَنَا ٱللَّهُ لَآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنَا۠ فَٱعۡبُدۡنِي﴾

{Hakika Mimi ndiye Allah. Hapana apasaye kuabudiwa ila Mimi tu. Basi niabudu Mimi}. [Twaaha: 14].

Wala hakuna tagaa la Imani lililo juu zaidi kulililiko; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Imani ni matagaa sabiini na kitu - au: sitini na kitu -; lilio bora zaidi ni: *'laa ilaaha illa llaah'***», imepokewa na Muslim.

Nayo ndio maneno matakatifu zaidi, na kitu kizito zaidi katika mizani, na inalingana [katika thawabu] na kuacha huru watumwa, na ni kinga inayokinga kutokana na shetani kila siku;

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«***atakaye sema: 'laa ilaaha illa llaahu wahadahuu laa shariika lah, lahul mulku, walahul hamd, wa huwa a'laa kulli shay-in qadiir'*, mara mia moja kwa siku; itakuwa kwake ni sawa na kuacha huru watumwa kumi, ataandikiwa mema mia moja, atafutiwa maovu mia moja, itakuwa kwake ni kinga ya kumkinga na shetani siku yake ile hadi jioni, na hatakuja mtu [siku ya Kiyama] na jambo bora zaidi kuliko aliyokuja nayo yeye, ila mtu atakayefanya zaidi ya hivyo [alivyo fanya yeye]**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

«***Laa ilaaha illa llaah***», midomo haijawahi kunuketo, wala kutingisika na neno zuri kulililiko; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Bora zaidi niliyoyasema mimi na Manabii kabla yangu*: 'Laa ilaaha illa llaahu wahadahuu laa shariika lah, lahul mulku, walahul hamd, wa huwa a'laa kulli shay-in qadiir'***», imepokewa na Tirmidhi.

Neno na kudumu milele, Allah ameahidi kuwa kutabaki katika watu watakao lisema na kulilingania; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَجَعَلَهَا كَلِمَةً بَاقِيَةً فِي عَقِبِهِ﴾

{Na akalifanya hili liwe neno lenye kubaki katika vizazi vyake} [Az-zukhruf: 28].

Nayo ndio kauli madhubuti, mwenye kushikamana nayo Allah humfanya kuwa imara duniani na akhera; [Allah] mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿يُثَبِّتُ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا بِالْقَوْلِ الثَّابِتِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَفِي الْآخِرَةِ﴾

{Allah huwatia imara wenye kuamini kwa kauli ya imara katika maisha ya dunia na katika Akhera}. [Ibrahim: 27],

Na kiumbe mkamilifu zaidi ni yule aliyekamilika zaidi katika kumuabudu Yeye, na ukamilifu wa mja na utukufu wa cheo chake unakuwa kwa kadri ya kuitekeleza kwake Tawhidi, na Allah humtetea mtu wa Tawhidi katika Dini yake na dunia yake, na anayetarajiwa zaidi kupata msamaha wa Allah ni mtu wa Tawhidi;

Allah aliyetukuka amesema katika hadithi Qudsi:

«**lau utanijia na madhambi yaliokaribia kujaa ardhi, kisha ukakutana nami hali haunishirikishi na chochote, basi nitakujia na msamaha uliokaribia kujaa ardhi**», imepokewa na Tirmidhi, ibnu Rajab Allah amrehemu amesema: "Tawhidi ndio sababu kubwa; basi atakayeikosa amekosa msamaha, na atakayekuja nayo, basi hakika amekuja na sababu kubwa zaidi ya kupata msamaha ».

Shetani hana njia ya kughilibu mwenye Tawhidi:

﴿إِنَّهُۥ لَيۡسَ لَهُۥ سُلۡطَٰنٌ عَلَى ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَلَىٰ رَبِّهِمۡ يَتَوَكَّلُونَ﴾

{Hakika yeye hana madaraka juu ya walio amini na wakamtegemea Mola wao Mlezi} [An-Nahl: 99],

Na kinga ya Allah kwake inazidi kwa kadri ya Tawhidi yake, amesema aliyetakasika:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ يُدَٰفِعُ عَنِ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ﴾

{Hakika Allah huwakinga walio amini}. [Al-hajj: 38],

Aliyetekeleza Tawhidi ya Allah sawa sawa basi Allah atamhifadhi kutokana na madhambi ya kuangamiza na machafu, [Allah] alisema kuhusu Yusuf salamu zimshukie:

﴿كَذَٰلِكَ لِنَصۡرِفَ عَنۡهُ ٱلسُّوٓءَ وَٱلۡفَحۡشَآءَۚ إِنَّهُۥ مِنۡ عِبَادِنَا ٱلۡمُخۡلَصِينَ﴾

{Hayo hivyo ni kwa ajili tumuepushe na uovu na uchafu. Hakika yeye alikuwa katika waja wetu walio safishwa [Yusuf: 24].

Ibnul Qayyim Allah amrehemu amesema: "kila moyo unapokuwa dhaifu zaidi katika Tawhidi, na wenye shirki zaidi, basi utakuwa ni wenye machafu zaidi".

Mwenye Tawhidi ana utulivu katika maisha ya duniani, na ni mwenye kupata amani ndani yake kwa kadri ya Imani yake

﴿ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَلَمۡ يَلۡبِسُوٓاْ إِيمَٰنَهُم بِظُلۡمٍ أُوْلَٰٓئِكَ لَهُمُ ٱلۡأَمۡنُ وَهُم مُّهۡتَدُونَ﴾

{Wale ambao wameamini, na hawakuchanganya imani yao na dhulma - hao ndio watakao pata amani na wao ndio walioongoka}. [Al-an`aam: 82].

Na wafu wananufaika na maombi ya watu wenye Tawhidi, wala hayakubaliwi maombi katika swala ya janaza ila yao; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Hakuna mtu Muisilamu atakufa, na wasimame katika jeneza lake watu arubaini wasiomshirikisha Allah na kitu; isipokuwa Allah hukubali maombi yao kwake**», imepokewa na Muslim.

Na Allah humbashiria mtu wa Tawhidi Pepo pindi kinapokaribia kifo chake; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Yule yatakao kuwa maneno yake ya mwisho ni 'laa ilaaha illa llaah' ataingia Peponi**», imepokewa na Abu Daaud.

Na kama Allah alivyompa ushindi mtu wa Tawhidi duniani, basi hakika Allah atamkirimu na atanyanyua cheo chake akhera, na atamlipa malipo ya wenye kutenda amali yalio bora zaidi; basi atakayekufa juu ya Tawhidi atapata Pepo ima kutokea mwanzo au atamalizikia [humo], na hata akiingia Motoni kwa ajili ya madhambi yake hatabakishwa milele humo; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Atakaye kufa hali hamshirikishi Allah na chochote basi ataingia Peponi**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Wala hawatapata uombezi wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie ila watu wa Tawhidi; Abu Hureira Allah amridhie amesema:

«**Ewe Mtume wa Allah! Ni nani anayestahiki maombezi yako siku ya Kiyama? Akasema: Ni aliyesema 'laa ilaaha illa llaah'; kwa ikhlasi katika nafsi yake**», imepokewa na Bukhari.

Na mwenye kuitekeleza Tawhidi ataingia kupitia mlango anaotaka katika milango minane ya Pepo; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Hakuna yeyote kati yenu atatawadha akakamilisha udhu, kisha aseme: *'ash-hadu an laa ilaaha illa llaahu wahadahu laa shariika lah, wa ash-hadu anna Muhammadan abduhuu wa rasuuluh*; ila atafunguliwa milango ya Pepo minane, aingie kwa wowote anaoutaka**», imepokewa na Muslim.

Ibnu Al-Qayyim Allah amrehemu amesema: "Kila ikiwa Tawhidi ya mja kubwa; msamaha wa Allah kwake huwa timamu zaidi, basi atakaye kutana Naye hali ya kuwa hamshirikishi na chochote kabisa; atamsamehe madhambi yake yote».

Na watu elfu sabiini wataingia Peponi bila ya hesabu, wote ni watu wa Tawhidi, [Mtume] swala na salamu zimshukie:

«**wao ni wale ambao hawaombi kufanyiwa ruqya, wala hawaitakidi nuksi, wala hawajitibu kwa kujichoma moto, na wanamtegemea Mola wao mlezi**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

**Na baada ya hayo, enyi Waisilamu:**

Tawhidi ndio kitu ghali zaidi anachomiliki Muisilamu, na aliyeongozwa na Allah katika hiyo [Tawhidi] basi aing'ate kwa magego, na ailinde kutokana na yenye kuibomoa au kuitia dosari au kasoro, na aliyemuomba asiyekuwa Allah, au akatufu katika kaburi, au akalichinjia, basi hakika ameenda hasara ya nuru za Tawhidi na fadhila zake, na hatokubaliwa ibada yoyote, na atakuwa amejitia katika dalili za kukemea kukaa milele motoni.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿قُلْ إِنَّمَآ أَنَا۠ بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوحَىٰٓ إِلَيَّ أَنَّمَآ إِلَٰهُكُمْ إِلَٰهٌ وَٰحِدٌۖ فَمَن كَانَ يَرْجُواْ لِقَآءَ رَبِّهِۦ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَٰلِحًا وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِۦٓ أَحَدَۢا﴾

{Sema: Mimi ni mwanaadamu kama nyinyi. Ninaletewa Wahyi kwamba Muabudiwa wenu ni Muabudiwa Mmoja. Mwenye kutaraji kukutana na Mola wake Mlezi basi na atende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola wake Mlezi}. [Al-kahf: 110].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi Waisilamu:**

Tawhidi ni neema kubwa kutoka kwa Allah, humpatia anaye mtaka katika waja wake, na ni juu ya Muisilamu kufanya bidii kuitekeleza katika nafsi yake, kizazi chake na watu wa karibu katika jamaa wake na watu wote kwa jumla.

Na ni katika kuishukuru neema ya Tawhidi: Kuwalingania viumbe katika hiyo [Tawhidi], na kutahadharisha kila maafa yenye kupingana na asili yake au ukamilifu wake.

Na ni katika njia za kuimarika juu yake: kumuomba Allah akuthibitishe juu yake, kukaa mbali na uzushi na shubuha [yenye kutia shaka] na matamanio, kukithirisha ibada, kujiandaa na elimu ya kisheria, na kuuliza maulamaa walezi kila lenye kutia mushkili katika hiyo [elimu].

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# UBORA WA NENO LA TAWHIDI[1]

Sifa njema zote ni za Allah, twamhimidi, twamtaka msaada, na msamaha, na twajilinda Naye kutokana na shari za nafsi zetu, na amali zetu mbovu, yule atakayeongozwa na Allah basi hakuna wa kumpoteza, na atakaye mpoteza basi hakuna wa kumuongoza, na nashuhudia kuwa hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah peke Yake, hana mshirika Naye, na nashuhudia kuwa Muhammad ni mja wake na Mtume wake, swala za Allah ziwe juu yake, na juu ya watu wake na sahaba zake, na awateremshie salamu nyingi.

**Ama baada [ya himdi hii]**

Basi mcheni Allah - enyi waja wa Allah - haki ya kumcha, na kamateni Uisilamu katika kishikio madhubuti,

**Enyi waisilamu:**

Utukufu wa kiumbe uko katika kumtii Allah, na kujilazimisha kumuabudu Yeye, na hiyo ni hekima ya kuumba [kwa Allah] na amri [Yake], na kwayo ndio yanapatikana mafanikio na kufaulu duniani na akhera:

﴿وَمَن يُطِعِ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ فَقَدۡ فَازَ فَوۡزًا عَظِيمًا﴾

{Na anaye mt'ii Allah na Mtume wake, bila ya shaka amefanikiwa mafanikio makubwa}, [Al-Ahzaab: 71],

Na hakika si mengine furaha, ladha, uzuri wa umri na neema yanakuwa ndani ya kumtambua Allah, kumfanyia tawhidi na kumuamini.

Na maneno bora kabisa, na yanayopendeza zaidi kwa Allah ni yale yaliokuwa ni kumsifu Yeye, na sifa bora zaidi kwa Allah ni neno la tawhidi «laa ilaaha illa llah», neno ambalo kwa ajili yake zimesimama mbingu na ardhi, na kwa ajili yake ndio waliumbwa

[1] [Hutuba hii] imetolewa siku ya ijumaa, tarehe sita ya mwezi wa jumaadal uulaa, mwaka wa elfu moja mia nne na thalathini na nane hijria, ndani ya msikiti wa Nabii (Al-Masjidi Nnabawi).

viumbe, na kwa ajili yake ndio Allah aliteremsha Vitabu vyake na akatumiliza Mitume wake, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَمَآ أَرۡسَلۡنَا مِن قَبۡلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِيٓ إِلَيۡهِ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنَا۠ فَٱعۡبُدُونِ﴾

{Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa isipokuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu}, [Al-Anbiya : 25]

Nao Mitume waliwaonya nalo kaumu zao [waliwaonya kulikeuka neno hilo]; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿أَنۡ أَنذِرُوٓاْ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنَا۠ فَٱتَّقُونِ﴾

{ili nyinyi muonye kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Mimi, basi nicheni Mimi}. [An-Nahl: 2].

Allah amelishuhudia neno hili kwa nafsi yake, na akawashuhudiza viumbe vyake walio bora zaidi; amesema aliyetakasika:

﴿شَهِدَ ٱللَّهُ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ وَٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ وَأُوْلُواْ ٱلۡعِلۡمِ قَآئِمَۢا بِٱلۡقِسۡطِۚ
لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡحَكِيمُ﴾

{Allah na Malaika na wenye elimu, wameshuhudia kuwa hakika hapana apasaye kuabudiwa ila Yeye, ndiye Mwenye kusimamisha uadilifu; hapana apasaye kuabudiwa ila Yeye Mwenye nguvu na Mwenye hikima} [Aalu-Imran: 18].

Asema ibnul Qayyim Allah amrehemu: "huu ndio ushahidi mkubwa zaidi, mtukufu zaidi, muadilifu zaidi, na wa ukweli zaidi, kutoka kwa Shahidi mkubwa zaidi, juu ya jambo kubwa zaidi la kushuhudiwa".

Sheria zote [za Uisilamu] zimejengwa juu ya neno hili, na dini yote ni miongoni mwa haki zake, na thawabu zote ni katika kulitekeleza, na adhabu zote ni katika kuliacha au kufanya upungufu katika kulitekeleza, na nguzo [za dini] zote zinasimama juu yake, ni neno lenye daraja za juu, lenye fadhila nyingi, kwani [neno] hili ndio kichwa cha Uisilamu wote, na ndio ya kwanza kati ya nguzo zake na majengo yake makubwa, na juu yake ndio zinasimama nguzo zote [za Uisilamu zilizo baki], nalo ndio

nguzo ya kumuamini Allah na sehemu yake kubwa zaidi, basi haiwi sahihi imani bila [kulitekeleza neno] hili, wala hainyooki [imani] ila [inapojengwa] juu yake.

Mila [ya Uisilamu] imeasisiwa juu ya [neno hili], na kibula kimewekwa [kwa ajili yake], nalo ndio haki ya Allah juu ya waja wote. Ni neno la Uisilamu, na ufunguo wa nyumba ya salama [Pepo]. Kwa ajili yake watu wamegawanyika wakawa [baina ya] waovu na wema, waliokubaliwa [katika rehema za Allah] na waliofukuzwa, [neno hili] ni lenye kutofautisha baina ya ukafiri na Uisilamu, na watu hawajatamka neno zuri zaidi kuliko [neno] hili, na kati ya matendo hawajatenda yaliyo mazuri zaidi kuliko yale yanayotendwa kwa mujibu wa [neno] hili, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

**«maneno yanayopendeza zaidi kwa Allah ni manne: 'sub-haana llaah', 'al-hamdu lillah', 'laa ilaaha illa llaah' na 'Allahu ak-bar'**». Imepokewa na Muslim.

Hili ndilo neno la kuchamngu ambalo Allah kalifanya maalum kwa vipenzi vyake; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَأَلۡزَمَهُمۡ كَلِمَةَ ٱلتَّقۡوَىٰ﴾

{na akawalazimisha neno la kuchamngu} [Al-Fat-h: 26],

Nalo ndio kishikio madhubuti ambacho atakaye shikamana nacho ataokoka; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿فَمَن يَكۡفُرۡ بِٱلطَّٰغُوتِ وَيُؤۡمِنۢ بِٱللَّهِ فَقَدِ ٱسۡتَمۡسَكَ بِٱلۡعُرۡوَةِ ٱلۡوُثۡقَىٰ لَا ٱنفِصَامَ لَهَا﴾

{Basi anaye mkufuru Shet'ani na akamuamini Allah bila ya shaka amekamata kishikio madhubuti, kisicho vunjika}. [Al-Baqarah: 256]

Ujuu ndio sifa yake [neno hili], na kubaki kunaambatana nalo, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَكَلِمَةُ ٱللَّهِ هِيَ ٱلۡعُلۡيَا﴾

{na Neno la Allah kuwa ndilo juu} [At-Taubah: 40].

Ni neno zuri, Allah kalipigia mfano katika kitabu chake, akasema:

﴿أَلَمۡ تَرَ كَيۡفَ ضَرَبَ ٱللَّهُ مَثَلٗا كَلِمَةٗ طَيِّبَةٗ كَشَجَرَةٖ طَيِّبَةٍ أَصۡلُهَا ثَابِتٞ وَفَرۡعُهَا فِي ٱلسَّمَآءِ﴾

{Hebu hukuona vipi Allah alivyo piga mfano wa neno zuri? Ni kama mti mzuri, mizizi yake ni imara, na matawi yake yako mbinguni}. [Ibrahim: 24],

Kwalo kunapatikana ukunjufu wa kifua:

﴿فَمَن يُرِدِ ٱللَّهُ أَن يَهۡدِيَهُۥ يَشۡرَحۡ صَدۡرَهُۥ لِلۡإِسۡلَٰمِ﴾

{Basi yule ambaye Allah anataka kumuongoza humfungulia kifua chake kwa Uislamu}. [Al-an`aam: 125],

Ibnu Juraij Allah amrehemu amesema: "humfungulia kwa [neno la] (laa illaaha illa llaah). Kwalo kunapatikana salama ya moyo,

﴿يَوۡمَ لَا يَنفَعُ مَالٞ وَلَا بَنُونَ ۞ إِلَّا مَنۡ أَتَى ٱللَّهَ بِقَلۡبٖ سَلِيمٖ﴾

{Siku ambayo kwamba mali hayato faa kitu wala wana. Isipo kuwa mwenye kumjia Mwenyezi Mungu na moyo uliyo salimika}, [Ash-shuaraa`: 88-89],

Ibnu Abbaasi amesema Allah amridhie yeye na babake: "Moyo uliosalimika ni ashuhudie kuwa hakuna apasaye kuabudia isipokuwa Allah".

Nalo ndio ulinganizi wa haki ambao hauna batili ndani yake, ni kauli ya sawa ambayo haina kombo ndani yake, na ni ushahidi wa ukweli hauna uongo ndani yake, nalo ndio Sifa ya juu kabisa ambayo Allah kaifanya maalum kwake pasina viumbe vyake, nalo ndilo neno lililobaki baada kuondoka kwa Ibrahim salamu zimshukie; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَجَعَلَهَا كَلِمَةَۢ بَاقِيَةٗ فِي عَقِبِهِۦ لَعَلَّهُمۡ يَرۡجِعُونَ﴾

{Na akalifanya hili liwe neno lenye kubaki katika vizazi vyake ili warejee [kwa hili neno, kwa kuliamini na kuitekeleza]} [Az-zukhruf: 28]

Ibnu Kathiir Allah amrehemu amesema: "nalo [Neno hilo] ni: laa ilaaha illa llaah: alilifanya ni lenye kudumu katika kizazi

chake, wale walioongozwa na Allah katika kizazi cha Ibrahim wanamuiga yeye katika kulitekeleza [neno hili]".

"Laa ilaaha illa llaah" ni neema kubwa zaidi juu ya viumbe; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَأَسۡبَغَ عَلَيۡكُمۡ نِعَمَهُۥ ظَٰهِرَةٗ وَبَاطِنَةٗ﴾

{na akakujalizieni neema zake, za dhaahiri na za siri} [Luqman: 20],

Sufyan ibnu Uyeina Allah amrehemu amesema: «Allah hajawaneemesha waja wake kwa neema kubwa kuliko [hii] ya kuwatambulisha: laa ilaala illa llaah»

Nalo ni Neno linalotoshana na dunia pamoja na vilivyomo ndani yake; Mtume swala na salamu zimshukie alisema:

«**Kusema kwangu: 'Sub-haana llaah', 'wal-hamdu lillaah', 'wa laa ilaaha illa llaah', 'wa llaahu akbar'; kunapendeza zaidi kwangu kuliko kila kilicho chomozewa na jua**», imepokewa na Muslim.

Nalo [Neno hili] ndio wajibu wa kwanza -kuwa na elimu nalo na kulitekeleza- juu ya waja; [Allah] aliyetakasika anasema:

﴿فَٱعۡلَمۡ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱللَّهُ﴾

{Basi jua ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah} [Muhammad: 19],

Sheikhul Islaam Allah amrehemu amesema: "Wema waliotangulia na Maimamu wameafikiana ya kuwa jambo la kwanza wapasalo kuamrishwa waja ni Shahada mbili". Nalo pia ni wajibu wa mwisho; Mtume swala na salamu zimshukie alisema:

«**Yule ambaye mazungumzo yake ya mwisho yatakuwa ni: 'laa ilaaha illa llaah', ataingia Peponi**», imepokewa na Abu Daaud.

Mwenye elimu nalo na mwenye kulitekeleza Neno hili ndiye aliye nyooka sawa [katika dini] kihakika, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ قَالُواْ رَبُّنَا ٱللَّهُ ثُمَّ ٱسۡتَقَٰمُواْ﴾

{Hakika walio sema: Mola wetu Mlezi ni Allah! Kisha wakanyooka sawa}, [Al-Ahqaf: 13]

Ibnu Abbaas Allah amridhie yeye na babake amesema: yaani: shahada ya 'laa ilaaha illa llaah',

﴿فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ﴾

{hawatakuwa na khofu, wala hawatahuzunika}. [Al-Ahqaf: 13],.

Pindi Neno hili litasadiki basi moyo utatwahirika kutokana na kila asiyekuwa Allah, na atakaye kuwa mkweli katika Neno hili basi hatampenda isipokuwa Allah, hatamuona isipokuwa Yeye, hatamcha ila Yeye, hatategemea ila kwake, na hakutabakia [moyoni mwake] athari za [kuitanguliza] nafsi yake na matamanio yake [mbele ya Allah na amri yake].

Neno hili ni kinga ya mali na damu; Mtume swala na salamu zimshukie alisema:

«**Atakaye sema: 'laa ilaaha illa llaah', na akawakufuru wanaoabudiwa kinyume ya Allah; basi mali yake na damu yake zitakuwa haramu, na kumhasibu ni jukumu la Allah aliye na nguvu na aliyetukuka**», imepokewa na Muslim.

Nalo [Neno hili] ndilo jambo linaloanziwa nalo ulinganizi [daawah], Nabii swala na salamu zimshukie alianza nalo ulinganizi wake, na juu yake ndio alikuwa akichukua 'bai-ah' [ahadi ya kuinusuri dini] kutoka kwa sahaba zake, na alikuwa akituma walinganizi katika miji na Neno hili, akasema kumwambia Muaadh Allah amridhie pindi alipomtuma kuenda Yemen:

«**Hakika wewe unawendea watu waliopewa Kitabu; basi walinganie katika shahada ya 'laa ilaaha illa llaah' na kuwa mimi ni Mtume wa Allah**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea [hadith] hii.

Nalo ndilo Neno la Tawhidi, Neno lilio sawa, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿قُلْ يَٰٓأَهْلَ ٱلْكِتَٰبِ تَعَالَوْاْ إِلَىٰ كَلِمَةٍ سَوَآءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ

﴿أَلَّا نَعۡبُدَ إِلَّا ٱللَّهَ وَلَا نُشۡرِكَ بِهِۦ شَيۡـًٔا﴾

{Sema: Enyi Watu wa Kitabu! Njooni kwenye neno lilio sawa baina yetu na nyinyi: Ya kwamba tusimuabudu yeyote ila Allah, wala tusimshirikishe na chochote} [Aalu-Imran: 64],

Atakaye lisema kwa haki [kwa kulisema hali ya kulifahamu maana yake halisi na kulitekeleza] amefaulu; Nabii swala na salamu zimshukie alisema:

(**Enyi watu! Semeni 'laa ilaaha illa llaah' mtafaulu**) imepokewa na Ahmad.

Mwenye kushikamana nalo basi amekamata tagaa la juu kabisa la imani; Nabii swala na salamu zimshukie alisema:

(**Imani ni matagaa sabiini na, basi bora kabisa kati yao ni kauli ya: 'laa ilaaha illa llaah**'), imepokewa na Muslim.

Na aya iliolikusanya [Neno hili] ndio aya adhimu kabisa katika Qur-ani, na istighfari bora kabisa imelikusanya.

Nalo ndio amali inayozidisha zaidi na yenye ujira zaidi, kwani:

(**atakaye sema katika siku mara mia moja: *'laa ilaaha illa llaah, wah-dahuu laa shariika lah, lahul mulk, walahul hamd, wa huwa alaa kulli shay-in qadiir'*, yatakuwa [malipo yake] kwake ni sawa na kuacha huru watumwa kumi, na ataandikiwa thawabu mia moja, atafutiwa dhambi mia moja, na yatakuwa [maneno haya] kwake ni kinga kutokana na shetani siku yake ile hadi jioni, na hatakuja mtu [siku ya Kiyama] na bora kuliko aliokuja nayo yeye, ila mtu aliyetenda zaidi ya hilo [alilotenda yeye]**), imepokewa na Bukhari na muslim.

Na: (**atakayesema: *'laa ilaaha illa llaah, wahdahuu laa shariika lah, lahul mulk, walahul hamd, wa huwa alaa kulli shay-in qadiir'*, mara kumi; atakuwa ni kama aliyeacha huru nafsi nne miongoni mwa wana wa Ismail**), imepokewa na Muslim.

Neno hili ndio sadaka kubwa zaidi bila kutoa mali; Mtume

swala na salamu zimshukie alisema: «**Na kauli ya 'laa ilaaha illa llaah' ni sadaka**», imepokewa na Muslim, nalo [kulitekeleza Neno hili] ndio kuokoka ndani ya kaburi, na [kuishi] juu yake [duniani] ndiko kunamthibitisha mtu pindi anapohojiwa [kaburini], Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**Anapoulizwa Muisilamu ndani ya kaburi: atashuhudia kuwa hapana apasaye kuabudiwa ila Allah, na kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah; na hiyo ndio [tafsiri ya] kauli ya Allah: {Allah huwatia imara wenye kuamini kwa kauli ya imara katika maisha ya dunia na katika Akhera}**» wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea [hadith] hii.

Na sajili [jalada] za madhambi zinakuwa nyepesi [katika mizani ya amali] kwa ajili ya uzito wa Neno hili - hilo ni kwa neema ya Allah -, Mtume swala na salamu zimshukie alisema: «**Hakika Allah mwenye nguvu na utukufu atamtoa mtu miongoni mwa ummah wangu mbele ya viumbe siku ya Kiyama, amfungulie sajili [za dhambi zake] tisaini na tisa, [ukubwa wa] kila sajili moja ni upeo wa macho, kisha atolewe kibahasha, mnao ndani yake: 'ash-hadu an laa illaaha illa llaah, wa ash-hadu anna Muhammadan rasuulu llaah', basi ziwekwe sajili zile katika mkono wa mizani, sajili zikawa nyepesi na kibahasha kikawa kizito**», imepokewa na Ahmad. «**Na lau mbingu saba na ardhi saba zitawekwa katika mkono wa mizani, na ikawekwa 'laa ilaaha illa llaah' katika mkono mwengine; 'laa ilaaha illa llaah' itazishinda, na lau mbingu saba na ardhi saba zitakuwa ni duara lilio fungwa [lisio na njia ya kutokea, au amali kupanda kwa Allah], basi [amali ya] 'laa ilaaha illa llaah' ingezipasua [na inyanyuke kuenda kwa Allah**], imepokewa na Ahmad.

Watu wake [Neno hili] ndio wenye Uombezi [siku ya Kiyama], na wanao ahadi mbele ya Ar-Rahmaan [Allah mwingi ya rehema]; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿لَّا يَمۡلِكُونَ ٱلشَّفَٰعَةَ إِلَّا مَنِ ٱتَّخَذَ عِندَ ٱلرَّحۡمَٰنِ عَهۡدٗا﴾

{Hawatakuwa na mamlaka ya uombezi ila wale walio chukua ahadi kwa Ar-Rahmani Mwingi wa Rehema}. [Maryam: 87].

Na watakaofaidika zaidi na uombezi wa Nabii swala na salamu zimshukie ni wenye ikhlasi walio wakweli katika kulisema kwao [Neno hili], Nabii swala na salamu zimshukie alisema:

«**Mtu atakayefaidika zaidi na uombezi wangu siku ya Kiyama ni aliyesema: 'laa ilaaha illa llaah' kwa ikhlasi kutoka ndani ya nafsi yake**», imepokewa na Bukhari.

Na Pepo ni malipo ya aliyelisema [Neno hili] kwa ukweli [yaani moyo wake na vitendo vyake vilisadikishe Neno hili], kwa ikhlasi ndani ya moyo wake, na akiwa na yakini nalo bila kuwa na shaka [hata ndogo], akawa mwenye kulitendea kazi, mwenye kuepuka kila lenye kuenda kinyume nalo; Mtume swala na salamu zimshukie alisema:

«**Hakuna mja yeyote atasema 'laa ilaaha illa llaah', kisha afariki juu ya hilo; isipokuwa ataingia Peponi**» wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

[Neno hili] ni lenye kumfungulia anayelisema milango ya Pepo minane, aingie kupitia wowote anaotaka; bali aliyekuwa mkweli katika kulisema, mtenda kazi wa yanayowajibishwa nalo; Moto hautamgusa, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Hakuna yeyote anaye shuhudia kuwa hapana apasaye kuabudiwa ila Allah, na kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah, [ashuhudia hilo] hali yakuwa mkweli ndani ya moyo wake, isipokuwa Allah ataharamisha yeye kuingia Motoni**»,

wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, na Allah atamtoa kutoka Motoni kila atakaye lisema na hali ya kuwa ndani ya moyo wake mna imani uzito wa chungu ndogo kabisa;

«**Allah mwenye Ushindi na Uwezo mkubwa amesema: naapa kwa ushindi wangu, Utukufu wangu, Kiburi changu na Ukuu wangu; hakika nitamtoa kutoka [Motoni] kila aliye sema 'laa ilaaha illa llaah**»', imepokewa na Bukhari.

Na kwa ajili ya umuhimu wa tawhidi katika kila punde ya maisha ya mja; ndio Sheria imekuja kuhimiza kushikamana nayo [tawhidi] katika hali zake [mja] zote na mambo yake yote;

basi «**atakaye sema pindi inapoingia asubuhi: *'laa ilaaha illa llaah, wah-dahu laa shariika lah, lahul mulku, walahul hamdu, wa huwa alaa kulli shay-in Qadiir'*; atakuwa [na ujira wa] kama aliyeacha huru mtumwa miongoni mwa wana wa [Nabii] Ismail, na ataandikiwa mema kumi, atafutiwa maovu kumi, atanyanyuliwa daraja kumi, na atakuwa ndani ya ulinzi kutokana na Shetani hadi iingie jioni, na anaposema hayo jioni, basi atapata [malipo] mfano wa hayo hadi iingie asubuhi**», imepokewa na Abu Daaud,

Na akilisema [Neno hili] pindi anapomaliza kujitwahirisha kwake, basi atafunguliwa milango ya Pepo [yote] minane, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Hakuna yeyote kati yenu atatawadha, akakamilisha udhu wake, kisha akasema: *'ash-hadu an laa ilaaha illa llaah, wa ash-hadu anna Muhammadan abduhuu wa rasuuluh'*, isipokuwa atafunguliwa milango ya Pepo minane**», imepokewa Muslim.

Nalo [Neno hili] ndio kianzio cha adhana na kimalizio chake, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Pindi muadhini anaposema: 'Allah ak-bar, Allah ak-bar', na mmoja wenu akasema: 'Allah ak-bar, Allah ak-bar', kisha muadhini akasema: 'ash-hadu an laa ilaaha illa llaah', [naye] akasema: 'ash-hadu an laa ilaaha illa llaah', kisha muadhini akasema: 'ash-hadu anna Muhammadan rasuulu llaah', [naye] akasema: 'ash-hadu anna Muhammadan rasuulu llaah', kisha muadhini akasema: 'hayya alaa sswalaah', [naye] akasema: 'laa hawla walaa quwwata illaa billaah', kisha muadhini akasema: 'hayya alal falaah', [naye] akasema: 'laa hawla walaa quwwata illaa billaah', kisha muadhini akasema: 'Allah ak-bar, Allah ak-bar', [naye] akasema: 'Allah ak-bar, Allah ak-bar', kisha muadhini**

**akasema: 'laa ilaaha illa llaah', [naye] akasema: 'laa ilaaha illa llaah', [yote hayo akayasema] kutoka moyoni mwake, basi ataingia Peponi**»,imepokewa na Muslim.

Na «**atakaye sema pindi atamsikia muadhini: *'ash-hadu an laa ilaaha illa llaahu wahadahuu laa shariika lah, wa ash-hadu anna Muhammadan abduhuu wa rasuuluh, radwitu bi llaahi rabaa, wa bi Muhammadin rashuulaa, wa bil islaami diinaa*; atasamehewa dhambi zake'**», imepokewa na Muslim.

Na katika Swala; pindi Muisilamu atasimama kuingia kwenye Swala anaifungua na tawhidi, na Swala haisihi ila kwa [kupatikana] 'tashahhud' [ndani yake], na kabla ya mwenye kuswali atoe salamu ili kutoka kwenye Swala anaomba akitawasali kwa Allah nalo [Neno hili la tawhidi]

«**Ewe Allah, nisamehe [dhambi] nilizozitanguliza, na [amali] nilizoziacha, na [dhambi] nilizozifanya kwa siri, na zile nilizozidhihirisha, na yale niliofanya israfu ndani yake na kuvuka mipaka, na yale ambayo Wewe ndiye unayajua zaidi kuliko mimi, Wewe ndiye mwenye kutanguliza [baadhi ya waja wako unaowataka na kuwanyanyua daraja za ukamilifu], na Wewe ndiye mwenye kuwachelewesha [baadhi ya waja wako unaowataka na kuwaangusha katika tabaka za chini na udunifu], 'laa ilaaha illa anta'**», imepokewa na Muslim,

Na mwisho wa kila Swala anasema:

«***'laa ilaaha illa llaahu wahadahuu laa shariika lah, lahul mulku, walahul hamd, wa huwa alaa kulli shay-in qadiir'***», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na [mja] anahitimisha nalo Neno hili] 'Tasbihi', 'Tahmidi' na 'Takbira', basi:

«**akasamehewa [kwalo] dhambi zake, hata kama ni mfano wa povu la bahari**», imepokewa na Muslim.

Na katika ibada za hija anaambatana nayo [katika hali zote];

«**Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa pindi anapanda [kilima] cha Swafaa na Marwa; anaelekea kibla,**

**akamsifu Allah na upweke [kwa Neno hili la tawhidi], na akamuadhimisha [kwa kuleta takbira]**» imepokewa na Muslim,

Na walipokuwa Muzdalifah:

«**Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alikuja 'Al-Mash-ar' [kiwanja cha Muzdalifah], akapanda juu yake, akamuhimidi Allah, na akamsifu na tawhidi, akamuadhimisha [kwa kuleta takbira], na akasema 'laa ilaaha illa llaah'**», imepokewa na Nasai.

**Na [alikuwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie] anaporudi kutoka vitani au hija au umrah, analeta takbiira mara tatu kila akipanda sehemu ya juu ya ardhi, kisha akisema: *'laa ilaaha illa llaahu wah-dahu laa shariika lah, lahul mulku wa lahul hamd, wa huwa alaa kulli shay-in qadiir***» wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na katika misimu ya heri - kama kumi la kwanza la dhul hijja - inapendekezwa kulikithirisha [kulisema Neno hili], na katika hutuba, mwanzo wake unafunguliwa na tawhidi, na katika kuchangamana kwake [mja] na watu, pindi amekaa kikao kilichokithiri ndani yake kelele, kisha mja akasema kabla kusimama kutoka kikao chake kile:

«***Sub-haanaka llaahumma wa bihamdik, ash-hadu anlaa ilaaha illaa anta, astaghfiruka wa atuubu ilaik*; ila atasamehewa yaliyotokea kwenye kikao chake kile**», imepokewa na Tirmidhi.

Na «**atakayezinduka usiku - akasema Neno hili- kisha akaomba; maombi yake yataitikiwa, na akitawadha na kuswali; swala yake itakubaliwa**», imepokewa na Bukhari.

Na katika hali ya janga anasema:

«***'laa ilaaha illa llaahul Adhwiimul H'aliim, laa ilaaha illa llaahu Rabbul Arshi' adhwiim, laa ilaaha illa llaahu Rabbu ssamaawaati wal ardwi wa Rabbul arshil kariim***», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na kumsifu Allah nalo [Neno hili] kabla ya maombi ni sababu

ya kuitikiwa; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَذَا ٱلنُّونِ إِذ ذَّهَبَ مُغَٰضِبًا فَظَنَّ أَن لَّن نَّقۡدِرَ عَلَيۡهِ فَنَادَىٰ فِي ٱلظُّلُمَٰتِ أَن لَّآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنتَ سُبۡحَٰنَكَ إِنِّي كُنتُ مِنَ ٱلظَّٰلِمِينَ ۞ فَٱسۡتَجَبۡنَا لَهُۥ وَنَجَّيۡنَٰهُ مِنَ ٱلۡغَمِّ﴾

{Na Dhun-Nun alipoondoka hali ameghadhibika, na akadhani ya kwamba hatutakuwa na uwezo juu yake. Basi aliita katika giza: Hapana apasaye kuabudiwa isipo kuwa Wewe Sub-hanaka Uliye takasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu [nafsi zao]. Basi tukamwitikia na tukamwokoa kutokana na dhiki} [Al-Anbiya`: 87-88],

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**katu hajawahi Muisilamu yeyote kuomba kwa dua hii; ila Allah humuitikia**» imepokewa na Tirmidhi.

Nalo ndio kafara ya kiapo; Mtume swala na salamu za zimshukie:

«**Atakaye apa akasema katika kiapo chake: Naapa kwa lata na uzza; basi aseme: 'laa ilaaha illa llaah**» wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na inapendekezwa kumtamsha aliofikwa na kifo Neno hili; Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**watamsheni maiti zenu: 'laa ilaaha illa llaah**», imepokewa na Muslim.

Na aliyekuwa nje ya mila [ya Uisilamu] analinganiwa katika Neno hili hata akiwa katika wakati wa mwisho wa maisha yake; Abu Twalib alifikwa na mauti, basi Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akasema kumwambia:

«**Ewe ami yangu, sema 'laa ilaaha illa llaah', Neno ambalo nitakutolea ushahidi nalo mbele ya Allah**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

**Na baada ya hayo, enyi waisilamu:**

Basi [jueni kuwa] nguvu na ushindi ni ndani ya tawhidi, Umar Allah amridhie amesema: "Sisi ni watu ambao Allah ametupa nguvu na ushindi kwa Uisilamu", na shahada ndio anuani yake [Uisilamu] na lenye kuutambulisha, na kauli yenye kuvunjwa na

vitendo hainufaishi, na asiyelitamka [Neno] hili basi atakosa ladha na raha za dunia na akhera, na nguvu na udhaifu wa waisilamu zinategemea kulitekeleza kwao Neno hili kimatamshi na kimatendo, basi hili ndio mizani yao mbele ya Allah na mbele ya watu, linapopata nguvu kwao basi Allah atawaridhia, watapata ushindi, na watanyanyuka, na linapodhuufika watakuwa mbali na Allah, watadhuufika na watadhalilika.

***Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim:***

﴿فَٱعْلَمْ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱللَّهُ وَٱسْتَغْفِرْ لِذَنۢبِكَ وَلِلْمُؤْمِنِينَ وَٱلْمُؤْمِنَٰتِ ۗ وَٱللَّهُ يَعْلَمُ مُتَقَلَّبَكُمْ وَمَثْوَىٰكُمْ﴾

{Basi jua ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah, na omba maghufira kwa dhambi zako na za Waumini wanaume na Waumini wanawake. Na Allah anajua mahali penu pa kwenda na kurudi, na mahali penu pa kukaa.} [An-Naml: 19].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi waisilamu:**

Elimu ya maana ya 'laa ilaaha illa llaah', kuitendea kazi, na kuwa mbali na yenye kulipinga [Neno hili] na yenye kulivunja; [yote hayo] ni sharti ya kupata yanayo wajibu kwalo [Miongoni mwa malipo na mazuri ya Neno hili] yaliokuja katika dalili, basi maana yake [Neno hili]: ni kukanusha kustahiki kuabudiwa kwa asiyekuwa Allah, na kulithibisha hilo kwa Allah pekee, na hili ndilo walilolikanusha makafiri wa kikureshi, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿إِنَّهُمْ كَانُوٓاْ إِذَا قِيلَ لَهُمْ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱللَّهُ يَسْتَكْبِرُونَ﴾

{Wao walipo kuwa wakiambiwa 'laa ilaaha illa llah' [Hapana apasaye kuabudiwa ila Allah tu], wanafanya kiburi [As-Swaffaat: 35],

Na kuikiri kwao tawhidi ya rubuubiyyah peke yake hakukuwanufaisha kitu.

Kila aliyekuwa mjuzi zaidi wa maana yake, na mtekeleza zaidi wa mahitaji yake, basi mizani [ya mema] yake itakuwa nzito zaidi, kutofautiana kwa watu ndani yake [Neno hili] ni kwa kiwango cha kuhakikisha kwao masharti yake, na roho na siri ya Neno hili: Ni kumpwekesha Allah kwa ibada, basi atakaye mshirikisha kiumbe katika haki ya Allah na ibada zake, hilo linakuwa ni lenye kuvunja kauli yake: "laa ilaaha illa llaah".

Na mwenye kuneemeka [na maisha mema] ni yule aliye

ihifadhi tawhidi yake na akafariki juu yake, wala asijichafue na yoyote yenye kuivunja, au yenye kuitia dosari, au yenye kulivunja, na [maisha] haya ndio matamanio ya waja wa Allah wakweli:

﴿تَوَفَّنِي مُسۡلِمٗا وَأَلۡحِقۡنِي بِٱلصَّٰلِحِينَ﴾

{Nifishe hali ya kuwa ni Muislamu [aliyejisalimisha kwa Allah na tawhidi] na nikutanishe na waja wema}. [Yusuf: 101].

Kisha jueni ya kuwa Allah amewaamuru kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# AMALI INAYOPENDEZA ZAIDI KWA ALLAH[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakaye mpoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Enyi waja wa Allah, mcheni Allah haki ya kumcha, na kamateni Uislamu katika kishiko madhubuti kabisa.

**Enyi Waisilamu:**

Allah amewaumba waja wake, akawadhalilishia vyote vilivyoko mbinguni na ardhini [iwe sahali kwao kuvitumia na kunufaika navyo], na akawamiminia neema zake kwa dhahiri na batini; [yote hayo] ili wampwekeshe Yeye aliyetakasika na ibada, basi watu baada ya Adam [salamu zimshukie] walidumu katika kumuabudu Allah peke yake kwa karne kumi, baada ya hapo shetani akawapambia baadhi ya watu ibada ya masanamu nao wakayaabudu;

Basi Allah akatumiliza Mitume na akateremsha pamoja nao Vitabu; ili watu warudi katika kumuabudu Allah peke yake, na katika huruma yake kwa viumbe vyake: amejaalia umbile lao ni lenye kuafikiana na lengo waliloumbiwa kwalo, basi kila kinachozaliwa huzaliwa juu ya umbile la kumpwekesha Allah na ibada, na [kutambua ya] kwamba Yeye ndiye mstahiki wa kuabudiwa peke yake pasina wengine, aliyetukuka amesema:

---

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe ishirini na tisa, mwezi wa Shawwali, mwaka elfu moja mia nne na thalathini na moja hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

﴿فِطۡرَتَ ٱللَّهِ ٱلَّتِي فَطَرَ ٱلنَّاسَ عَلَيۡهَا﴾

{[Tawhidi] ndilo umbile la Allah alilo waumbia watu}. [Ar-Ruum: 30].

Na shetani anaenda mbio ili kufisidi maumbile ya watu; ili awakoseshe waja radhi za Mola wao Mlezi, na neema za daima zilizoandaliwa katika Pepo ya 'Adni'; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema siku moja katika hotuba:

«**Jueni kuwa Mola wangu Mlezi ameniamrisha niwafundishe msio yajua katika alionijulisha leo hii, [nalo ni kuwa Allah amesema: ] Na hakika Mimi nimewaumba waja wangu wote wakiwa Hunafa-a [watu wa Tawhidi wenye kuepuka shirki], na wao walijiwa na mashetani wakawaepusha na Dini yao, wakawaharamishia niliowahalalishia, na wakawaamrisha wanishirikishe na ambayo sijawateremshia hoja nayo**», imepokewa na Muslim.

Ibilisi anawaita viumbe waingie katika dhambi kubwa zaidi analoasiwa nayo Allah; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie aliulizwa:

«**Ni dhambi gani kubwa zaidi? Akasema: Ni umfanyie Allah mshirika hali Yeye ndiye aliyekuumba**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, basi wengi kati ya watu wakawaabudu wasiokuwa Allah; kama alivyosema [Allah] aliyetakasika:

﴿وَلَٰكِنَّ أَكۡثَرَ ٱلنَّاسِ لَا يُؤۡمِنُونَ﴾

{lakini watu wengi hawaamini}. [Ar-Ra`ad: 1].

Na ni katika athari za kutoamini: kuwa amali zote zinazo tendwa - hata zikiwa njema - hazina thawabu; kwa ajili ya kukosa msingi wa Dini, Aisha Allah amridhie alisema:

«**Ewe Mtume wa Allah! Ibnu Jud'aan wakati wa jahiliyyah [kabla Mtume kuja na Uisilamu] alikuwa akiunga kizazi, na akilisha maskini, basi je hilo litamnufaisha [siku ya Kiyama]? [Mtume] akasema: Halitamnufaisha, kwani yeye hakuwahi kusema hata siku moja: Mola wangu Mlezi**

**nisamehe madhambi yangu Siku ya Malipo**», imepokewa na Muslim.

Na dhambi hili ni sababu kwa yule aliyelifanya kupata hasira za Allah na kuteremkiwa na udhalilifu na unyonge; [Allah] mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ ٱتَّخَذُواْ ٱلۡعِجۡلَ سَيَنَالُهُمۡ غَضَبٞ مِّن رَّبِّهِمۡ وَذِلَّةٞ فِي ٱلۡحَيَوٰةِ ٱلدُّنۡيَا﴾

{Hakika wale walio muabudu ndama, itawapata ghadhabu ya Mola wao Mlezi na madhila katika maisha ya dunia}; [Al-A`raaf: 152].

na mwenye [dhambi hili] anageuka geuka katika majanga, hamu na huzuni; [Allah] mtukufu wa shani amesema:

﴿وَمَن يُرِدۡ أَن يُضِلَّهُۥ يَجۡعَلۡ صَدۡرَهُۥ ضَيِّقًا حَرَجٗا كَأَنَّمَا يَصَّعَّدُ فِي ٱلسَّمَآءِ﴾

{Na anaye taka kumpoteza hukifanya kifua chake kina dhiki, kimebana, kama kwamba anapanda mbinguni}, [Al-an`aam: 125],

na dhambi hili] linamzuia kuingia Peponi na linamtia milele Motoni; [Allah] mtukufu wa shani amesema:

﴿إِنَّهُۥ مَن يُشۡرِكۡ بِٱللَّهِ فَقَدۡ حَرَّمَ ٱللَّهُ عَلَيۡهِ ٱلۡجَنَّةَ وَمَأۡوَىٰهُ ٱلنَّارُ﴾

{Kwani anaye mshirikisha Allah, hakika Allah atamharimishia Pepo, na mahala pake ni Motoni}. [Al-Maaidah: 72].

Na ili waja wasiingie ndani ya mtego wa shetani, wakamkasirisha Mola wao Mlezi, na wasitiwe milele Motoni, ndio Allah ameutumilizia kila umma Mtume awatahadharishe na ulinganizi wa shetani, na awaamrishe kumuabudu 'Al-Rahmaan', na ameteremsha Vitabu, akailingania [Tawhidi] katika aya za Qur-ani nyingi, zote zilizo ndani ya Qur-ani zinaijulisha, na amri ya kwanza katika Qur-ani ni amri yake, [Allah] aliyetukuka na aliye juu amesema:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ ٱعۡبُدُواْ رَبَّكُمُ ٱلَّذِي خَلَقَكُمۡ﴾

{Enyi watu! Muabuduni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni nyinyi}, [Al-Baqarah: 21]. yaani: mwepwekesheni Mola wenu

Mlezi, na katazo la kwanza analolisoma msomaji wa Qur-ani ni katazo la kinyume chake:

﴿فَلَا تَجۡعَلُواْ لِلَّهِ أَندَادًا وَأَنتُمۡ تَعۡلَمُونَ﴾

{Basi msimfanyizie Allah washirika, na hali nyinyi mnajua}, [Al-Baqarah: 22].

Surah ya ikhlasi inalingana na thuluthi ya Qur-ani, kwa kule kukusanya kwake Tawhidi, na aya tukufu zaidi ni iliyo kusanya Tawhidi yake: Ayatul Kursiy.

Na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikaa baada ya kutumilizwa miaka kumi akilingania Tawhidi ya Allah, halinganii katika kitu chochote kisichokuwa hiyo [Tawhidi], kisha zikafuatana kwake sheria, akawa anazilingania pamoja na Tawhidi hadi kufa kwake,

Na alikuwa akisema asubuhi na jioni:

«**Tumepambazuka tukiwa juu ya umbile la Uisilamu, na juu ya Neno la ikhlasi, na juu ya Dini ya Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie na juu ya mila ya baba yetu Ibrahim 'haniif' [mwenye kuelekeaa katika Tawhidi na kuepuka shirki] Muisilamu, wala hakuwa katika Washirikina**», imepokewa na Ahmad,

Na alikuwa akiifungua siku yake na Tawhidi, akisoma katika rakaa mbili za [sunnah ya] Alfajiri suratul «Kaafiruun» na «Ikhlaas», na akiikhitimisha nayo [Tawhidi]; akisoma katika rakaa mbili za kabla ya witru na witru yenyewe suratul «Kaafiruun» na «Ikhlaas».

[Mtume] aliwausia nayo umma wake, alikuja A'arabi [mtu wa mashambani] kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akasema:

«**Nijulishe amali endapo nitaifanya nitaingia Peponi, [Mtume] akasema: Muabudu Allah wala usimshirikishe na chochote, usimamishe Swala iliowajibishwa, utoe Zaka iliofaradhishwa, na ufunge Ramadhani**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na alikuwa akiwaamrisha masahaba wake wampe 'bai-ah' [ahadi ya kuinusuru dini] juu ya kumuabudu Allah peke yake; Auf ibnu Malik Allah amridhie:

«**Tulikuwa kwa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie tukiwa watu tisa au wanane au saba, akasema: Hamumpatii 'bai-ah' Mtume wa Allah? Tukasema: Ewe Mtume wa Allah tushakupatia 'bai-ah'! Tukupe 'bai-ah' juu ya jambo gani? Akasema: Juu ya kuwa mumuabudu Allah wala musimshirikishe na chochote, na Swala tano**», imepokewa na Muslim.

Na anapotuma walinganizi katika miji: anawaamrisha waanze na kulingania katika Tawhidi; alimtuma Muadh [Allah amridhie] kuenda Yemen, na akamuambia:

«**Hakika wewe unawaendea watu miongoni mwa waliopewa Kitabu; basi walinganie katika shahada ya 'laa ilaaha illa llaah' na kuwa mimi ni Mtume wa Allah**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na anapokujiwa na makundi huwafundisha Tawhidi; alijiwa na kundi la [kabila la] Abdul Qays, akawaambia:

«**Je mnajua ni nini kumuamini Allah peke yake? Wakasema: Allah na Mtume wake wanajua zaidi, [Mtume] akasema: Ni kushuhudia kuwa hapana apasaye kuabudiwa ila Allah, na kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah...»,** wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea

Mitume waliwaogopewa wana wao jambo la kumfuata shetani kwa kuabudu masanamu; kipenzi cha Allah [Ibrahim] salamu zimshukie:

﴿وَٱجۡنُبۡنِي وَبَنِيَّ أَن نَّعۡبُدَ ٱلۡأَصۡنَامَ﴾

{na uniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu}, [Ibrahim: 35]

na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie aliwaogopea umma wake; akasema:

«**Ninalowaogopea zaidi ni shirki ndogo, akaulizwa**

**kuihusu, akasema: ni riya [kufanya amali kwa lengo la kuonekana]**», imepokewa na Ahmad, nayo [Tawhidi] ni katika haki za Allah juu ya waja, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Ewe Muadh! Je unajua ni ipi haki ya Allah juu ya waja, akasema: Allah na Mtume wake wanajua zaidi, akasema: Haki ya Allah juu ya waja: ni wamuabudu Yeye, wala wasimshirikishe na chochote**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Nayo inamkaribisha mja na Pepo na inamuepusha na Moto; alikuja mtu wa kijijini [A'raabi] kwa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, akasema:

«**Nihadithie jambo lenye kunikaribisha na Pepo na kuniepusha na Moto, [mpokezi] asema: [Nabii] swala na salamu za Allah zimshukie akanyamaza, kisha akawaangalia Masahaba wake, kisha akasema kuwaambia: Hakika huyu ameafikiwa - au alisema: Hakika huyu ameongozwa. [Nabii akamgeukia A'raabi] akasema: Umesemaje? [mpokezi] asema: Akarudia [swali], basi Nabii swala na salamu za Allah zimshukie akasema: Muabudu Allah wala usimshirikishe na chochote, usimamishe Swala, utoe Zaka, na uunge kikazi**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Wala haipatikani saada duniani na akhera ila kwayo; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Semeni 'laa ilaaha illa llaah'; mtafaulu**», imepokewa na Ahmad, na yule itakayo kuwa hatima yake juu ya shahada ataingia Peponi, [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Yule yatakao kuwa maneno yake ya mwisho ni 'laa ilaaha illa llaah' ataingia Peponi**», imepokewa na Abu Daaud, na atakaye kufa juu yake [yaani: aishi akiwa ni mwenye kuitekeleza na kuihifadhi hadi mauti yamkute hata kama hakuitamka wakati wa kufa kwake] ataingia Peponi, [Nabii] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**atakaye kutana na Allah [atakaye kufa] hali ya kuwa hamshirikishi na chochote ataingia Peponi, na atakaye kutana Naye hali anamshirikisha na chochote ataingia Motoni**», imepokewa na Muslim.

Amali za watu wa Tawhidi zinazidiana kwa sababu ya kuzidiana yaliomo ndani ya nyoyo miongoni mwa Imani na Ikhlasi, na la azizi [jambo lenye thamani zaidi] analomiliki mja ni Tawhidi yake kwa Mola wake Mlezi, na jambo muhimu zaidi kwake ni kujihifadhia [Tawhidi yake] kutokana na kubatilika, au yenye kuiingia na kuitia toa na dosari, ibnul Qayyim Allah amrehemu alisema: "Tawhidi ni kitu laini zaidi, takatifu zaidi, nadhifu zaidi na safi zaidi; basi kitu kidogo kinaitia toa, kinaichafua na kinaiathiri, nayo ni kama nguo nyeupe zaidi: athari ndogo zaidi inaiathiri, na kama kioo kisafi sana: kitu kidogo zaidi kinakiathiri".

Allah mwenye ushindi na utukufu amewafunulia Mitume wake ya kwamba, endapo watafanya shirki amali zao zitaporomoka, basi iweje kwa wasiokuwa wao?! Allah mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿وَلَقَدۡ أُوحِيَ إِلَيۡكَ وَإِلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِكَ
لَئِنۡ أَشۡرَكۡتَ لَيَحۡبَطَنَّ عَمَلُكَ وَلَتَكُونَنَّ مِنَ ٱلۡخَٰسِرِينَ﴾

{Na kwa yakini yamefunuliwa kwako na kwa walio kuwa kabla yako: Bila ya shaka ukimshirikisha Allah amali zako zitaanguka, na lazima utakuwa miongoni mwa wenye kukhasiri}, [Az-zumar: 65],

kwa ajili hii ndio Ibrahim salamu zimshukie aliiogopa shirki, akawa anamuomba Mola wake Mlezi - alipokuwa anajenga Kaaba -:

﴿وَٱجۡنُبۡنِي وَبَنِيَّ أَن نَّعۡبُدَ ٱلۡأَصۡنَامَ﴾

{na uniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu}, [Ibrahim: 35],

na ikiwa kipenzi cha Allah anajiogopea shirki, basi wasio

kuwa yeye wanastahiki zaidi [kujiogopea shirki].

Na kuwafunza Watoto msingi wa Dini [Tawhidi] na kuwauliza daima kuihusu ni mfumo wa Mitume; Yakub salamu zimshukie - akiwa katika hali ya kutoka roho - anawauliza wanawe kuhusu Tawhidi yao:

﴿أَمۡ كُنتُمۡ شُهَدَآءَ إِذۡ حَضَرَ يَعۡقُوبَ ٱلۡمَوۡتُ إِذۡ قَالَ لِبَنِيهِ مَا تَعۡبُدُونَ مِنۢ بَعۡدِيۖ قَالُواْ نَعۡبُدُ إِلَٰهَكَ وَإِلَٰهَ ءَابَآئِكَ إِبۡرَٰهِـۧمَ وَإِسۡمَٰعِيلَ وَإِسۡحَٰقَ إِلَٰهٗا وَٰحِدٗا وَنَحۡنُ لَهُۥ مُسۡلِمُونَ﴾

{Je! Mlikuwapo yalipo mfikia Yaaqub mauti, akawaambia wanawe: Mtamuabudu nani baada yangu? Wakasema: Tutamuabudu Muabudiwa wako na Muabudiwa wa baba zako, Ibrahim na Ismail na Is- hak, Muabudiwa Mmoja tu, na sisi tunasilimu kwake}, [Al-Baqarah: 133],

na Nabii wetu swala na salamu za Allah zimshukie alimuuliza msichana mdogo:

«**Allah yuko wapi? Akasema: yuko Juu mbinguni**», imepokewa na Muslim.

Kusoma vitabu vya itikadi iliyosalimika, na kushikamana na vikao vya wenye ilimu ni katika sababu za kupata imara; [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**nimeacha kwenu vitu viwili ambavyo hamtapotea baada yake [baada ya kushikamana navyo]: Kitabu cha Allah na sunnah yangu**», imepokewa na Al-Haakim, sheikh Muhammad ibnu Abdil-Wahhaab Allah amrehemu amesema: "la muhimu zaidi linalo kulazimu ni: kuijua Tawhidi, kabla ya kujua ibada zote hata Swala", na kuomba kupata imara juu ya Dini ni njia ya Manabii; Yusuf salamu zimshukie alisema:

﴿تَوَفَّنِي مُسۡلِمٗا وَأَلۡحِقۡنِي بِٱلصَّٰلِحِينَ﴾

{Nifishe hali ya kuwa ni Muislamu na nichanganyishe na watendao mema}, [Yusuf: 101].

na kuadhimisha kumpwekesha Muumba [kuadhimisha Tawhidi], kujua umuhimu wake, na kukaa mbali na shubuha [yenye kutia shaka] ni katika sababu za uongofu.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿فَٱعۡلَمۡ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱللَّهُ وَٱسۡتَغۡفِرۡ لِذَنۢبِكَ وَلِلۡمُؤۡمِنِينَ وَٱلۡمُؤۡمِنَٰتِۗ وَٱللَّهُ يَعۡلَمُ مُتَقَلَّبَكُمۡ وَمَثۡوَىٰكُمۡ﴾

{Basi jua ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah, na omba maghufira kwa dhambi zako na za Waumini wanaume na Waumini wanawake. Na Allah anajua mahali penu pa kwenda na kurudi, na mahali penu pa kukaa} [Muhammad: 19].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi Waislamu:**

Tawhidi ndio jambo kubwa lenye kutakasa nafsi, na wala haipatikani ila kwa kukufuru vyote vinavyo abudiwa kinyume na Allah - nayo ni maana ya Shahada -: [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Atakaye sema 'laa ilaaha illa llaah', na akakufuru yanayo abudiwa kinyume na Allah, basi mali yake na damu yake yatakuwa haramu [kuyafanyia uadui], na hesabu yake ni juu ya Allah mwenye ushindi na utukufu**», imepokewa na Muslim, na atakaye itekeleza Tawhidi majanga yake yataondoka, atapata Radhi za Allah, amali zake zitakubaliwa, malipo yake yatakuwa maradufu, maisha yake yatakuwa mazuri, madhambi yake yatasamehewa, na ataingia Peponi bila ya kuhesabiwa wala kuadhibiwa, wala hakuna neema kubwa zaidi kuliko neema ya Dini na kuwa imara juu yake.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# UTUKUFU WA ALLAH[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakaye mpoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Enyi waja wa Allah, mcheni Allah haki ya kumcha, na kamateni Uislamu katika kishiko madhubuti kabisa.

**Enyi Waislamu:**

Allah amewaleta waja kutoka kutokuwepo, akawapa neema, akawaondolea majanga na mzito, na maumbile yaliosalimika yanampenda aliye waneemesha na kuwafanyia ihsani, na haja ya nafsi kumjua Mola wao Mlezi ni kubwa kuliko haja yao ya chakula, kinywaji na pumzi, wala hakuna saada duniani na akhera ila kwa kumtambua Allah, kumpenda na kumuabudu, mtu anayemtambua zaidi ndiye mwenye kumuadhimisha zaidi na kumuamini zaidi.

Na ibada za moyo ni kubwa kuliko ibada za viungo, na ni nyingi zaidi na za kudumu zaidi, kwani ni wajibu katika wakati wote, nazo amali za viungo ni kwa lengo la kuutengeneza moyo; ibnul Qayyim Allah amrehemu amesema: "Na Allah anamueka mja katika Nafsi yake cheo kile kile mja anachomuweka Yeye katika nafsi yake mja", na kiumbe anapomtambua Mola wake Mlezi; basi nafsi yake hupata utulivu Kwake, na moyo wake

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe kumi na nane, mwezi wa Jumaada Al-Ulaa, mwaka elfu moja mia nne na thalathini na mbili hijria, katika Msikiti wa Mtume swal na salamu za Allah zimshukie.

hutulia, na atakayekuwa mjuzi zaidi wa kumjua Allah na Sifa zake, basi kumtegemea kwake Allah kutakuwa sahihi zaidi na kutakuwa na nguvu zaidi, na mtu aliye mkamilifu zaidi kiibada ya Allah: ni yule mwenye kumuadhimisha Allah, na mwenye kumuabudu kwa Majina yake yote na Sifa zake zote.

Na Allah aliyetakasika ana Majina yalio mazuri zaidi - Majina yake ni sifa na taadhima -, ana Sifa za juu zaidi - na Sifa zake ni za ukamilifu -, na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akisema katika rukuu yake: «umetakasika mwenye kukahiri, mwenye kumiliki, mwenye kiburi na utukufu», imepokewa na Nasai, ana ukamilifu usio na mipaka katika kila jambo, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alikuwa akisema:

«**siwezi kukamilisha kukusifu, Wewe ni kama ulivyo jisifu Nafsi yako**», imepokewa na Muslim.

Na vyote vilivyo mbinguni na ardhini vinamtakasa Allah kutokana na kila aibu na kasoro, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿سَبَّحَ لِلَّهِ مَا فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِي ٱلْأَرْضِۖ وَهُوَ ٱلْعَزِيزُ ٱلْحَكِيمُ﴾

{Kinamsabihi kumtakasa Allah kila kiliomo ndani ya mbingu na ardhi. Na Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima} [Al-Hashr: 1]. na vyote vinamsujudia; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَلِلَّهِ يَسْجُدُ مَا فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِي ٱلْأَرْضِ مِن دَآبَّةٍ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةُ وَهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُونَ﴾

{Na vyote viliomo katika mbingu na katika ardhi, tangu wanyama mpaka Malaika, vinamsujuidia Allah, na wala havitakabari}. [An-Nahl: 49].

Uumbaji na amri ni zake Yeye aliyetakasika peke yake, amekifanya barabara alicho kitengeneza, na amekifanya vizuri alichokiumba, na amekadiria makadirio ya viumbe kabla hata kuumba mbingu na ardhi kwa miaka elfu hamsini, na hukumu ni yake, hashirikiani Naye yeyote katika hilo, hakuna wa kurudisha kudura yake, wala wa kupinga hukumu yake, ni aliye hai asiye kufa, viumbe vyote vimo chini ya ukahiri wake na ukamataji wake, anawafisha na kuwahuisha, anawachekesha na kuwaliza,

amewakwasisha na kuwafukarisha, na awatia sura wakiwa ndani ya vizazi namna anavyotaka.

﴿مَّا مِن دَآبَّةٍ إِلَّا هُوَ ءَاخِذُۢ بِنَاصِيَتِهَآ﴾

{Hapana kiumbe yeyote ila Yeye anamwendesha atakavyo}, [Huud: 56]

anakiendesha anavyotaka, na nyoyo za waja zimo baina ya Vidole vyake viwili, anazigeuza geuza anavyotaka, na vipaji vyao vimo Mkononi mwake, na hatamu za mambo zimefunganishwa na hukumu yake na kadari yake.

Hashindani naye yeyote, wala yeyote hamghilibu, lau umma wote utakusanyika ili kumdhuru mtu ambaye Allah hajamuandikia madhara hayo; hataweza yeyote kumdhuru, na lau watakusanyika ili kumnufaisha, na hali Allah hajataka hilo; basi hataweza yeyote kumnufaisha.

Hakuna mwenye kuirudisha adhabu yake inaposhuka, wala hakuna mwenye kuiondoa iwapo imeteremka ila Yeye, anaumba anachokitaka, na anafanya alitakalo

﴿لَا يُسۡـَٔلُ عَمَّا يَفۡعَلُ﴾

{Yeye hahojiwi kwa ayatendayo}, [Al-Anbiya`: 21]

Na viumbe wanahojiwa, amesimama kwa Nafsi yake, hawahitajii viumbe vyake, na amewatawala wote, funguo za ghaibu ziko kwake, hakuna anayeyajua ila Yeye, na ameificha elimu yake [ghaibu] hata kwa Malaika, basi walio mbinguni hawajui yatakayo tokea kesho au duniani kabla hayajakua.

Ni Mmiliki anaendesha amri ya waja wake, anaamrisha akikataza, anatoa akinyima, anaangusha akinyanyua, amri zake ni zenye kuandamana kwa kuandamana nyakati, ni zenye kupita kulingana na matakwa yake, basi alitakalo litakuwa, na asiolitaka haliwi

﴿يَسۡـَٔلُهُۥ مَن فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضِۚ كُلَّ يَوۡمٍ هُوَ فِي شَأۡنٍ﴾

{Vinamwomba Yeye vilivyomo katika mbingu na ardhi. Kila siku Yeye yumo katika mambo}, [Ar-Rahman: 29].

Na ni katika jumla ya mambo yake: kuondoa janga, kuunga palipovunjika, kumkwasisha fakiri, kuitikia maombi, alisema kuihusu Nafsi yake:

﴿وَمَا كُنَّا عَنِ ٱلۡخَلۡقِ غَٰفِلِينَ﴾

{Nasi hatukuwa wenye kughafilika na viumbe}. [Al-mu`minuun: 17].

Elimu yake imeenea kila kitu, anajua yaliyokuwa, yanayokuwa na yatakayokuwa, na ambayo hayajakuwa, haitetemeki chembe ndogo na ilio kubwa zaidi yake ila kwa idhini yake, wala halianguki jani ila kwa elimu yake, haifichamani kwake chochote, ni sawa kwake siri na dhahiri; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿سَوَآءٞ مِّنكُم مَّنۡ أَسَرَّ ٱلۡقَوۡلَ وَمَن جَهَرَ بِهِۦ وَمَنۡ هُوَ مُسۡتَخۡفِۭ بِٱلَّيۡلِ وَسَارِبُۢ بِٱلنَّهَارِ﴾

{Ni sawa anaye ficha kauli yake kati yenu na anaye idhihirisha, na anaye jibanza usiku na anaye tembea jahara mchana}. [Ar-Ra`ad: 10].

Anasikia sauti za viumbe na hali Yeye yupo juu ya Arshi yake, Aisha Allah amridhie amesema: «Sifa njema zote anastahiki Allah ambaye uskizi wake umeenea sauti zote, hakika alikuja yule mwanamke mwenye kujadili kwa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anamzungumzisha, na hali mimi niko pembeni mwa nyumba sisikii anachosema, Allah mwenye ushindi na utukufu akateremsha:

﴿قَدۡ سَمِعَ ٱللَّهُ قَوۡلَ ٱلَّتِي تُجَٰدِلُكَ فِي زَوۡجِهَا وَتَشۡتَكِيٓ إِلَى ٱللَّهِ وَٱللَّهُ يَسۡمَعُ تَحَاوُرَكُمَآۚ إِنَّ ٱللَّهَ سَمِيعُۢ بَصِيرٌ﴾

{Allah amekwisha sikia usemi wa mwanamke anaye jadiliana nawe juu ya mumewe, na anamshitakia Allah. Na Allah anayasikia majibizano yenu. Hakika Allah ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona} », [Al-mujadalah: 1] imepokewa na Ahmad.

Na matendo ya waja yakiwa ndani ya giza la usiku wenye giza kali si yenye kufichamana kwake; [Allah] mwenye shani tukufu amesema:

﴿ٱلَّذِى يَرَىٰكَ حِينَ تَقُومُ ۞ وَتَقَلُّبَكَ فِى ٱلسَّٰجِدِينَ﴾

{Ambaye anakuona unapo simama * Na mageuko yako kati ya wanao sujudu} [Ash-shu`ara`: 218-219].

anaona kutambaa kwa chungu mweusi juu ya jiwe manga ndani ya usiku wa giza na hali Yeye yupo juu ya mbingu zake.

Hazina zake za mbinguni na ardhini zimejaa, na Mikono yake miwili imekunjuka kwa utoaji, «Mtoaji wa usiku na mchana», anatoa namna anavyo taka, mwingi wa vipawa, mkunjufu wa ukarimu, anatoa kabla hajaombwa na baada ya kuombwa, na anashuka

«**kila usiku hadi mbingu ya [karibu na] dunia pindi inaposalia thuluthi ya mwisho ya usiku, akawa anasema: Ni nani ataniita ni muitikie? Ni nani ataniomba nimpatie?** », na humkasirikia asiyemuomba.

Na ameifungua milango ya vipawa vyake kwa waja wake; akazidhalilisha bahari, akaitembeza mito, na akateremsha riziki. Anawaletea waja riziki zao; akamruzuku chungu akiwa ndani ya ardhi [chini ya dongo], na ndege akiwa katika hewa, na samaki wakiwa ndani ya maji:

﴿وَمَا مِن دَآبَّةٍ فِى ٱلْأَرْضِ إِلَّا عَلَى ٱللَّهِ رِزْقُهَا﴾

{Na hakuna mnyama yoyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Allah}, [Huud: 6]

Na riziki yake imeenea kila kitu; basi anamletea mtoto riziki yake akiwa ndani ya uzazi wa mamake, na mwenye nguvu akiwa katika milki yake, ni Mkarimu anapenda kutoa kwa ukarimu, akiombwa hutoa, na haridhii kufikishwa mahitaji kwa mwengine, na heri zote zatoka Kwake

﴿وَمَا بِكُم مِّن نِّعْمَةٍ فَمِنَ ٱللَّهِ﴾

{Na neema yoyote mliyo nayo inatoka kwa Allah} [An-Nahl: 53].

Riziki yake haiishi; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Mwaonaje aliyoyatoa kutoka aumbe mbingu na ardhi? Basi hayajapunguza chochote yalio katika Mkono wake wa kuume**», imepokewa na Muslim, na lau waja wake wote watamuomba, naye awape wote walioyaomba; basi hilo halitapunguza chochote katika ufalme wake, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema katika aliyoyapokea kutoka kwa Mola wake Mlezi kuwa amesema:

«**Enyi waja wangu! Lau wa mwanzo wenu na wa mwisho wenu, na binadamu wenu na majini wenu, watasimama katika uwanja mmoja, wakaniomba; nami nikampa kila mtu maombi yake, hilo halitapunguza chochote katika yalio kwangu, ila kama inavyopunguza sindano inapoingizwa katika bahari**», imepokewa na Muslim.

Na Yeye huzidisha thawabu maradufu; kwake jema ni mara kumi yake hadi ziada mara mia saba, hadi ziada nyingi [zaidi ya hapo], na muda mchache wa utiifu anaukithirisha; basi 'laylatul qadr' ni bora kuliko miezi elfu moja, na kufunga siku tatu za kila mwezi ni kama kufunga mwaka mzima, na endapo mja atatoa mali kwa kukusudia Uso wake; basi Yeye humrudishia mali yale yakiwa yamezidishwa mara nyingi, na huzidisha katika ukarimu zaidi ya matamanio [ya mja], akawapa watu wa Peponi ambayo hayajaonekana na jicho, wala hayajaskika na sikio, wala hayajapita katika moyo wa mtu, na endapo mja ataacha kitu kwa ajili yake basi atampa badali iliyo bora zaidi.

Ni mkwasi hawahitaji viumbe vyote, na kila kitu ni chenye kumuhitajia Yeye,

﴿يَـٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ أَنتُمُ ٱلْفُقَرَآءُ إِلَى ٱللَّهِ ۖ وَٱللَّهُ هُوَ ٱلْغَنِىُّ ٱلْحَمِيدُ﴾

{Enyi watu! Nyinyi ndio wenye haja kwa Mwenyezi Mungu, na Allah ndiye Mkwasi, Msifiwa}, [Fatwir: 15],

waja hawaafikii kumnufaisha wakamnufaisha, wala kumdhuru wakamdhuru, aliye juu Mkuu, Kursii ni sehemu ya Miguu yake aliyetakasika, nayo Kursii imeenea mbingu na ardhi, na mbingu saba katika Kursii ni mfano wa dirhamu saba zilizotupwa ndani

ya ngao, nayo Kursii katika Arshi ni mfano wa ringi ya chuma iliyotupwa katika jangwa, na Arshi yake ndiyo kiumbe kikubwa zaidi, na chini ya Arshi kuna bahari, na wanao ibeba Arshi ni Malaika ambao baina ya ndewe ya sikio la mmoja wao na bega lake ni masafa ya mwendo wa miaka mia saba, na Mola wetu Mlezi ameenda juu ya Arshi yake - kama inavyolingana na utukufu wake - naye Allah ni Mkwasi hahitajii Arshi wala vilivyo chini yake.

Amezunguka kila kitu [kielimu], wala chochote hakimzunguki Yeye, na anayadiriki macho wala macho hayamdiriki Yeye, na uwezo wake umekusanya viumbe vyake vyote, navyo ni vidhaifu mbele yake hata vikiwa vikubwa katika macho ya viumbe, mbingu [Allah] aliyetakasika atazikunja siku ya Kiyama, kisha azichukue kwa Mkono wake wa kuume, kisha aseme:

«**Mimi ndiye Mfalme [Mmiliki], wako wapi majabari? Wako wapi wenye kiburi? Kisha azikunje ardhi kwa Mkono wake wa kushoto, kisha aseme: Mimi ndiye Mfalme [Mmiliki], wako wapi majabari? Wako wapi wenye kiburi** », imepokewa na Muslim, na ataziweka

«**mbingu katika kidole, na ardhi katika kidole, na maji na michanga katika kidole, na viumbe katika kidole, kisha avitingishe, kisha aseme: Mimi ndiye Mfalme, Mimi ndiye mfalme**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, na anapozungumza wahyi basi mbingu hutingisika na watu wa mbinguni huzimia, na wakwanza wa kupata fahamu ni Jibrili, na mbingu zinamuogopa Yeye, asema aliye na ushindi na utukufu:

﴿تَكَادُ ٱلسَّمَٰوَٰتُ يَتَفَطَّرۡنَ مِن فَوۡقِهِنَّ﴾

{Zinakaribia mbingu kupasuka juu huko}, [Ash-shuuraa: 5],

Adh-dhwahaak Allah amrehemu amesema: "zinapasuka kwa hofu ya utukufu wa Allah - yaani kwa ajili ya kumuogopa-".

«**Ndiye Msimamia mambo yote asiye lala, wala haipasi kwake kulala, anaishukisha mizani na anaipandisha, na anainyanyua kwake amali ya usiku kabla amali ya mchana,**

**na amali ya mchana kabla ya amali ya usiku, pazia yake ni nuru, lau ataiondoa, basi nuru ya Uso wake itaunguza katika viumbe vyake kila ambaye jicho lake litamfikia**» imepokewa na Muslim. Anapelekesha Yeye mambo yote

﴿مِنَ ٱلسَّمَآءِ إِلَى ٱلْأَرْضِ ثُمَّ يَعْرُجُ إِلَيْهِ فِى يَوْمٍ كَانَ مِقْدَارُهُۥٓ أَلْفَ سَنَةٍ مِّمَّا تَعُدُّونَ﴾

{yalio baina mbingu na ardhi, kisha yanapanda kwake kwa siku ambayo kipimo chake ni miaka elfu kwa mnavyo hisabu nyinyi} [As-sajda: 5].

﴿وَلَوْ أَنَّمَا فِى ٱلْأَرْضِ مِن شَجَرَةٍ أَقْلَٰمٌ وَٱلْبَحْرُ يَمُدُّهُۥ مِنۢ بَعْدِهِۦ سَبْعَةُ أَبْحُرٍ مَّا نَفِدَتْ كَلِمَٰتُ ٱللَّهِ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ﴾

{Na lau kuwa miti yote iliyomo duniani ikawa ni kalamu, na bahari (ikawa wino), na ikaongezewa juu yake bahari nyengine saba, maneno ya Allah yasingeli kwisha. Hakika Allah ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima}. [Luqman: 27].

Ni mwenye nguvu asiye shindwa na chochote, akilitaka jambo huliambia: kuwa; nalo likawa, na amri yake ni kama kupepesa kwa jicho; bali amri yake ni karibu zaidi [kuliko kupepesa kwa jicho], na ana majeshi asioyajua yeyote ila Yeye, alivigeuza vijiji vya kaumu ya luut, akavijaalia juu chini, na pindi wana wa Isaraili walipo kataa kukubali yaliyo ndani ya Taurati alilinyanyua jabali juu ya vichwa vyao likawa kama wingu, na wakayakinisha kuwa litawaangukia, naye aliyetakasika alijidhihirisha kwa jabali, nalo likawa vipande vipande, na Musa [salamu zimshukie] alipoona hayo alianguka akazimia.

Na wakati utakapoisha [Allah] ataitingisa ardhi na aivunje vipande vipande, na atayavuruga vuruga majabali, kwa mpulizo mmoja tu atakao puliza Israfil katika parapanda viumbe watababaika, na kwa mpulizo wa pili watakufa, na kwa wa tatu watainuka ili kukusanywa, na pindi atakaposhuka aliye takasika ili kuhukumu; mbingu zitapasuka kwa kushuka kwake kwa kumuadhimisha na kumuogopa.

Na Allah aliye takasika yupo juu ya wanavyo msifu wenye

kumsifu, hana mshirika, wala hana mfano, Mitume walimtambua Mola wao Mlezi basi wakakithirisha kumdhalilikia, kumuabudu na kumyenyekea; Daud salamu zimshukie akawa anafunga siku na akila siku, na Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie anasimama usiku akiswali hadi miguu yake ikifura, na Ibrahim salamu zimshukie ni mwingi wa kunyenyekea kwa Allah, na mwepesi wa kurejea na kutubia kwake, na atakaye fuata njia ya manabii; atapata saada na maisha bora.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿وَمَا قَدَرُواْ ٱللَّهَ حَقَّ قَدۡرِهِۦ وَٱلۡأَرۡضُ جَمِيعٗا قَبۡضَتُهُۥ يَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِ
وَٱلسَّمَٰوَٰتُ مَطۡوِيَّٰتُۢ بِيَمِينِهِۦۚ سُبۡحَٰنَهُۥ وَتَعَٰلَىٰ عَمَّا يُشۡرِكُونَ﴾

{Na wala hawakumhishimu Allah kama anavyo stahiki kadiri yake. Na Siku ya Kiyama ardhi yote itakuwa mkononi mwake, na mbingu zitakunjwa katika mkono wake wa kuume. Subhanahu wa Taa'la Ametakasika na Ametukuka na hayo wanayo mshirikisha nayo}. [Az-zumar: 67].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi Waislamu:**

Hakuna yeyote ambaye sifa zinapendeza zaidi kwake kuliko Allah, kwa sababu hiyo ndio akajisifu Nafsi yake, na asili ya kuzidiana kiubora baina ya watu ni kwa kumtambua Allah, kumpenda na kumsifu, na aliyemtambua Allah na hali moyo wake uko salama; atampenda na atamuadhimisha, na kila akizidi kumtambua ndio atazidi kumtii.

Madhambi yanadhoofisha kumtukuza Allah, na lau utamakinika utukufu wa Allah ndani ya moyo wa mja basi hangejasiri yeyote kumuasi, na maasi yote yanakuwa ni kwa sababu ya ujinga wa kutomtambua Allah.

Na kumtukuza Allah kunakua kwa matendo ya utiifu, na ibada kubwa zaidi anayo jikurubisha nayo mja kwa Mola wake Mlezi; ni kupwekesha Yeye kwa ibada, basi asiombwe ila Yeye, wala kusitakwe uokozi ila kwake, wala asipelekewe ibada yoyote ila Yeye peke yake.

Na atakaye muabudu mwengine pamoja naye; basi huyo hajatukuza haki ya cheo chake ipasavyo, na atakuwa amejidhulumu nafsi yake kwa kuingia katika shirki, na atakayeongozwa na Allah katika kumuadhimisha Mola Mlezi na kumpwekesha kwa ibada; itakuwa wajibu juu yake kumlingania mwengine katika kumpwekesha Allah na kumuadhimisha.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# KUMUADHIMISHA ALLAH[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakaye mpoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Enyi waja wa Allah, mcheni Allah haki ya kumcha, na kamateni Uislamu katika kishiko madhubuti kabisa.

**Enyi Waislamu:**

Utukufu wa elimu unapimwa kwa utukufu wa kile kinachojulikana [kwa elimu ile], na kitukufu zaidi na kitakatifu zaidi kati ya vinavyojulikana ni kumjua Allah, na haja ya kumtambua Allah aliye takasika na kumuadhimisha iko juu ya haja zote; bali hilo ndio msingi wa mambo ya dharura [haja za lazima].

Na Allah amewapa waja wake maumbile ya kumpenda na kumtambua, na hakika si mengine moyo umeumbwa kwa ajili ya hilo:

﴿فِطۡرَتَ ٱللَّهِ ٱلَّتِي فَطَرَ ٱلنَّاسَ عَلَيۡهَاۚ لَا تَبۡدِيلَ لِخَلۡقِ ٱللَّهِ﴾

{ndilo umbile la Allah alilo waumbia watu. Hapana mabadiliko katika uumbaji wa Allah} [Ar-Ruum: 30] nalo ndio 'Al-Haniifiyyah' ambayo kila kinachozaliwa huzaliwa juu yake, na mashetani wa kijini na wa kibinadamu wanafanya bidii

---

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe ishirini na nne, mwezi wa Jumadal Ulaa, mwaka elfu moja mia nne na thalathini na saba hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

kupotosha maumbile ya viumbe, Allah alisema katika Hadithi Qudsi:

«**Nimewaumba waja wangu wote wakiwa 'Hunafa-a' [wakiwa katika umbile la 'Al-Haniifiyyah'], nao walijiwa na mashetani; wakawaepusha na Dini yao**», imepokewa na Muslim, kila Muisilamu ameamrishwa kuchunga umbile lake, lipate kurudi [umbile] lile liliopotoka katika asili yake, na wapate kuzidi Imani wale walioamini.

Na Allah amesimamisha alama zake ziwe dalili juu ya Ulezi wake na kustahili kwake ibada, na lau bahari ingekuwa wino, na zikaletwa bahari nyengine zikaongezwa juu yake, basi hayataisha maneno ya Allah na alama zake za kumtambulisha.

Na Mitume walitumilizwa ili kukitisha umbile [la kumpenda Allah na kumtambua] na kulikamilisha, na Tawhidi ya 'Rubuubiyyah' kwa kumpwekesha Allah kwa matendo yake ni miongoni mwa makubwa waliokuja nayo Mitume, kwani huo ni msingi miongoni mwa misingi ya Imani, na ni mojawapo ya aina za Tawhidi ambazo kwa ajili yake Allah amewaumba waja, nayo ni dalili ya kupwekeka kwake katika 'Uluuhiyyah' [kustahiki kuabudiwa], na Allah ametolea hoja nayo [Tawhidi ya Rubuubiyyah] juu ya ulazima wa kumpwekesha Yeye na Ibada, na shirki ndani yake [Tawhidi ya Rubuubiyyah] ni aina nzito zaidi na mbaya zaidi, wala hakosei katika Tawhidi ya Uluuhiyyah ila yule ambaye hakuipa [Tawhidi ya Rubuubiyyah] haki yake.

Na Allah aliye takasika amekamilika katika dhati yake, sifa zake na matendo yake, na ni miongoni mwa sifa zake aliye mtukufu wa shani: Ulezi [Rubuubiyyah]; hana mshirika naye ndani yake, kama vile hana mshirika naye katika ibada [Uluuhiyyah], [Allah] aliye tukuka amesema:

﴿قُلۡ أَغَيۡرَ ٱللَّهِ أَبۡغِي رَبّٗا وَهُوَ رَبُّ كُلِّ شَيۡءٖ﴾

{Sema: Je nitafute Mola Mlezi asiye kuwa Allah, na hali Yeye ndiye Mola Mlezi wa kila kitu?} [Al-an`aam: 164].

Naye aliye takasika amepwekeka na uumbaji, umiliki, kuruzuku, na uendeshaji, ni muumba wala hakuna muumba pamoja naye, muumba wa mbingu na ardhi pasina ruwaza, aliumba, na akaweka sawa, na ametengeneza vizuri umbo la kila kitu, naye ndiye Muumbaji Mjuzi, na kama alivyo anzisha viumbe basi atawarudisha siku ya Kiyama, bali hilo ndilo pesi zaidi kwake, na kila asiyekuwa Allah hastahiki kufanyiwa ibada, na Allah ndiye anaye zistahiki peke yake, kwa sababu Yeye ndiye muumba:

﴿أَفَمَن يَخْلُقُ كَمَن لَّا يَخْلُقُۚ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ﴾

{Ati anaye umba ni kama asiye umba? Basi hebu, hamkumbuki?} [An-Nahl: 17].

Naye aliye takasika ndiye Mfalme, na ufalme ni wake:

﴿ذَٰلِكُمُ ٱللَّهُ رَبُّكُمْ لَهُ ٱلْمُلْكُۚ وَٱلَّذِينَ تَدْعُونَ مِن دُونِهِۦ مَا يَمْلِكُونَ مِن قِطْمِيرٍ﴾

{Huyo ndiye Allah Mola wenu Mlezi. Ufalme ni wake. Na hao mnao waomba badala yake hawamiliki hata ugozi wa kokwa ya tende} [Fatwir: 13]

Naye ndiye Mmiliki wa viumbe vyake, ni vyake vilivyo mbinguni na ardhini, na viumbe ni vyenye kunyenyekea kwake na kumsabihi, na wote ni wenye kumsujudia.

Yeye ndiye Bwana hana mshirika naye, na wote [wasiokuwa Yeye] ni watumwa wake:

﴿إِن كُلُّ مَن فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ إِلَّآ ءَاتِي ٱلرَّحْمَٰنِ عَبْدًا﴾

{Hapana yeyote aliomo mbinguni na ardhini ila atafika kwa Arrahmani Mwingi wa Rehema kuwa ni mtumwa wake} [Maryam: 93] anao Yeye ufalme uliotimia wenye kudumu, Mmiliki wa dunia na Siku ya malipo, na Siku ya mwisho atadhihiri na aseme:

﴿لِّمَنِ ٱلْمُلْكُ ٱلْيَوْمَ﴾

{ufalme ni wa nani leo?}; [Ghafir: 16].

Basi ajijibu Nafsi yake kwa kusema:

﴿لِلَّهِ ٱلۡوَٰحِدِ ٱلۡقَهَّارِ﴾

{Ni wa Allah Mmoja Mtenda nguvu}. [Ghafir: 16].

Aliye takasika amepwekeka na kuendesha mambo ya viumbe vyake na ufalme wake, kwani amri yote iko Mkononi mwake peke yake:

﴿أَلَا لَهُ ٱلۡخَلۡقُ وَٱلۡأَمۡرُۗ﴾

{Fahamuni! Kuumba na amri ni zake} [Al-a`raaf: 54],

Anaamrisha na anakataza, anaumba na anaruzuku, anatoa na ananyima, anaangusha na ananyanyua, anapatia ushindi na anadhalilisha, anahuisha na anafisha:

﴿يُكَوِّرُ ٱلَّيۡلَ عَلَى ٱلنَّهَارِ وَيُكَوِّرُ ٱلنَّهَارَ عَلَى ٱلَّيۡلِۖ وَسَخَّرَ ٱلشَّمۡسَ وَٱلۡقَمَرَ﴾

{Hufunika usiku juu ya mchana, na hufunika mchana juu ya usiku. Na amefanya jua na mwezi vitumike}, [Az-zumar: 5],

﴿يُخۡرِجُ ٱلۡحَيَّ مِنَ ٱلۡمَيِّتِ وَيُخۡرِجُ ٱلۡمَيِّتَ مِنَ ٱلۡحَيِّ وَيُحۡيِ ٱلۡأَرۡضَ بَعۡدَ مَوۡتِهَا﴾

{Hukitoa kilicho hai kutokana na kilicho kufa, na hukitoa kilicho kufa kutokana na kilicho hai. Na huihuisha ardhi baada ya kufa kwake}. [Ar-ruum: 19],

Viumbe vyote viko chini ya kahari yake na matakwa yake, na nyoyo za waja na vipaji vyao vimo Mkononi mwake, na hatamu za mambo zimefungwa na hukumu yake na kudura yake, mwenye kusimamia kila nafsi kwa iliyo yachuma, na mbingu na ardhi zimesimama kwa amri yake,

﴿وَيُمۡسِكُ ٱلسَّمَآءَ أَن تَقَعَ عَلَى ٱلۡأَرۡضِ إِلَّا بِإِذۡنِهِۦٓ﴾

na {amezishika mbingu zisianguke juu ya ardhi ila kwa idhini yake}, [Al-Hajj: 65]

﴿يُمۡسِكُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضَ أَن تَزُولَا﴾

Na {ndiye anaye zuilia mbingu na ardhi zisiondoke} [Fatwir: 41]

na kilicho mbinguni na ardhini kinamuomba Yeye,

﴿كُلَّ يَوۡمٍ هُوَ فِي شَأۡنٖ﴾

{Kila siku Yeye yumo katika mambo} [Ar-rahman: 29], na ni katika jumla ya mambo yake: husamehe dhambi, humuongoza aliyepotea, hufariji hamu, huunga palipovunjika, humkwasisha fakiri, huitikia maombi, [Allah] aliye tukuka amesema:

﴿وَمَا كُنَّا عَنِ ٱلۡخَلۡقِ غَٰفِلِينَ﴾

{Nasi hatukuwa wenye kughafilika na viumbe}. [Al-mu`minuun: 17].

Amri zake ni zenye kuandamana, na matakwa yake ni yenye kupita, tembe ndogo kabisa ulimwenguni haitingisiki ila kwa idhini yake, basi alitakalo linakuwa, na asiolitaka haliwi, anaumba akitakacho na anafanya alitakalo, na amri yake ni kudura iliyo kwisha kadiriwa [isio budi kuwa], hakuna wakuzuia alichokitoa, wala wa kutoa alichokizuia, hakuna wa kupinga hukumu yake wala wakurudisha kudura yake, wala wa kuzuia matakwa yake, wala wa kubadili maneno yake, amekadiria makadiro ya viumbe kabla ya kuumba mbingu na ardhi kwa miaka elfu hamsini, na lau viumbe watakusanyika juu ya jambo ambalo Allah hajaliandika ili walifanye liwe; hawataweza hilo, na lau watakusanyika juu ya lile ambalo ni lenye kuwa ili walizuie; basi hawataweza hilo, na lau umma utakusanyika juu ya kumdhuru mja ambaye Allah hajataka adhurike basi hawatamdhuru, na lau utakusanyika juu ya kumnufaisha, na hali Allah hajaidhinisha anufaike basi hawatamnufaisha, humuongoza anaye mtaka kwa fadhila zake, na humpoteza anaye mtaka kwa uadilifu wake, anapolitaka jambo basi huliambia kuwa; nalo likawa:

﴿لَا يُسۡـَٔلُ عَمَّا يَفۡعَلُ وَهُمۡ يُسۡـَٔلُونَ﴾

{Yeye hahojiwi kwa ayatendayo, na wao ndio wanao hojiwa kwa wayatendayo} [Al-anbiya`: 23].

Maneno yake ndio maneno mazuri zaidi, maneno yake hayana mwanzo wala hayana mwisho:

﴿وَلَوۡ أَنَّمَا فِي ٱلۡأَرۡضِ مِن شَجَرَةٍ أَقۡلَٰمٞ وَٱلۡبَحۡرُ يَمُدُّهُۥ مِنۢ بَعۡدِهِۦ سَبۡعَةُ أَبۡحُرٖ مَّا نَفِدَتۡ

﴿كَلِمَٰتُ ٱللَّهِ﴾

{Na lau kuwa miti yote iliyomo duniani ikawa ni kalamu, na bahari (ikawa wino), na ikaongezewa juu yake bahari nyengine saba, maneno ya Allah yasingeli kwisha}. [Luqman : 27],

Na elimu yake aliyetukuka imeenea kila kitu, ajua yaliokuwa, yanayokuwa, ambayo hayakuwa, na ambayo hayatokuwa, na ajua wanaoyafanya viumbe na watakaoyafanya, na ajua yalio barani na baharini, na halianguki jani ila analijua,

﴿مِثْقَالُ ذَرَّةٍ فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَلَا فِي ٱلْأَرْضِ﴾

{Hapana kinacho fichikana kwake hata chenye uzito wa chembe tu, si katika mbingu wala katika ardhi} [Saba`: 3], anajua yalioghibu kwetu na tunayo yashuhudia, ajua wasiwasi wa nafsi, na yaliofichika katika vifua, na ajua anachokibeba mwanamke ndani ya tumbo, na funguo za ghaibu hakuna azijuae ila Yeye, na elimu za viumbe wote ni kama tone [la maji] katika bahari ya elimu yake, na haikuwa elimu yao ila kwa kutaka kwake, kindege kilidona katika bahari, basi Al-khidhru akamuambia Musa salamu ziwashukie: «**elimu yangu na elimu yako hazijapunguza katika elimu ya Allah ila mfano wa kindege hiki kilivyopunguza katika bahari**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Usikizi wake umeenea sauti zote, basi hazihitalifiani kwake wala hazifanani; mwanamke alimshitakia mumewe kwa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, na hali Aisha Allah amridhie yupo pembeni mwa nyumba, na baadhi ya maneno yake yanafichana kwake [hayasikii], na Allah ameyasikia maneno yake kutoka juu ya mbingu ya saba na akateremsha [aya]:

﴿قَدْ سَمِعَ ٱللَّهُ قَوْلَ ٱلَّتِي تُجَٰدِلُكَ فِي زَوْجِهَا وَتَشْتَكِيٓ إِلَى ٱللَّهِ وَٱللَّهُ يَسْمَعُ تَحَاوُرَكُمَآ﴾

{Allah amekwisha sikia usemi wa mwanamke anaye jadiliana nawe juu ya mumewe, na anamshitakia Allah. Na Allah anayasikia majibizano yenu}, [Al-mujadalah: 1].

Na uoni wake umezunguka kila kinachoonekana, basi

matendo ya waja yakiwa ndani ya giza la usiku hayafichani kwake, Naye ni mwenye kuyasimamia matendo yao yote wala hayampiti.

Na kwa kuwa viumbe ni vyake Yeye basi hukumu ni yake peke yake; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿إِنِ ٱلۡحُكۡمُ إِلَّا لِلَّهِ﴾

{Hapana hukumu ila ya Allah}, [Al-an`aam: 51],

Na hukumu zake, mipaka yake, na sheria zake ndio hukumu bora zaidi, wala hakuna aliye mzuri zaidi wa hukumu kuliko Yeye,

﴿وَهُوَ خَيۡرُ ٱلۡحَٰكِمِينَ﴾

{Naye ndiye Mbora wa wenye kuhukumu}. [Al-a`raaf: 87],

Anahukumu wala hakuna wa kupinga hukumu yake

﴿وَلَا يَظۡلِمُ رَبُّكَ أَحَدٗا﴾

{Na Mola wako Mlezi hamdhulumu yeyote}, [Al-kahf: 49],

Hakuna mwenye huruma kuliko Yeye, basi Yeye ndiye mwingi wa wenye kurehemu na mbora wao, ni mwenye kurehemu kuliko mama mzazi kwa mwanaye, rehema zake zimeenea kila kitu, anazo aliyetakasika rehema mia moja; ameteremsha moja, ndio waja wanarehemeana kwayo baina yao, na amezuia kwake [rehema] tisaini na tisa.

Ni Mkarimu hakuna mkarimu kuliko Yeye, apenda kuwafanyia ihsani na kuwapa viumbe vyake, anawaruzuku kutoka juu yao na chini yao, fadhila zake ni kubwa na hazina zake haziishi,

﴿قُلۡ مَن يَرۡزُقُكُم مِّنَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضِ﴾

{Sema: Ni nani anaye kuruzukuni kutoka mbinguni na kwenye ardhi?} [Saba`: 24], na Mkono wake umejaa haupungui kwa kutoa, «Mtoaji sana usiku na mchana», [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Mwaonaje aliyoyatoa kutoka aumbe mbingu na ardhi? Basi hayajapunguza chochote yalio katika Mkono wake**»,

wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, anaitikia maombi ya waja, [Allah] aliye takasika amesema:

﴿وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌۖ أُجِيبُ دَعْوَةَ ٱلدَّاعِ إِذَا دَعَانِ﴾

{Na waja wangu watakapo kuuliza khabari zangu, waambie kuwa Mimi nipo karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anaponiomba} [Al-Baqarah: 186],

wala hakuna mahitaji yatakuwa makubwa kwake asiweze kuyatoa, na lau kuwa waja - wa kwanza wao na wa mwisho wao, binadamu wao na jini wao - watasimama katika kiwanja kimoja wakamuomba, basi akampa kila moja wao maombi yake, hilo halitapunguza kitu katika yalio kwake ila kama sindano inapunguza inapoingizwa katika bahari.

Naye aliye takasika amedhamini kuruzuku viumbe vyote katika binadamu na majini, Muisilamu wao na kafiri wao –

﴿وَمَا مِن دَآبَّةٍ فِي ٱلْأَرْضِ إِلَّا عَلَى ٱللَّهِ رِزْقُهَا﴾

{Na hakuna mnyama yoyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Allah} [Huud: 6],

Naye ni mbora wa wenye kuruzuku, amefungua milango ya heri kwa waja wake, akazidhalilisha bahari, akaitembeza mito, na akateremsha riziki, amewapa waja wake neema nyingi hali wao hawajamuomba hizo neema, na amewapa kila walilomuomba, na anawaita waja wake wamuombe, akisema kila usiku: «**Ni nani ataniomba nimpatie?** », wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea. Kila heri imetoka kwake:

﴿وَمَا بِكُم مِّن نِّعْمَةٍ فَمِنَ ٱللَّهِ﴾

{Na neema yoyote mliyo nayo inatoka kwa Allah} [An-Nahl: 53],

na kila kiumbe amemfikishia riziki yake, akamruzuku mtoto akiwa ndani ya tumbo la mamake, na chungu akiwa shimoni mwake, na ndege wakiwa angani, na samaki wakiwa ndani ya maji:

﴿وَكَأَيِّن مِّن دَآبَّةٍ لَّا تَحْمِلُ رِزْقَهَا ٱللَّهُ يَرْزُقُهَا وَإِيَّاكُمْ﴾

{Na wanyama wangapi hawawezi kujimilikia riziki zao! Allah anawaruzuku hao na nyinyi pia}. [Al-Ankabuut: 60].

Yeye yuko karibu [na waja wake] na ni mwenye kuitikia maombi, na humkasirikia asiye muomba, na aliyenyimwa ni yule anayemtumai asiyekuwa Mola wake Mlezi, wala hakuna yeyote mwenye kusubiria udhia zaidi ya Allah, wanamshirikisha, na wanamdaia kuwa na mtoto, kisha anawaafu na anawaruzuku.

Amewaafikia - kwa fadhila na ukarimu wake - wenye kumtii, na baada ya kuwaafikia akawalipa thawabu. Ni mwenye kushukuru sana, hulipa mema kwa [ibada] chache na hukithirisha malipo kwa [ibada ilio] nyingi, kwake [malipo ya] jema moja ni [kuanzia] mara kumi yake hadi nyongeza nyingi, na amewaandalia waja wake Peponi [neema] ambazo jicho halijawihi kuona, wala sikio halijawahi kusikia, wala hayajawahi kupita kama fikra tu katika moyo wa mtu, na hataacha kuwaridhisha [watu wa Peponi] akisema:

«**Je mmeridhika? Nao waseme: Na tuna nini hata tusiridhike na hali umetupa ambayo hujampa yeyote katika viumbe vyake! Basi aseme: Mimi nitawapa lilio bora zaidi kuliko hayo. Basi waseme: Ewe Mola wetu Mlezi! Na ni jambo gani bora zaidi kuliko haya? Aseme: Nitawateremshia Radhi zangu, wala sitawakasirikia baada yake kabisa**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Ni mkwasi kwa dhati yake, ni 'Swamad' [anaye kusudiwa kukidhi mahitaji]; viumbe vinamkusudia katika mahitaji yao, ni Bwana aliye kamilika hakuna faragha ndani yake:

﴿لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ * وَلَمْ يَكُن لَّهُۥ كُفُوًا أَحَدٌۢ﴾

{Hakuzaa wala hakuzaliwa * Wala hana anaye fanana naye hata mmoja} [Al-ikhlaas: 3-4],

﴿مَا ٱتَّخَذَ صَٰحِبَةً وَلَا وَلَدًا﴾

{hana mke wala mwana} [Al-Jinn: 3],

﴿وَلَمْ يَكُن لَّهُۥ شَرِيكٌ فِى ٱلْمُلْكِ وَلَمْ يَكُن لَّهُۥ وَلِىٌّ مِّنَ ٱلذُّلِّ﴾

{wala hana mshirika katika ufalme, wala hana rafiki wa kumsaidia kwa sababu ya udhaifu wake}, [Al- Israa : 111]

﴿وَمَا كَانَ مَعَهُۥ مِنۡ إِلَٰهٍۚ﴾

{wala hanaye muabudiwa mwengine pamoja naye} [Al-mu`minuun: 91],

hatiiwi ila kwa sababu ya fadhila yake, na haasiwi ila kwa kujua kwake, hahitajii viumbe vyake, anasimama kwa Nafsi yake, na kila kitu kinasimama kwa kumtegemea Yeye, kinamuhitajia Yeye:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ أَنتُمُ ٱلۡفُقَرَآءُ إِلَى ٱللَّهِۖ وَٱللَّهُ هُوَ ٱلۡغَنِيُّ ٱلۡحَمِيدُ﴾

{Enyi watu! Nyinyi ndio wenye haja kwa Allah, na Allah ndiye Mwenye kujitosha, Msifiwa} [Fatwir: 15],

utiifu wa wenye kutii haumnufaishi, wala uasi wa wenye kuasi haumdhuru, na lau binadamu na majini wangekuwa na moyo kama wa mtu mmoja mchamgu zaidi, hilo halingezidisha kitu katika ufalme wake, na lau wangekuwa na moyo kama wa mtu mmoja muovu zaidi, hilo halingepunguza kitu katika ufalme wake, waja hawatafikia kumnufaisha wakamnufaisha, wala kumdhuru wakamdhuru.

Aliye hai, Msimamia mambo yote milele, hashikwi na usingizi mwepesi wala usingizi mzito, anateremsha mizani [ya uadilifu na ya riziki] na anainyanyua: «**anainyanyua kwake amali ya usiku kabla ya amali ya mchana, na amali ya mchana kabla ya amali ya usiku, pazia yake ni nuru, lau ataifungua nuru ya Uso wake itaunguza katika viumbe vyake kila ambaye jicho lake litamfikia**».

Ni Mkubwa Mtukufu, Jabari Mwenye nguvu, ushindi ndio izari yake, na kiburi ndio ridai yake, ni mwenye nguvu hakuna wa kumshinda, aliye juu hana mfano wake, vitu vyote vinaangamia ila Uso wake.

Amezunguka kila kitu [kielimu] na hakuna kitu kinacho mzunguka Yeye:

﴿لَّا تُدۡرِكُهُ ٱلۡأَبۡصَٰرُ وَهُوَ يُدۡرِكُ ٱلۡأَبۡصَٰرَ﴾

{Macho hayamfikilii bali Yeye anayafikilia macho} [Al-an`aam: 103],

﴿وَٱلۡأَرۡضُ جَمِيعٗا قَبۡضَتُهُۥ يَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِ وَٱلسَّمَٰوَٰتُ مَطۡوِيَّٰتُۢ بِيَمِينِهِۦ﴾

{Na Siku ya Kiyama ardhi yote itakuwa mkononi mwake, na mbingu zitakunjwa katika mkono wake wa kuume} [Az-zumar: 57],

Hakutakwi uombezi Naye kwa yeyote katika viumbe vyake, wala hakuna yeyote awezaye kuombea mbele yake ila kwa idhini yake, na 'Kursii' yake - sehemu ya Miguu yake - imeenea mbingu na ardhi, na

«**Kursii si chochote katika Arshi ila kama ringi ya chuma iliyotupwa katika jangwa**».

Na Arshi ndio kiumbe kikubwa zaidi, inabebwa na Malaika ambao baina ya ndewe ya sikio la mmoja wao hadi begani mwake ni masafa ya mwendo wa miaka mia saba.

Na Allah ameenda juu ya Arshi yake - kama inavyo lingana na utukufu wake - Naye haihitajii Arshi na vilivyo chini yake:

﴿تَكَادُ ٱلسَّمَٰوَٰتُ يَتَفَطَّرۡنَ مِن فَوۡقِهِنَّ﴾

{Zinakaribia mbingu kupasuka juu huko} [Ash-shuuraa: 5].

kwa hofu ya utukufu wa Allah, na anapozungumza wahyi mbingu zinatetemeka mtetemeko mkubwa, na walio mbinguni wanazimia, na huanguka kumsujudia.

Yeye ni wa Kwanza wala hakuna kitu kabla yake, na ni wa mwisho wala hakuna kitu baada yake, na wa dhahiri wala hakuna kitu juu yake, na wa batini wala hakuna kitu chini yake, ni muweza wa kila kitu, na nguvu zote ni zake, hashindwi na chochote ardhini wala mbinguni, amri yake ni kama kupepesa kwa jicho, bali amri yake ni karibu zaidi, na anao majeshi asio yajua yeyote ila Yeye, na amri ya dunia itakapoisha ataitingisa tingisa ardhi na ataivunja vunja, na atayaendesha majabali kwa mwendo mkubwa, na atayavuruga vuruga, na kwa mpulizo

mmoja [katika parapanda] watu watababaika, na kwa [mpulizo] mwengine watakufa, na kwa [mpulizo] watatu watasimama kuenda sehemu ya kukusanywa.

'Subbuuhun Qudduusun' aliye takasika kutokana na kila aibu na upungufu, anao katika ukamilifu wa juu kabisa, na anao katika utimamu na uzuri zaidi, hana mshirika naye wala mfano, wala hakuna mwenye jina kama lake, wala anaye fanana naye:

﴿لَيْسَ كَمِثْلِهِۦ شَىْءٌ ۖ وَهُوَ ٱلسَّمِيعُ ٱلْبَصِيرُ﴾

{Hapana kitu kama mfano wake. Naye ni Mwenye kusikia Mwenye kuona}.[Ash-shuuraa: 11].

**Na baada ya haya, enyi Waisilamu:**

Basi hivi haiwi wajibu kwetu kumpenda Mola wetu Mlezi, ambaye hizi ndizo Sifa zake na matendo yake, na tumuhimidi na tumsifu, na tumtakasie Yeye ibada?

Na atakaye mtambua Allah basi atamkurubia, atamnyenyekea, atadhalilika mbele yake, na atapumbaa Naye, atapata utulivu, atatarajia thawabu zake, na ataogopa adhabu yake, atateremsha mahitaji yake kwake na atamtegemea Yeye.

Na atakaye msifu Allah na akakithirisha basi atanyanyuka, kwani hakuna yeyote ambaye sifa zinapendeza zaidi kwake kuliko Allah, na kwa ajili ya hilo ndio amejisifu Nafsi yake, na atakaye mpenda Allah na akamuabudu Allah naye atampenda, atamridhia na atamuingiza Peponi.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿إِنَّ ٱللَّهَ رَبِّى وَرَبُّكُمْ فَٱعْبُدُوهُ ۚ هَٰذَا صِرَٰطٌ مُّسْتَقِيمٌ﴾

{Hakika Allah ni Mola wangu Mlezi na ni Mola wenu Mlezi. Basi muabuduni Yeye. Hii ndiyo Njia Iliyo Nyooka}. [Maryam: 36].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi Waisilamu:**

Atakaye mshirikisha Allah na wengine katika viumbe; basi hakika amemtia kasoro Mola Mlezi wa viumbe vyote, na amechukulia dhana mbaya, na amemsawazisha mwengine Naye

Na shirki inaporomosha amali zote, wala Allah hamsamehe mwenye kuifanya, wala hamuingizi Peponi, naye atakuwa katika wenye kukaa milele Motoni, na shirki ndio mabadiliko makubwa yaliokumba umbile [fitra], na ndio ufisadi mkubwa ardhini, na ndio asili ya kila balaa, na mkusanyiko wa kila magonjwa, madhara yake ni makubwa, na hatari yake ni mbaya.

Na uovu wa maasi ni mkubwa, yanakusanyika kwa mja hadi yakamuangamiza, na yanamzuia mja na moyo wake, na kwa kadri dhambi litakavo kuwa dogo katika jicho [la mja] ndivo litakavo kuwa kubwa mbele ya Allah; basi usiangalie udogo wa maasi, lakini angalia ukubwa wa unaye muasi.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# MJA KUMTAMBUA MOLA MLEZI[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha; kwani neema zinakuwa katika kufuata uongofu, na uovu unakuwa katika kufuata matamanio [ya nafsi].

**Enyi Waislamu:**

Allah ameumba viumbe ili utiifu uwe ni wake na kujidhalilisha ni kwake, na ukamilifu wa saada ni katika kumtambua Allah na kumuamini, mja kumjua Mola wake Mlezi ndio msingi wa kwanza ambao ni wajibu juu ya binadamu kuujua, nao ndio jambo la kwanza atakaloulizwa mja ndani ya kaburi lake. Allah amewaleta viumbe baada ya kutokuweko, na akawapa neema kwa wingi, na akawadhaminia riziki:

﴿وَمَا مِن دَآبَّةٖ فِي ٱلۡأَرۡضِ إِلَّا عَلَى ٱللَّهِ رِزۡقُهَا﴾

{Na hakuna mnyama yoyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Allah} [Huud: 6].

Amewaleta walimwengu baada ya kuwa hakuwa ni kitu:

﴿هَلۡ أَتَىٰ عَلَى ٱلۡإِنسَٰنِ حِينٞ مِّنَ ٱلدَّهۡرِ لَمۡ يَكُن شَيۡـٔٗا مَّذۡكُورًا﴾

{Hakika kilimpitia binaadamu kipindi katika zama ambacho

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe kumi na tano, mwezi wa Safar, mwaka elfu moja mia nne na ishirini na sita hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

kwamba hakuwa kitu kinacho tajwa} [Al-Insaan: 1].

Ni Mola Mlezi aliyepwekeka na jambo la kuumba, kuruzuku, na kuendesha:

﴿أَلَا لَهُ ٱلۡخَلۡقُ وَٱلۡأَمۡرُۗ تَبَارَكَ ٱللَّهُ رَبُّ ٱلۡعَٰلَمِينَ﴾

{Fahamuni! Kuumba na amri ni zake. Ametukuka kabisa Allah, Mola Mlezi wa viumbe vyote}. [Al-a`raaf: 54].

Amepwekeka na Tawhidi, amesifika na utukufu na kahari, hatamu za mambo yote ziko Mikononi mwake, ni mwenye nguvu sana, mwenye kukahiri aliye juu ya waja wake, haridhii kuabudiwa mwengine ila Yeye:

﴿إِن تَكۡفُرُواْ فَإِنَّ ٱللَّهَ غَنِيٌّ عَنكُمۡۖ وَلَا يَرۡضَىٰ لِعِبَادِهِ ٱلۡكُفۡرَۖ وَإِن تَشۡكُرُواْ يَرۡضَهُ لَكُمۡ﴾

{Mkikufuru basi Allah si mwenye haja nanyi, wala haridhii kufuru kwa waja wake. Na mkishukuru, basi Yeye huridhia hilo kwenu}. [Az-Zumar: 7].

Amesimamisha katika kila kiumbe alama ya kujulisha kupwekeka kwake; ili kushikamana kwa moyo na Mola wake mlezi kuzidi. Alama mbili zinaandamana juu yetu, zinatukumbusha kupwekeka kwa Allah, nao ni usiku unao funika na mchana unadhiri, kila mmoja wao anamfukuza mwenzake kwa kasi:

﴿يُغۡشِي ٱلَّيۡلَ ٱلنَّهَارَ يَطۡلُبُهُۥ حَثِيثٗا﴾

{Huufunika usiku kwa mchana, ufuatao upesi upesi}. [Al-a`raaf: 54],

Jua na mwezi zinatembea katika njia ilio pangika, yenye kushangaza wenye busara, hili linachomoza na ule unaondoka, mwendo uliopangika, hautangulii mbele wala hauchelewi:

﴿لَا ٱلشَّمۡسُ يَنۢبَغِي لَهَآ أَن تُدۡرِكَ ٱلۡقَمَرَ وَلَا ٱلَّيۡلُ سَابِقُ ٱلنَّهَارِۚ وَكُلّٞ فِي فَلَكٖ يَسۡبَحُونَ﴾

{Haliwi jua kuufikia mwezi, wala usiku kuupita mchana. Na vyote vinaogelea katika njia zao}. [Yaasin: 40].

Ardhi inatubeba, na mbingu zinazotufunika, wala hatuachi kuvihitajia. Uumbaji wa kina, na uendeshaji wa Muumbaji mzuri:

﴿هَٰذَا خَلۡقُ ٱللَّهِ فَأَرُونِي مَاذَا خَلَقَ ٱلَّذِينَ مِن دُونِهِۦ﴾

{Huu ni uumbaji wa Allah. Basi nionyesheni wameumba nini hao wasio kuwa Yeye!} [Luqman: 11],

Na Muisilamu anajivunia kuwa mja wa [Allah] mwenye kuendesha huu ulimwengu mkubwa:

﴿قُلۡ إِنَّنِي هَدَىٰنِي رَبِّيٓ إِلَىٰ صِرَٰطٖ مُّسۡتَقِيمٖ﴾

{Sema: Kwa hakika mimi Mola wangu Mlezi ameniongoa kwenye Njia Iliyo Nyooka} [Al-an`aam: 161],

hamuabudu ila Mola Mlezi wa huu ulimwengu aliyetukuka na aliye juu, wala hapeleki chochote katika aina za ibada kwa asiye kuwa Yeye, anakimbilia kwake katika mambo mazito, na anamuogopa Yeye peke yake hadharani na mafichoni:

﴿وَإِن يَمۡسَسۡكَ ٱللَّهُ بِضُرّٖ فَلَا كَاشِفَ لَهُۥٓ إِلَّا هُوَ﴾

{Na ikiwa Mwenyezi Mungu akikugusisha madhara, basi hapana wa kukuondolea hayo ila Yeye} [Al-an`aam: 17],

hamuogopi maiti asije kumdhuru na uovu, au akatarajia ihsani kutoka kwake.

Na kukimbilia kwake peke yake ni [dalili ya] wingi wa akili, na ni amani ya moyo, na utulivu wa roho, na aliyemuogopa Mola wake Mlezi basi hataogopeshwa na yeyote; bali ni mwenye imara ya moyo na utulivu wa viungo, na ni neema ya ajabu ya nafsi isiyopata pumbao ila pamoja na Allah:

﴿فَلَا تَخَافُوهُمۡ وَخَافُونِ إِن كُنتُم مُّؤۡمِنِينَ﴾

{basi msiwaogope, bali niogopeni Mimi mkiwa nyinyi ni Waumini} [Aalu-Imran: 175]

Abu Suleiman Ad-Daaraani Allah amrehemu anasema: "Hofu [ya Allah] haijaepuka moyo wowote ila unaharibika".

Mja aliye karibu zaidi na Allah ni yule anaye muogopa zaidi, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema:

**«Hakika mimi ndio mjuzi wao zaidi wa kumjua Allah, na mchamngu wao zaidi»**, wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, nayo ni miongoni mwa yanayo lazimu Imani na

yanayo wajibishwa nayo, na atakayemuogopa Mola wake Mlezi peke yake atafunguliwa milango ya Pepo; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَلِمَنۡ خَافَ مَقَامَ رَبِّهِۦ جَنَّتَانِ﴾

{Na mwenye kuogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake Mlezi [akawa ni mwenye kufanya mema na kuepuka maovu] atapata Pepo mbili} [Ar-Rahman: 46]

wenye elimu [ya sheria] walisema: "Allah hamkusanyii mja wake hofu mbili; basi atakayemuogopa duniani atampa amani siku ya Kiyama, na atakaye jichukulia amani duniani, na asimuogope Mola wake Mlezi, basi atamuogopesha akhera"; basi mchunge Mola wako [katika maamrisho yake na makatazo yake] na muogope aliyekuumba, utakuwa mja mwenya saada zaidi mbele ya Allah.

Wala usitaraji kutimia matakwa au kusalimika na yanayohofiwa kutoka kwa asiyekuwa Allah, - miongoni mwa: kuondokewa ugonjwa na kasoro, au kupoa kwa ugonjwa, au kutaka riziki, au kuleta afya -, na yatekeleze [yafunge] matarajio yako kwa Allah pasina wengine; kwani viumbe wamepewa umbile la udhaifu, hawana uwezo wa kuziletea nafsi zao manufaa, na kuzikinga na madhara, nao sio waweza wa kuwafanyia hayo wengine, wala hajawahi yeyote kumtarajia kiumbe ila dhana yake kwake huenda patupu, basi usifunge tamaa yako na matarajio yako na asiyekuwa Allah, kwani hautavuna ila majuto na udhalilifu wa kuomba, na tarajia ukarimu wa Allah, vipawa vyake, na neema zake nyingi, kwani kutarajia yalio kwa Allah ni ibada, na mnao katika kudhalilika moyo kwa Allah nguvu na ushindi wa nafsi, kunyanyuka daraja, na kupata matarajio.

Na raha [mapumziko] ya nafsi yamo ndani ya kutegemeza amri yake kwa Muumba wake, na mashikamano yake na Mola wake yanazidi inapokumbuka ya kuwa Mola wake ni Mjuzi wa hali yake, ni mwenye rehema na jambo lake, ni muweza wa

kumuondolea madhara yake, na kwani nini kushikamana [moyo] na kiumbe asiye weza kuondoa madhara, mgumu katika kutoa?! Na hali Mola wako anakutosheleza mambo yako yote; naye ni mwenye kuyasimamia endapo utampelekea haja zako, na ukamkabi hatamubza mambo yako

﴿وَمَن يَتَوَكَّلۡ عَلَى ٱللَّهِ فَهُوَ حَسۡبُهُۥٓ﴾

{Na anaye mtegemea Allah Yeye humtosha}[At-Twalaaq: 3].

Na mwenye saada ni yule mwenye shauku na rehema za Allah, na mwenye kuogopa adhabu yake, aliye dhalili katika kumuabudu Mola wake, na hizo ni sifa za hali ya juu zilizosifika nazo nyumba za Manabi; [Allah] aliyetakasika alisema kuhusu Zakariya salamu zimshukie na jamaa zake:

﴿إِنَّهُمۡ كَانُواْ يُسَٰرِعُونَ فِي ٱلۡخَيۡرَٰتِ وَيَدۡعُونَنَا رَغَبٗا وَرَهَبٗاۖ وَكَانُواْ لَنَا خَٰشِعِينَ﴾

{Hakika wao walikuwa wepesi wa kutenda mema, na wakituomba kwa shauku na khofu. Nao walikuwa wakitunyenyekea}[Al-Anbiyaa: 90],

na Mitume ni wenye kutangulia mno katika kuwa na shauku ya yaliyo kwa Allah; [Allah] aliyetakasika alisema kumwambia Nabii wake Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie:

﴿وَإِلَىٰ رَبِّكَ فَٱرۡغَب﴾

{Na Mola wako Mlezi ndio mshughulikie}[Ash-sharh: 8],

nayo shauku ya yaliyo kwa Allah inapungua kwa mja kwa kadri ya madhambi, na inazidi kwa kuzidi imani, ibnu Qayyim Allah amrehemu amesema: "Allah anapomtakia mja heri, humuafikia katika kutumia uwezo na kufanya bidii katika kumshughulikia Yeye na kumuogopa Yeye; kwani hayo mawili ndio vyanzo viwili vya kuafikiwa, kwa kadri itakavyo simama shauku na hofu ndani ya moyo ndio itapatikana taufiki".

Na kuogopa kiumbe ni udhalilifu na utwevu, na atakaye muogopa Muumba wake ataishi akiwa azizi, na atakuwa ni mwenye saada katika maisha yake, na hilo litang'arisha fahamu yake awe mwenye kukumbuka [kumkumbuka Allah], [Allah]

aliyetakasika amesema:

﴿سَيَذَّكَّرُ مَن يَخۡشَىٰ﴾

{atakumbuka mwenye kuogopa}[Al-a`laa: 10],

Na atafaidika na mawaidha na mazingatio; [Allah] Mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَعِبۡرَةً لِّمَن يَخۡشَىٰٓ﴾

{kwa hakika katika hayo kuna mazingatio kwa wanaoogopa}[An-nazi`aat: 26],

Na Kitabu cha Allah kitakuwa kwake ni Saada na ukumbusho:

﴿مَآ أَنزَلۡنَا عَلَيۡكَ ٱلۡقُرۡءَانَ لِتَشۡقَىٰٓ * إِلَّا تَذۡكِرَةً لِّمَن يَخۡشَىٰ﴾

{hatukukuteremshia Qur-ani ili upate mashaka * bali ni mawaidha kwa wenye kuogopa}[Twahaa: 2-3],

Nalo [jambo la kumuogopa Allah] ni lenye kuwajibisha msamaha wa Allah na vipawa vyake vingi:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ يَخۡشَوۡنَ رَبَّهُم بِٱلۡغَيۡبِ لَهُم مَّغۡفِرَةٞ وَأَجۡرٞ كَبِيرٞ﴾

{hakika wanaomuogopa Mola wao Mlezi kwa ghaibu watapata msamaha na ujira mkubwa} [Al-mulk: 12],

Basi mjaaliye Mola wako Mlezi mbele ya macho yako, wala usijiaminie makri yake [mipango yake] na kushuka kwa adhabu yake, wala usimuogope asiyekuwa Allah katika kukatika kwa riziki, au kuchelewa kwa ponyo, au kushuka kwa mashaka, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿فَلَا تَخۡشَوۡهُمۡ وَٱخۡشَوۡنِي وَلِأُتِمَّ نِعۡمَتِي عَلَيۡكُمۡ وَلَعَلَّكُمۡ تَهۡتَدُونَ﴾

{basi msiwaogope wao, lakini niogopeni mimi – na ili nikutimizieni neema yangu, na ili mpate kuongoka} [Al-Baqarah: 150].

Mja ni dhaifu akitegemea nafsi yake, anahitajia msaada wa Mola wake Mlezi mwenye nguvu, na kwa kutaka msaada kwake aliye mtukufu na aliye juu kunatosheleza kutokana na kutaka msaada kwa viumbe, na atakayefanya bidii kutekeleza analolitaka, kisha asiwe ni mwenye kutaka msaada kwa Allah na

asiwe mwenye kumuhitajia Yeye katika kulipata analolihitaji; basi milango itafungwa mbele ya uso wake, na mapato yatakuwa na uzito mbele yake, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema kumwambia ibnu Abbaas Allah amridhie yeye na babake:

**«Ewe kijana! Mimi nakufundisha maneno, mhifadhi Allah Naye atakuhifadhi, mhifadhi Allah utamkuta mbele yako, unapoomba basi muombe Allah, na unapotaka msaada basi taka kutoka kwa Allah»**, imepokewa na Tirmidhi.

Na mzungukio wa Dini uko juu ya kutaka msaada kwa Allah:

﴿إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ﴾

{Wewe tu tunakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada} [Al-fatiha: 5],

Na Mitume waliwaamrisha kaumu zao nalo:

﴿قَالَ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِ ٱسْتَعِينُوا۟ بِٱللَّهِ وَٱصْبِرُوٓا۟﴾

{Musa akawaambia watu wake: Ombeni msaada kwa Allah, na subirini} [Al-a`raaf: 128],

Sheikhul Islaam Allah amrehemu amesema: "Dini ni asiabudiwe ila Allah, na kusitakwe msaada ila kwake".

Na ukamilifu wa ukwasi wa mja ni katika kufungamana kwake na Mola wake Mlezi, na ni katika fadhila za Allah juu ya waja wake kuwa humsaidia anayefungamana Naye, na riziki huwa nyepesi kwa utiifu na kutaka msaada kwa Allah, na huzidi kwa kumtegemea Allah na kunyenyekea kwake, [Allah] aliye takasika amesema:

﴿وَمَن يَتَّقِ ٱللَّهَ يَجْعَل لَّهُۥ مَخْرَجًا * وَيَرْزُقْهُ مِنْ حَيْثُ لَا يَحْتَسِبُ﴾

{Na anaye mcha Allah humtengezea njia ya kutokea * Na humruzuku kwa jiha asiyo tazamia}. [At-Twalaaq: 2-3],

Maisha yamejaa maafa na machukivu; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿لَقَد خَلَقنَا الإِنسَـٰنَ فِي كَبَدٍ﴾

{Hakika tumemuumba mtu katika taabu}, [Al-balad: 4],

ni kila kiumbe kina maadui katika majini na binadamu, na kiongozi wao akiwa ni ibilisi - laana za Allah zimshukie -; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿إِنَّ ٱلشَّيۡطَٰنَ لَكُمۡ عَدُوّٞ فَٱتَّخِذُوهُ عَدُوًّا﴾

{Hakika Shet'ani ni adui yenu, basi mfanyeni kuwa ni adui} [Faatwir: 6],

basi mja haachi kuwa muhitaji wa kutaka kinga kwa Allah, na kutaka kulindwa Naye, na kushikamana na himaya yake kutokana na shari.

Na Mola Mlezi amesifika na Ujabari na Ushindi; na atakaye shikamana Naye basi hakuna mtu atamsibu na madhara, na madhara hayatamfika hata lau sababu zake zikiwepo; [Mtume] swala na salamu zimshukie amesema:

«**atakaye shukia sehemu akasema: *'audhu bi kalimaati llaahi ttaammaati min sharri maa khalaq'*; hatadhuriwa na kitu hadi aondoke sehemu yake ile**», imepokewa na Muslim, al-Qurtubi amesema: "Tokea niisikie Habari [hadithi] hii nimekuwa nikiifanyia kazi; basi sikudhuriwa na kitu hadi nilipoiacha, basi nikaumwa na nge siku moja nilipokuwa mji wa Al-Mahdiyyah, nakafikiria katika nafsi yake, nikajipata kumbe nilisahau kujilinda na maneno hayo [aliyoyafundisha Mtume katika hadithi iliyotangulia]".

Na kiumbe huwa ni mwenye kupata maudhi, wala maisha yake hayawi mazuri ila kwa kushikamana na Allah na kujikinga Naye, kwani madhara na manufaa yote yamo Mkononi mwake, na atakayefanya bidii kukudhuru basi halitatimia lengo lake iwapo Allah hajalitaka hilo; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**na jua ya kwamba lau umma mzima utakusanyika ili wakudhuru na kitu, hawatakudhuru na chochote ila kile alichokuandikia Allah**», imepokewa na Tirmidhi, na Allah alimuamrisha Nabii wake swala na salamu za Allah zimshukie ajilinde na Muumba wa asubuhi kutokana na shari za viumbe

vyote, na shari ya giza la usiku, na ya hasidi, na aliye mueza wa kuliondoa hili giza katika ulimwengu; ni mueza wa kumuondolea aliyejilinda Naye anayo yaogopa, na mwenye kushikamana na Allah, mwenye kujilinda Naye katika kila hali, huyo yumo ndani ya ngome imara [ya kumkinga] kutokana na wenye shari na vitimbi.

Mola wetu Mlezi hatuna pa kukimbilia katika mazito ila kwake, wala hatuna pa kuelekea ili kujikinga Naye ila kwake Yeye, na anayetaka uokozi kwa Allah na hifadhi yake huwa ametekeleza aina ya juu ya maombi, na kutaka uokozi kwa Mola Mlezi ndio jambo wanalolikimbilia Manabii na watu wema katika hali nzito na vitimbi, [Allah] aliye takasika amesema:

﴿إِذْ تَسْتَغِيثُونَ رَبَّكُمْ فَٱسْتَجَابَ لَكُمْ أَنِّى مُمِدُّكُم بِأَلْفٍ مِّنَ ٱلْمَلَٰٓئِكَةِ مُرْدِفِينَ﴾

{Mlipo kuwa mkimuomba msaada Mola wenu Mlezi, naye akakujibuni kuwa: Kwa yakini Mimi nitakusaidieni kwa Malaika elfu wanao fuatana mfululizo} [Al-Anfaal: 9].

na [Allah] aliyetakasika amesema tena:

﴿أَمَّن يُجِيبُ ٱلْمُضْطَرَّ إِذَا دَعَاهُ﴾

{Au nani yule anaye mjibu mwenye shida pale anapomuomba} [An-Naml: 62]

Atakayeomba maiti basi maombi hasikiwi, na mahitaji yake hayatanyanyuliwa; [Allah] aliyetakasika amesema tena:

﴿وَٱلَّذِينَ تَدْعُونَ مِن دُونِهِۦ مَا يَمْلِكُونَ مِن قِطْمِيرٍ *

إِن تَدْعُوهُمْ لَا يَسْمَعُوا۟ دُعَآءَكُمْ وَلَوْ سَمِعُوا۟ مَا ٱسْتَجَابُوا۟ لَكُمْ﴾

{Na hao mnao waomba badala yake hawamiliki hata ugozi wa kokwa ya tende * Mkiwaomba hawasikii maombi yenu; na hata wakisikia hawakujibuni}, [Faatwir: 13-14],

basi yanapokushukia mazito, na yakakulemea majanga, basi taka uokozi kwa Mjuzi wa ghaibu [Allah]:

﴿إِنَّمَآ أَمْرُهُۥٓ إِذَآ أَرَادَ شَيْـًٔا أَن يَقُولَ لَهُۥ كُن فَيَكُونُ﴾

{Hakika amri yake anapotaka kitu ni kukiambia tu: Kuwa! Na

kikawa} [Yaasin: 82].

Na kumpwekesha Allah kwa matendo ya waja ni usafi katika itikadi, na ni saada yenye kuenea jamii, na ni utulivu ndani ya nafsi.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿يَـٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ ٱعْبُدُوا۟ رَبَّكُمُ ٱلَّذِى خَلَقَكُمْ وَٱلَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ * ٱلَّذِى جَعَلَ لَكُمُ ٱلْأَرْضَ فِرَٰشًا وَٱلسَّمَآءَ بِنَآءً وَأَنزَلَ مِنَ ٱلسَّمَآءِ مَآءً فَأَخْرَجَ بِهِۦ مِنَ ٱلثَّمَرَٰتِ رِزْقًا لَّكُمْ ۖ فَلَا تَجْعَلُوا۟ لِلَّهِ أَندَادًا وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ﴾

{Enyi watu! Muabuduni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni nyinyi na wale wa kabla yenu, ili mpate kuokoka * (Mola) ambaye amekufanyieni hii ardhi kuwa kama tandiko, na mbingu kama paa, na akateremsha maji kutoka mbinguni, na kwayo akatoa matunda yawe riziki zenu. Basi msimfanyizie Allah washirika, na hali nyinyi mnajua}. [Al-Baqarah: 21-22].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii, enyi Waisilamu:**

Milango ya saada na heri inafunguliwa kwa kufungamana kwa moyo na Allah, na milango ya shari inafungwa kwa toba na istighfari, na afueni ya moyo iko katika kuacha maovu, na neema ya dunia imo katika kuvutika moyo kwa Allah kwa kumpenda, kumuogopa, na kutarajia fadhila zake, kwani hofu inakuepusha na kumuasi Allah, na matarajio yanakusukuma katika kumtii, na kumpenda kunakuvuta kwake, basi zifanye amali zako zote ni zenye kutakasiwa Allah, zenye kusimama kwa njia iliyo kamili zaidi kidhahiri na batini, pamoja na kuwa na yakini kuwa Allah anaona ya siri na niya, ni mwenye kuona na ni Mjuzi wa yaliyofichana.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# ITIKADI YA MUISILAMU[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakaye mpoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake

**Ama baada ya himdi hii:**

Mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha; kwani mwenye kumcha Mola wake Mlezi ataokoka, na mwenye kumsadikisha hapatwi na udhia, na mwenye kumtarajia basi [Yeye] atakuwa na mtarajiwa mwema kwake.

**Enyi Waislamu:**

Hakika Dini ya Uisilamu iko katika upeo wa ukamilifu, ni Dini iliyo kusanya maslahi yote ya binadamu, mnao ndani yake [aina za] ibada, miamala, hududi [adhabu maalumu za baadhi ya makosa], na taaziir [aina za adhabu anazozikisi kiongozi]; ambazo zinamtakasa mtu na jamii, na zinahifadhi jamii kutokana na vurugu na migongano, na zinaikomesha nafsi ya kibinadamu na zinaitia hatamu hamu yake ya kufanya munkari na kuchuma maovu, zinamtoa binadamu kutoka katika mambo ya uduni na tabia mbaya. Hakuna saada atakayopata mtu yeyote maishani ila kwa kushikamana kwake na Dini yake [Uisilamu], na jema linakuwa kubwa na thawabu zake zinakithiri kwa kuzidi kwa imani na ikhlasi, na thawabu za amali huporomoshwa na kushirikisha.

Hakika walikuwemo kati ya makureshi watu waliokuwa

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe ya kumi na nne, mwezi wa Dhul-hijjah, mwaka elfu moja mia nne na ishirini na moja hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

wakifanya ibada, wakihiji, wakifanya umra, wakitoa sadaka, wakiunga kizazi, wakiwakirimu wageni, na wakikiri ya kwamba Allah ndiye aliyepwekeka katika uumbaji na uendeshaji, na wanamtakasia Allah ibada nyakati za shida, lakini wao walikuwa wakichukua wa kati baina yao na baina ya Allah, wanawaomba, wanawachinjia, wanawatilia nadhiri, na wanawaomba uokozi ili wawafanyie uombezi [kwa Allah], wakidai kuwa wao ni wakaribu zaidi na Allah kwa yenye kufikisha kwake, basi Allah akamtuma Muhammad [swala na salamu za Allah zimshukie] awajadidishie Dini ya baba yao Ibrahim salamu zimshukie, na awajulishe kuwa ibada ni haki ya Allah pekee, na kuwa tendo lao hili [la kujiwekea ukati baina yao na Allah] limewaharibia ibada walizonazo, kisha akawapiga vita ili yawe maombi, kuchinja, nadhiri, kuomba uokozi, na aina zote ibada zote ni za Allah peke yake.

Kutaka ponyo ya wagonjwa, msamaha wa madhambi, na mengineo ni katika mambo asio yaweza ila Allah, kwa hivyo hayaombwi ila kutoka kwake aliyetakasika, na makaburi hayakusudiwi kwa ajili ya kufanya maombi na swala sehemu yake, hakika si mengine makaburi ni makaazi ya wafu, ima ni neema kwao, ima ni Jahimu.

Ni katika uasi mkubwa sana kutaka uokozi kwao [wafu] na kutaka uokozi kwa kiumbe katika mambo asio yaweza; kama vile anayezama majini kutaka uokozi kwa anayezama, na hajawahi yeyote kumtarajia kiumbe kutarajia kamili ila dhana yake kwake huambulia patupu; basi elekea kwa Allah, kwani Allah huruzuku kupitia sababu na bila sababu, na kupitia njia usizotarajia, na Allah anatosha kuwa ni mlinzi na mwenye kunusuru.

Na kafara ya shirki ni: Tawhidi, na mema yanafuta maovu, na atakayemtarajia asiyekuwa Mola wake Mlezi kumkidhia mahitaji yake, na akauepusha moyo wake na kushikamana na Muumba wake; ataishi mawazoni na atakuwa ametaka muhali.

Na kutaka kinga ya maudhi kutoka kwa asiyekuwa Allah kwa kupitia mazunguo na hirizi ni kushikamana na asiyekuwa Allah,

[Mtume] swala na salamu zimshukie anasema:

«**Hakika mazunguo, hirizi na 'tiwalah' ni ushirikina**», imepokewa na Ahmad, na hirizi ni kitu kisicho na roho, haiwezi kurudisha chochote katika amri ya Allah, haikingi kutokana na maafa, wala machukivu, wala haitekelezi matakwa, na atakayeifunga katika shingo za watoto au wanawake au wengineo basi Allah atamtegemeza kwayo na hatamnusuru; basi shikamana na Allah, mteremshie Yeye mahitaji yako, elekea kwake na muachie Yeye jambo lako, nayo haja yako itatoshelezwa na kifua chako kitakunjuka:

﴿وَمَن يَتَوَكَّلۡ عَلَى ٱللَّهِ فَهُوَ حَسۡبُهُۥٓ﴾

{Na anaye mtegemea Allah Yeye humtosha} [At-Twalaaq: 3] na pindi Allah atamtosheleza mja wake aliyemtegemea Yeye humlinda, basi adui hana tamaa ya kumdhuru, wala usijaalie kumtegemea kwako Allah ni ajizi, wala ajizi yako kuwa ni kumtegemea [yaani: usizembee, ukaacha kutekeleza sababu kwa madai ya kumtegemea Allah].

Na kuwaendea wachawi na wapiga ramli, kusadikisha mazingaombwe yao, kuwauliza mambo ya ghaibu na ya mbeleni, kutaka kutoka kwao jambo la kumchukiza mke kwa mumewe au kumpendezesha, au kuridhi hayo, [yote hayo] ni dosari katika itikadi na ni upungufu katika kumtegemea Allah, ni kutosubiri ulioandikiwa na ni kukasirikia uliokadiriwa, [Mtume] swala na salamu zimshukie anasema:

«**Atakayemjia kuhani au mcheza ramli, na akamsadikisha kwa anayoyasema; basi hakika [kwa hilo] ameyakufuru aliyo teremshiwa Muhammad**», imepokewa na Ahmad.

Riziki ya Allah haivutwi na bidii ya mwenye bidii, wala hairudishwi na chuki ya mwenye chuki; Al-Hasan Al-Basri Allah amrehemu amesema: "Nilipojua kuwa riziki yangu haiwezi kuchukuliwa na mwengine moyo wangu ulipata utulivu", na kuwaendea wachawi hakuharakishi riziki, wala hakucheleweshi ajali, Al-Qurtubi amesema: "Ni wajibu kwa wenye uwezo wa

hilo miongoni mwa wenye wadhifa wa kuamrisha na kukanya na wengineo awakanye vikali wao - yaani wachawi - na wenye kuwaendea".

Hifadhi kiapo chako - usiape kirahisi rahisi - hata lau ukiwa mkweli, ili kuadhimisha heshima ya Mola wako Mlezi, wala usiape ila kwa Jina miongoni mwa Majina ya Allah na Sifa miongoni mwa Sifa zake, wala usiape kwa asiyekuwa Yeye aliyetakasika; kama vile Kaaba, Nabii, amana na walii - [mtu mwema] -.

Kuwa na yakini na kadari ya Allah, uumbaji wake na uendeshaji wake, na subiria mtihani wake na hukumu yake, na jisalimishe kwa amri yake, kwani dunia imejaa maovu na machafu, ina umbile la mazito na majanga; basi kuwa mwenye kuamini kadari, kwani kuiamini ni nguzo kati ya nguzo za Dini, na si kila yanayotamaniwa hupatikana, na kwa kukariri katika maombi na kuelekea kwa Allah kiukamilifu milango hufunguliwa na matakwa hupatikana.

Ni juu ya muumini iwe hofu yake na matarajio yake ni mamoja; yoyote kati ya mawili haya yakighilibu basi ataangamia, basi yule ambaye hofu yake itaghilibu ataingia katika aina ya ukataji tamaa, na yule ambaye matarajio yake yataghilibu ataingia katika aina ya kujiaminisha na adhabu yake na kudura yake, na hofu mzuri ni yenye kukuzuia na yale Allah aliyoharamisha.

Na endapo hutahisi ladha moyoni mwako ya amali uliyoitenda basi utuhumu moyo wako, kwani Mola mlezi ni mwingi wa shukrani, na duniani ipo Pepo, ambaye hataiingia basi hataingia Pepo ya akhera, na aliye nyimwa hakika ni yule ambaye moyo wake utazuiliwa na Mola wake Mlezi, na aliyeshikwa mateka hakika ni yule aliyeshikwa mateka na matamanio yake, na kusimamisha Swala pamoja na jamaa ya Waisilamu ndani ya nyumba za Allah inazidisha imani, inang'arisha uso, na inakinga kutokana na ya haramu; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَأَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَۖ إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ تَنۡهَىٰ عَنِ ٱلۡفَحۡشَآءِ وَٱلۡمُنكَرِ﴾

{Na simamisha Swala. Hakika Swala inazuilia mambo machafu na maovu} [Al-Ankabuut: 45].

Kula na kunywa ya halali ni dalili ya usalama wa Imani na uzuri wa mwenendo, na sababu ya kuitikiwa maombi; [Mtume] swala na salamu zimshukie anasema:

«**Ewe Sa'ad! Kufanye kuzuri kula kwako utakuwa mwenye kuitikiwa maombi**», na nafsi yako inanyanyuka na roho yako itatwahirika kwa kuepuka kutumia ribaa, au kuamiliana kwa ya haramu.

Jaalia muamala wako na wengine juu ya kidhibiti cha kupenda na kuchukia kwa ajili ya Allah, kwani anayetafuta radhi za Allah kwa hasira za watu Allah atamtosheleza uzito wa watu.

Tahadhari dhuluma; kwani dhuluma ni giza maradufu siku ya Kiyama, na aliyedhulumiwa ni mwenye kuitikiwa maombi, mwenye kutekelezewa matakwa, basi usiwanyime wenzako haki zao, wala usizifanyie [haki zao] uadui, na dhuluma haiachani na kuacha jema au kutenda ovu, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَمَن يَظۡلِم مِّنكُمۡ نُذِقۡهُ عَذَابٗا كَبِيرٗا﴾

{Na atakaye dhulumu miongoni mwenu tutamwonjesha adhabu kubwa} [Al-Furqaan: 19].

Hakika mwenye akili ni yule aliyejishughulisha na aibu za nafsi yake na kuacha za wengine, na akasimama na kumtii Mola wake Mlezi kwa jitihada, na mwenye kufuata njia kuelekea kwa Allah hana budi kuwa na hamu yenye kumuendesha na kumnyanyua, na elimu yenye kumtambulisha na kumuongoza, basi tembea kuenda kwa Allah ukiwa baina ya [hali mbili: hali ya] kuona neema [zake juu yako, na hali ya] kuona aibu za nafsi yako, na tahadhari kukejeli heshima za Waislamu kwa kuwasengenya na kuwazulia; [Mtume] swala na salamu zimshukie anasema:

«**Hakika damu zenu, mali yenu na heshima zenu ni haramu baina yenu [kuzifanyia uadui], kama uharamu wa**

**siku yenu hii [siku ya Arafa], katika mwezi huu, katika mji wenu huu [Makkah]**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Wala uhasidi na hawaa zisikubebe kuzusha urongo, kwani husuda ndio tabia ya ufisidifu zaidi, na binadamu ana maumbile ya kupenda kuwakalia wenzake juu, na lawama inamuelekea yule anayetenda kwa mujibu wa kughadhabika na kadari, au akasimama kumkejeli anayemuhusudu, basi ichukie tabia hiyo mbaya juu ya nafsi yako, na tumia uchamngu kuitibu, kwani anayemcha Allah na akasubiri Allah humnufaisha na uchamngu wake, hupambika na tabia za hali ya juu, na dumu juu ya ibada; kwani wingi wa ibada huepusha na riya [kujionyesha], na kutaka msaada kwa Allah kunazuia na kiburi, na balaa hukingwa na kuamrisha mema na kukataza maovu, na epuka maasi madogo na makubwa; kwani yanadhoofisha moyo na kiwiliwili, na huondosha neema na huleta adhabu, na shetani humpambia binadamu maasi, humsahaulisha adhabu, na hamuashiria ukunjufu wa rehema [ya Allah]; ili apate kumuingiza katika dhambi mara kwa mara, na audhuufishe mwendo wake wa kuelekea kwa Allah na nyumba ya akhera, na [shetani] amemtegeshea binadamu kamba [za mitego] na humtakia misiba, basi usifuate hatua zake, wala usiache kumpiga vita, na kithirisha kutenda amali za utiifu, kwani miongoni mwa alama za kukubaliwa jema ni kutenda jema baada yake.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿وَأَنَّ هَٰذَا صِرَٰطِي مُسۡتَقِيمٗا فَٱتَّبِعُوهُۖ وَلَا تَتَّبِعُواْ ٱلسُّبُلَ فَتَفَرَّقَ بِكُمۡ عَن سَبِيلِهِۦۚ ذَٰلِكُمۡ وَصَّىٰكُم بِهِۦ لَعَلَّكُمۡ تَتَّقُونَ﴾

{Na kwa hakika hii ndiyo Njia yangu Iliyo Nyooka. Basi ifuateni, wala msifuate njia nyingine, zikakutengeni na Njia yake. Haya amekuusieni ili mpate kuchamngu} [Al-an`aam: 153].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii, enyi Waisilamu:**

Hakika pamoja na uhai kuna mauti, na pamoja na dunia kuna akhera, na hakika kila kitu kina mwenye kukihesabia, na kila kitu kina mwenye kukichunga, na kila jema lina thawabu, na kila ovu lina adhabu, na hakika kila muda uko na mwisho ulioandikiwa, na hapana budi na mwendani ambaye utazikwa naye hali yeye yupo hai na wewe umekufa, basi akiwa mkarimu atakukirimu, na akiwa mtwevu atakufanyia uovu, kisha hatafufuliwa ila akiwa na wewe, wala hutaulizwa ila kumuhusu yeye, basi usimfanye ila kuwa mwema, kwani akiwa mwema hutapumbaa ila naye, na akiwa muovu hutapata hofu ila kutoka kwake, naye ni amali yako!

Basi kithirisha amali njema, nyooka juu ya Dini yako, jisubirishe juu ya kuitia nguvu, epuka makatazo yake, tekeleza maamrisho yake, shikamana na msingi wa Dini yako, simama kutekeleza yanayolazimu kwayo, jiandae na silaha ya elimu, imani na amali njema, waidhika na mazingatio ya majanga, zingatia mawaidha ya Qur-ani, kwani ni yenye habari za kweli, na mtaje Allah maisha yako yote, kwani kumtaja Allah hakuna mapumziko wala kumalizika, na kithirisha istighfari kwa ajili ya upungufu, na mshukuru Allah kwa kukuafikia.

Kisha mswalieni na msalimieni mbora wa viumbe vya Allah; Muhammad ibnu Abdillah, kwani Mola wenu Mlezi akuamrisheni kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# KUWA NA DHANA NJEMA KWA ALLAH[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakayempoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha, na kamateni Uislamu katika kishiko madhubuti kabisa.

**Enyi Waisilamu:**

Tawhidi ni haki ya Allah juu ya waja, na kwa ajili yake alitumiliza Mitume, na akateremsha vitabu, na uhakika wake ni: kumpwekesha Allah kwa ibada, na ibada ni: Jina liliokusanya kila anayoyapenda Allah na kuyaridhia - miongoni mwa kauli na matendo; ya dhahiri na ya batini -, unao moyo ibada zinazo uhusu, na ibada zake ni kubwa zaidi, nyingi zaidi na za kudumu zaidi kuliko ibada za viungo, na kuingia kwa amali za moyo katika imani ni aula zaidi kuliko amali ya viungo; kwani imani inayosimama kwa moyo kielimu na kihali ndio msingi mkusidiwa, na amali za dhahiri ni zenye kutimiza na kuandama, na wala haziwi njema zenye kukubaliwa ila kwa kupitia amali ya moyo; basi hiyo ndiyo roho ya ibada na kiini chake, na endapo amali za dhahiri zitaikosa zitakuwa ni kama mwili uliokufa usio na roho, na kwa kutengea kwa moyo ndio unatengea mwili wote; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe kumi na nane, mwezi wa Rabiul Aakhir, mwaka elfu moja mia nne na thalathini na tisa hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

«**Jueni ya kwamba ndani ya mwili mna kinyama, endapo kitatengea basi mwili mzima utatengea, jueni kuwa hicho kinyama ni moyo**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Kuzidiana kwa waja kunakuwa kwa kuzidiana yaliomo ndani ya nyoyo, na kwayo ndio amali zinazidiana, na hapo [moyoni] ndipo sehemu anapoangalia Mola Mlezi kutoka kwa waja wake; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Hakika Allah haangalii miili yenu, wala sura zenu, lakini anaangalia nyoyo zenu na amali zenu**», imepokewa na Muslim.

Kuwa na dhana njema na Allah ni katika amali za nyoyo zilizosisitizwa; kwani hilo ni katika faradhi za Uisilamu na moja wapo wa haki za Tawhidi na yanayowajibishwa nayo, na maana yake yenye kukusanya ni: Kila dhana inayolingana na ukamilifu wa dhati ya Allah aliyetakasika, Majina yake na Sifa Zake, nayo ni tagaa la elimu ya kumjua Allah na kumtambua, nayo inajengewa juu ya kujua ukunjufu wa rehema ya Allah, ushindi wake, ihsani yake, kudura yake, elimu yake, na uzuri wa kuchagua kwake, na huenda likawa hilo kupitia kushuhudia baadhi ya Majina ya Allah na Sifa zake.

Na yule ambaye kutasimama moyoni mwake hakika ya maana ya Majina ya Allah na Sifa zake basi itasimama ndani yake [moyo wake] dhana njema inayonasibiana na kila Jina na Sifa, kwa sababu kila Sifa ina ibada mahususi, na dhana njema inayoihusu.

Ukamilifu wa Allah, utukufu wake, uzuri wake na kuwaneemesha kwake waja wake, yote hayo yanawajibisha kuwa na dhana njema Naye Mwenye ushindi na utukufu, na Allah amewaamrisha waja wake hilo katika kauli yake:

﴿وَأَحۡسِنُوٓاْۚ إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلۡمُحۡسِنِينَ﴾

{Na fanyeni wema. Hakika Allah huwapenda wafanyao wema} [Al-Baqarah: 195],

Sufyan Ath-thauri amesema: "hisinisheni dhana [zenu] kwa

Allah", na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisisitiza hilo kabla ya kufa kwake kwa ajili ya utukufu wa cheo chake; Jabir Allah amridhie alisema: «Nilimsikia Mtume wa Allah kabla kufa kwake kwa siku tatu akisema: Asife mmoja wenu isipokuwa yeye ni mwenye kumhisinishia dhana Allah mwenye ushindi na utukufu», imepokewa na Muslim.

Allah amewasifu waja wake wanyenyekevu kwa kuwa na dhana njema Naye, na akawajaalia bishara yao ya hapa duniani ni kuwasahilishia ibada na akaifanya [dhana yao njema] ni msaada kwao; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَٱسۡتَعِينُواْ بِٱلصَّبۡرِ وَٱلصَّلَوٰةِۚ وَإِنَّهَا لَكَبِيرَةٌ إِلَّا عَلَى ٱلۡخَٰشِعِينَ ۞ ٱلَّذِينَ يَظُنُّونَ أَنَّهُم مُّلَٰقُواْ رَبِّهِمۡ وَأَنَّهُمۡ إِلَيۡهِ رَٰجِعُونَ﴾

{Na tafuteni msaada kwa kusubiri na kwa kusali; na kwa hakika jambo hilo ni gumu isipokuwa kwa wanyenyekevu * Ambao wana yakini kuwa hakika watakutana na Mola wao Mlezi na ya kuwa hakika watarejea kwake} [Al-Baqarah: 45-46].

na Mitume - salamu ziwashukie - walipata cheo cha juu katika kumjua kwao Allah; basi wakategemeza mambo yao kwake kwa dhana yao njema kwa Mola wao Mlezi, Ibrahim salamu zimshukie alimuacha [mke wake] Haajar na mwanawe Isamail sehemu ya nyumba [Kaaba] na hali Makkah siku hiyo hakuna mtu yeyote, wala hakuna maji, kisha Ibrahim akageuka kuondoka, na Haajar akamuandama na akasema:

«**Ewe Ibrahim! Unaenda wapi na kutuacha katika wangwa huu ambayo hakuna ndani yake mtu wala kitu? Akamuambia hilo mara kadhaa, na akawa [Ibrahim] hageuki kwake, basi [Haajar] akamuambia: Je ni Allah ndiye amekuamrisha hivi? [Ibrahim] akasema: Ndio, akasema: basi hatatupoteza**», imepokewa na Bukhari; basi ikawa miongoni mwa mwisho wa dhana yake njema kwa Allah yale yaliokuwa, ya kutoka maji yaliobarikiwa, na nyumba [Kaaba] ikaimarishwa, akawa Ismail Nabii, na wa mwisho wa Manabii na kiongozi wa Mitume akawa katika kizazi chake.

Yakub salamu zimshukie aliwakosa wanawe wawili, akasubiri, na amtegemezea Allah amri yake, na akasema:

﴿إِنَّمَآ أَشۡكُواْ بَثِّي وَحُزۡنِيٓ إِلَى ٱللَّهِ﴾

{Akasema: Hakika mimi namshitakia Allah sikitiko langu na huzuni yangu [Yusuf: 86],

na ukabakia moyo wake ukiwa umejaa dhana njema kwa Allah na kwamba Yeye ni mbora wa wenye kuhifadhi, na akasema:

﴿عَسَى ٱللَّهُ أَن يَأۡتِيَنِي بِهِمۡ جَمِيعًاۚ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلۡعَلِيمُ ٱلۡحَكِيمُ﴾

{Asaa Allah akaniletea wote pamoja. Hakika Yeye ni Mjuzi Mwenye hekima} [Yusuf: 83],

naye salamu zimshukie akawaamrisha watoto wake hilo, akasema;

﴿يَٰبَنِيَّ ٱذۡهَبُواْ فَتَحَسَّسُواْ مِن يُوسُفَ وَأَخِيهِ وَلَا تَاْيۡـَٔسُواْ مِن رَّوۡحِ ٱللَّهِۖ
إِنَّهُۥ لَا يَاْيۡـَٔسُ مِن رَّوۡحِ ٱللَّهِ إِلَّا ٱلۡقَوۡمُ ٱلۡكَٰفِرُونَ﴾

{Enyi wanangu! Nendeni mkamtafute Yusuf na nduguye, wala msikate tamaa na faraji ya Allah. Hakika hawakati tamaa na faraji ya Allah isipo kuwa watu makafiri} [Yusuf: 87].

Wana wa Israili walikumbwa na udhia wasioweza kuhimili, na pamoja ukubwa wa janga inabakia kuwa ndani dhana njema kwa Allah mna matarajio na njia; basi Musa salamu zimshukie akaiambia kaumu yake:

﴿ٱسۡتَعِينُواْ بِٱللَّهِ وَٱصۡبِرُوٓاْۖ إِنَّ ٱلۡأَرۡضَ لِلَّهِ يُورِثُهَا مَن يَشَآءُ مِنۡ عِبَادِهِۦۖ وَٱلۡعَٰقِبَةُ لِلۡمُتَّقِينَ﴾

{Ombeni msaada kwa Allah, na subirini. Hakika ardhi ni ya Allah. Naye humrithisha amtakaye katika waja wake. Na mwisho [mwema] ni wa wachamngu} [Al-a`raaf: 128],

na mazito yalimlea Musa salamu zimshukie pamoja na waliokuwa naye, bahari iko mbele yao, na Firauni na jeshi lake wako nyuma yao, na wakati huo:

﴿قَالَ أَصۡحَٰبُ مُوسَىٰٓ إِنَّا لَمُدۡرَكُونَ﴾

{watu wa Musa wakasema: Hakika sisi bila ya shaka

tumepatikana} [Ash-shu`araa: 61].

likawa jibu liliotoka kwa Nabii aliyezungumzishwa [na Allah, yaani Musa] ni lenye kushuhudia ukuu wa kumtegemea kwake Allah, na dhana yake njema kwa Mola Mlezi mwenye uwezo:

﴿قَالَ كَلَّآۖ إِنَّ مَعِيَ رَبِّي سَيَهۡدِينِ﴾

{(Musa) akasema: Hasha! Hakika yuko pamoja nami Mola wangu Mlezi. Yeye ataniongoa} [Ash-shu`araa: 62], wahyi ukaja na yasiopita katika fikra:

﴿فَأَوۡحَيۡنَآ إِلَىٰ مُوسَىٰٓ أَنِ ٱضۡرِب بِّعَصَاكَ ٱلۡبَحۡرَۖ فَٱنفَلَقَ فَكَانَ كُلُّ فِرۡقٖ كَٱلطَّوۡدِ ٱلۡعَظِيمِ * وَأَزۡلَفۡنَا ثَمَّ ٱلۡأٓخَرِينَ * وَأَنجَيۡنَا مُوسَىٰ وَمَن مَّعَهُۥٓ أَجۡمَعِينَ * ثُمَّ أَغۡرَقۡنَا ٱلۡأٓخَرِينَ﴾

{Tulimletea wahyi Musa tukamwambia: Piga bahari kwa fimbo yako. Basi ikatengana, na kila sehemu ikawa kama mlima mkubwa * Na tukawajongeza hapo wale wengine * Tukawaokoa Musa na walio kuwa pamoja naye wote * Kisha tukawazamisha hao wengine}. [Ash-shu`araa: 62].

Kiumbe mwenye kumuabudu Allah zaidi na mwenye dhana njema Naye zaidi ni: Nabii wetu Muhammad swala na salamu za Allah zimshukie; kaumu yake walimuudhi, akabaki akiwa ni mwenye kuamini ahadi ya Allah na kuinusuru kwake Dini yake, Malaika wa majabali alimuambia: «**Ukitaka niwafunike na 'Akhshabaini' [majabali mawili ya Makkah], Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akasema: Bali natarajia Allah atoe migongoni mwao watakaomuabudu Allah wala hawatamshirikisha na chochote**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Katika hali ya dhiki kabisa na nyakati za giza kubwa kabisa Nabii - swala na salamu za Allah zimshukie - haachi kumdhania Mola wake Mlezi dhana njema. Alitolewa Makkah, na akiwa njiani aliingia katika pango ya 'hiraa', Makafiri wakamfuata, mara tu wakawa wamemzingira, basi akawa anamwambia sahibu wake ili kumtia nguvu:

﴿لَا تَحۡزَنۡ إِنَّ ٱللَّهَ مَعَنَا﴾

{Usihuzunike. Hakika Allah yu pamoja nasi}, [At-Taubah: 40] Abubakar Allah amridhie amesema: «Nilisema kumwambia Nabii swala na salamu za Allah zimshukie na hali nipo ndani ya pango: Lau mmoja wao ataangalia miguu yake atatuona chini ya miguu yake, [Mtume] akasema: ewe Abubakar! Ni ipi dhana yako kwa wawili Allah ndiye watatu wao?» Wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Pamoja na yaliomfika miongoni mwa udhia, majanga, na vita kutoka kila upande, ila yeye ni mwenye yakini ya kufika kwa Dini hii pande zote kwa zama zote, na alikuwa akisema: «Hakika litafika jambo hili sehemu zote zilifika usiku na mchana, wala Allah hataacha nyumba ya dongo wala ya sufi, isipokuwa Allah ataiingiza Dini hii, kwa ushindi wa mshindi au udhalilifu wa dhalili», imepokewa na Ahmad, na 'Aarabi' alimtolea upanga Nabii swala na salamu za Allah zimshukie akiwa amelala, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Nikaamka nao [upanga] uko mkononi mwake ukiwa wazi, [Aarabi] akasema: Ni nani atakukinga na mimi? Nikasema: Allah - mara tatu -; wala hakumuadhibu, na ['aarabi'] akakaa**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, na katika riwaya ya Ahmad: «upanga ukamuanguka mkononi mwake».

Masahaba ni waja wenye yakini zaidi ya dhana njema zao kwa Allah baada ya Manabii, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿ٱلَّذِينَ قَالَ لَهُمُ ٱلنَّاسُ إِنَّ ٱلنَّاسَ قَدْ جَمَعُوا۟ لَكُمْ فَٱخْشَوْهُمْ فَزَادَهُمْ إِيمَٰنًا وَقَالُوا۟ حَسْبُنَا ٱللَّهُ وَنِعْمَ ٱلْوَكِيلُ﴾

{Walio ambiwa na watu: Kuna watu wamekukusanyikieni, waogopeni! Hayo yakawazidishia Imani, wakasema: Allah anatutosha, naye ni mbora wa kutegemewa} [Aalu-Imran: 173].

ibnu Ad-Daghina alimwendea Abubakar Allah amridhie ili [Abubakar] aswali na asome kwa siri au amrudishie hifadhi yake - yaani: avunje ahadi yake ya kumkinga, na awamakinishe makafiri wa kikureshi naye -, Abubakar Allah amridhie akasema:

«Basi mimi nakurudishia hifadhi yako, na naridhia hifadhi ya Allah mwenye ushindi na utukufu», imepokewa na Bukhari, na Umar Allah amridhie amesema: «Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie alituamrisha tutoe sadaka, hilo likaafiki niko na mali, nikasema: Ikiwa nitashinda siku, basi leo nitamshinda Abubakar. Akasema: Nikaja na nusu ya mali yangu. Akasema: Mtume swala na salamu za Allah zimshukie akaniambia: Umewabakishia nini watu wako? Nikasema: Mfano wake. Abubakar akamkujia na yote aliyokuwa nayo. Mtume wa Allah swala na salamu za Allah zimshukie akamwambia: Umewabakishia nini watu wako? Akasema: Nimewabakishia Allah na Mtume wake», imepokewa na Abu Daaud.

Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alimkujia Hadija nana wa wanawake wa ulimwenguni mwanzoni mwa Wahyi kuanza akamwambia: «Nimejiogopea nafsi yangu, Hadija Allah amridhie akamwambia: Hapana; chukua bishara njema! Wallaahi Allah hatakutweza kabisa, wallaahi wewe unaunga kizazi, unazungumza ukweli, unambeba asiyejiweza, unachuma yalioadimika na kuyawasilisha kwa watu, unakirimu mgeni, na unasaidia katika misiba ya haki», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na wema waliotangulia wa umma huu walifuata mwenendo huu, Sufyan Allah amrehemu amesema: "Sipendelei iwe hisabu yangu - yaani: kulipwa kwangu kwa mema na maovu - amewakilishwa nayo wazazi wangu, Mola wangu ni bora kwangu kuliko wazazi wangu», na ilikuwa miongoni mwa maombi ya Said ibnu Jubair Allah amrehemu: "Ewe Allah, mimi nakuomba tawakkul ya ukweli, na dhana njema kwako».

Na wamo miongoni mwa majini waliowema, dhana zao kwa Allah ni njema, wana yakini ya nguvu za Allah, na ukunjufu wa elimu yake; na katika kauli zao:

﴿وَأَنَّا ظَنَنَّآ أَن لَّن نُّعۡجِزَ ٱللَّهَ فِي ٱلۡأَرۡضِ وَلَن نُّعۡجِزَهُۥ هَرَبٗا﴾

{Nasi tulijua kuwa hatutomshinda Allah duniani, wala

hatuwezi kumponyoka kwa kukimbia}. [Al-jinn: 12].

Hakika wako miongoni mwa waja wa Allah ambao lau ataapa basi Allah atamtekelezea, si kuapa kwa kumkatia Allah na kumlazimisha, lakini ni dhana njema kwake aliyetukuka, na ni katika shani ya muumini kuwa na dhana njema kwa Allah katika nyakati zote na kila hali, na ni aula kuwa hivo pindi anapomuomba na kuzungumza naye, akiwa na yakini ya ukaribu wake, na kuwa Yeye humuitikia anayemuomba, wala hamkoseshi anayemtarajia.

Na dhana njema ya mtu kwa Mola wake Mlezi, ni miongoni mwa sababu za kukubaliwa toba, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema katika anayoyapokea kutoka kwa Mola wake Mlezi:

«**Mja wangu ametenda dhambi; akajua kuwa ana Mola Mlezi anayesamehe dhambi na anaadhibu kwa dhambi, fanya utakalo; nimekusamehe**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Katika mazito na misiba zinabainika dhana njema na zinakashifika dhana mbovu, katika vita vya Uhud waumini walikuwa imara, na wasiokuwa wao walikuwa wakimdhania Allah dhana ya kijahili, na katika vita vya Ahzaab dhana kwa Allah zilikuwa tofauti, Allah amesema kuhusu kipote:

﴿هُنَالِكَ ٱبۡتُلِيَ ٱلۡمُؤۡمِنُونَ وَزُلۡزِلُواْ زِلۡزَالٗا شَدِيدٗا ۝ وَإِذۡ يَقُولُ ٱلۡمُنَٰفِقُونَ وَٱلَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٞ مَّا وَعَدَنَا ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥٓ إِلَّا غُرُورٗا﴾

{Hapo ndipo waumini walipojaribiwa, na wakatikiswa mtikiso mkali. Na waliposema wanaafiki na wale wenye maradhi katika nyoyo zao: Allah na Mtume wake hawakutuahidi ila udanganyifu} [Al-Ahzaab: 11-12],

ama masahaba walikuwa na Yakini kuwa mazito ni mtihani utokao kwa Allah na baada yake huja ushindi na faraji, amesema aliyetakasika kuwahusu:

﴿وَلَمَّا رَءَا ٱلۡمُؤۡمِنُونَ ٱلۡأَحۡزَابَ قَالُواْ هَٰذَا مَا وَعَدَنَا ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥ وَصَدَقَ ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥۚ

وَمَا زَادَهُمۡ إِلَّآ إِيمَٰنٗا وَتَسۡلِيمٗا﴾

{Na Waumini walipo yaona makundi, walisema: Haya ndiyo aliyo tuahidi Allah na Mtume wake. Na Allah na Mtume wake wamesema kweli. Na hayo hayakuwazidisha ila Imani na utiifu}. [Al-Ahzaab: 22].

Njia ya kutokea katika dhiki, majanga, na hamu ni dhana njema kwa Allah; kwani wale watatu waliobaki nyuma [wasihudhurie vita vya Tabuk] Allah hakuwaondolea janga lililowashukia ila kwa dhana yao njema kwa Allah, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَعَلَى ٱلثَّلَٰثَةِ ٱلَّذِينَ خُلِّفُواْ حَتَّىٰٓ إِذَا ضَاقَتۡ عَلَيۡهِمُ ٱلۡأَرۡضُ بِمَا رَحُبَتۡ وَضَاقَتۡ عَلَيۡهِمۡ أَنفُسُهُمۡ وَظَنُّوٓاْ أَن لَّا مَلۡجَأَ مِنَ ٱللَّهِ إِلَّآ إِلَيۡهِ ثُمَّ تَابَ عَلَيۡهِمۡ لِيَتُوبُوٓاْۚ إِنَّ ٱللَّهَ هُوَ ٱلتَّوَّابُ ٱلرَّحِيمُ﴾

{Na pia wale watatu walioachwa nyuma hata dunia wakaiona dhiki juu ya ukunjufu wake, na nafsi zao zikabanika, na wakayakinisha kuwa hapana pa kumkimbia Allah isipokuwa kwake Yeye. Kisha akawaafikia toba ili watubu. Hakika Allah ndiye Mwenye kupokea toba na Mwenye kurehemu} [At-Taubah: 118]

Na Allah ni mwenye nguvu muweza, na nusra yake kwa waja wake na vipenzi vyake hakuna mwenye kuighilibu, na ni katika yakini kuwa imani na nusra yake, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿إِن يَنصُرۡكُمُ ٱللَّهُ فَلَا غَالِبَ لَكُمۡۖ وَإِن يَخۡذُلۡكُمۡ فَمَن ذَا ٱلَّذِي يَنصُرُكُم مِّنۢ بَعۡدِهِۦ﴾

{Akikunusuruni Allah hapana wa kukushindeni, na akikutupeni ni nani basi, baada yake Yeye ataye kunusuruni?} [Aalu-Imran: 160].

Naye aliyetakasika ni mwenye kurehemu [Rahiim] mwingi wa rehema [Rahmaan], atakaye muamini, akatenda mema na akatarajia vipawa vya rehema zake basi atazipata, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Pindi Allah alipomaliza kuumba aliandika katika kitabu chake, nacho kiko kwake juu ya Arshi: Hakika rehema**

**zangu zimeshinda hasira zangu**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Yule aliyefikwa na dhiki ya maisha basi dhana njema yake [kwa Mola wake Mlezi] ni ukunjufu na faraja, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**aliyefikwa na mahitaji akayateremsha kwa watu basi mahitaji yake hayatatekelezwa, aliyefikwa na mahitaji akayateremsha kwa Allah; basi imekurubia Allah kumfungulia riziki karibuni au baadaye**», imepokewa na Tirmidhi. Zubeir ibnul Aw-Waam alisema kumwambia mwanawe Abdallah Allah awaridhie wote wawili: "Ewe mwanangu! Unaposhindwa na chochote katika hili - yaani: Deni kulilipa -, basi taka msaada kwa Bwanangu. [Abdallah] akasema: Wallahi sikujua aliyoyakusudia hadi niliposema: Ewe babangu! Ni nani Bwanako? Akasema: Ni Allah. Basi wallahi sikuwahi kuingia katika janga la deni lake ila nikisema: Ewe bwana wa Zubair! Mkidhie deni lake; basi [Allah] akilikidhi", imepokewa na Bukhari.

Naye Aliyetakasika ni mkunjufu wa msamaha na vipawa, na atakayekuwa na dhana njema Naye katika ukwasi wake, ukarimu wake, na msamaha wake atampa anayoyaomba. [Allah] aliyetakasika anashuka kila usiku akisema:

«**Ni nani ataniita nimuitikie? Ni nani ataniomba nimpatie? Ni nani ataniomba msamaha nimsamehe?** », wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, na Mikono yake miwili imejaa,

«hayapunguwi kwa kutoa, Naye ni mtoaji sana usiku na mchana».

Naye Allah ni mwenye kukubali sana toba, hufurahi kwa toba za waja, na hukunjua Mkono wake usiku ili aliyefanya makosa mchana atubie, na hukunjua Mkono wake mchana ili aliyefanya makosa usiku atubie, na ni katika Sifa zake za ukamilifu kuwa aliyetakasika hamrudishi aliyemuijia, na wakati ambao mja ahitajia zaidi kuwa na dhana njema kwa Allah ni pindi ajali yake inapokurubia, akaaga dunia yake, na akaelekea kwa Mola wake

Mlezi, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Mmoja wenu asife ila hali yeye ni mwenye dhana njema kwa Allah mwenye ushindi na utukufu**», imepokewa na Muslim.

Mnao katika ibada hii [ya kuwa na dhana njema kwa Allah] kutekeleza amri ya Allah, na kutekeleza ibada yake, na mja atapata kutoka kwa Mola wake Mlezi yale aliyomdhania nayo, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«Allah aliyetukuka anasema: **Mimi niko katika dhana ya mja wangu kwangu, na niko naye pindi anaponidhukuru**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea. Ibnu Mas'ud Allah amridhie amesema: "Mja hawi na dhana njema kwa Allah; ila Allah humpatia aliyoyadhania, hilo ni kwa kuwa heri ipo Mkononi mwake aliyetakasika".

Pindi mja anaporuzukiwa dhana njema kwa Mola wake Mlezi; basi hakika Allah amemfungulia mlango mkubwa wa heri katika Dini, Ibnu Mas'ud Allah amridhie amesema: "Naapa na Yule ambaye hakuna apasaye kuabudiwa ila Yeye! Hajawahi mja muumini kupatiwa kitu bora zaidi kuliko dhana njema kwa Allah".

Amali za watu ni kwa kadri ya dhana zao kwa Mola wao Mlezi, ama muumini alikuwa na dhana njema kwa Allah kwa hivyo akafanya amali njema, ama kafiri alikuwa na dhana mbaya kwa Allah basi akafanya amali mbaya. Mnao katika ibada hii ubora wa Uislamu na ukamilifu wa Imani, nayo ndio njia ya kumfikisha mwenye kuifuata Peponi. Ni ibada ya kimoyo inayorithisha kumtegemea Allah na kuwa na imani Naye. Ibnul Qayyim Allah amrehemu amesema: "kumtegemea kwako Mola wako Mlezi kunakuwa kwa kadri ya dhana njema yako kwake na kumtarajia kwako, na kwa sababu hiyo baadhi yao [wafasiri] waliitafsiri Tawakkul kuwa ni dhana njema kwa Allah, na tafsiri ya undani: kuwa dhana njema inamuita [mtu] katika kumtegemea Allah; kwa kuwa haiwezekani kutemgemea uliye na dhana mbaya kwake, wala kumtegemea usiyemtarajia".

Ni katika athari za ibada: Utulivu wa moyo, kumuelekea Allah na kutubia kwake, wala hakuna lenye kuukunjua moyo zaidi baada ya Imani kuliko kumtegemea Allah na kumtarajia, kwani mnao ndani yake yenye kumfanya mja awe na fali njema, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Hakuna maambukizo wala nuksi, na napenda fali njema**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea. Al-Haliimi Allah amrehemu amesema: "Tashaaum [nuksi]: ni dhana mbaya kwa Allah, na Tafaaul [fali njema]: ni dhana njema kwa Allah".

[dhana njema] ni usaidizi kwa mtu juu ya kuwa mkarimu na shujaa, na inampa nguvu, Abu Abdillah As-Saaji Allah amrehemu amesema: «Atakayemtegemea Allah, hakika amekusanya nguvu zake, nayo ndio maandalizi bora zaidi na matayarisho mazuri zaidi". Salamata ibnu Diinar Allah amrehemu aliambiwa: "Ewe Abu Haazim! Ni yapi mali yako? Akasema: Kumtegemea Allah na kukata tamaa na vilivyoko katika mikono ya watu".

Atakaye kuwa na dhana njema kwa Mola wake Mlezi nafsi yake itakuwa karimu na itatoa mali yake ikiwa na yakini na kauli ya Allah:

﴿وَمَآ أَنفَقۡتُم مِّن شَيۡءٖ فَهُوَ يُخۡلِفُهُۥ﴾

{Na chochote mtakacho kitoa, basi Yeye [Allah] atakilipa badala yake}, Suleiman Ad-Daaraani Allah amrehemu amesema: "atakayemtegemea Allah katika riziki yake tabia yake njema itazidi, na itamletea busara, na nafsi yake itakuwa karimu katika matumizi yake, na wasiwasi wake katika Swala yake utapungua".

Nayo [dhana njema] ni yenye kupeleka kutarajia yalio kwa Allah, na kuaminia ahadi yake, na kutenda heri hali ya kutumai fadhila zake [Allah] kwa mujibu wa yaliokuja katika kauli yake:

﴿وَمَا يَفۡعَلُواْ مِنۡ خَيۡرٖ فَلَن يُكۡفَرُوهُ﴾

{Na heri yoyote wanayoifanya hawatanyimwa malipo yake} [Saba`: 39],

Allah anawaamili waja wake kwa kadri ya dhana zao kwake,

na malipo ni kwa kulingana na amali; basi atakaye dhania heri atapata hilo, na atakaye dhania mengineo hakika amehasirika, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Allah mwenye ushindi na utukufu amesema: Mimi niko kama anavyonidhania mja wangu; basi anidhanie anavyotaka, akinidhania heri ataipata, na akinidhania shari ataipata**», imepokewa na Ahmad, na mja anapokuwa mwenye dhana njema kwa Allah basi hakika Allah katu hatamfanyia kinyume cha dhana yake, na aliyekuwa na dhana njema na Mola wake Mlezi atasema siku ya Kiyama:

﴿هَآؤُمُ ٱقۡرَءُواْ كِتَٰبِيَهۡ ۞ إِنِّي ظَنَنتُ أَنِّي مُلَٰقٍ حِسَابِيَهۡ ۞
فَهُوَ فِي عِيشَةٖ رَّاضِيَةٖ ۞ فِي جَنَّةٍ عَالِيَةٖ﴾

{Haya someni kitabu changu! * Hakika nalijua ya kuwa nitapokea hisabu yangu * Basi yeye atakuwa katika maisha ya kupendeza * Katika Pepo ya juu} [Al-Haaqqah: 19-22].

**Na baada ya haya, enyi Waisilamu:**

Allah ni Mkarimu, mkubwa, mwenye nguvu aliye adhimu, anapokitaka kitu hukiambia: Kuwa, nacho kikawa. Ameahidi kukihifadhi Kitabu chake, na kunusuru Dini yake, na amejaalia mwisho mwema ni wa wachamngu, anamruzuku anayemtaka bila hesabu, na huyaondoa majanga ya mwenye kukimbia kwake.

Na yule itakayozidi elimu yake kumhusu Allah; yakini yake itazidi, na atakaye kuwa na dhana mbaya Naye; basi ni kwa sababu ya ujinga wake katika Majina yake na Sifa zake za ukamilifu, na hilo ni katika sifa za watu wa kijahili, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿يَظُنُّونَ بِٱللَّهِ غَيۡرَ ٱلۡحَقِّ ظَنَّ ٱلۡجَٰهِلِيَّةِ﴾

{wakamdhania Allah dhana isiyo kuwa ya haki, dhana ya kijinga} [Aalu-Imran: 154]

Na katika matunda ya kuamini Majina ya Allah na Sifa zake ni: dhana njema kwake, kumtegemea Yeye, na kusalimisha mambo kwake.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿فَمَا ظَنُّكُم بِرَبِّ ٱلۡعَٰلَمِينَ﴾

{Mnamdhania nini Mola Mlezi wa walimwengu wote?} [As-Swaaffaat: 87].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi Waislamu:**

Uhakika wa dhana njema kwa Allah unadhihiri katika amali njema, na inakuwa ni yenye kunufaisha inapokuwa na ihsani, na watu wenye dhana njema zaidi na Mola wao Mlezi ni wale wenye kumtii zaidi, na kila inapokuwa njema dhana ya mja kwa Mola wake Mlezi basi hapana budi amali yake nayo itakuwa njema, na yule ambaye matendo yake yatakuwa maovu basi dhana zake [kwa Mola wake] zitakuwa mbovu, na pindi dhana njema inapoambatana na kufanya maasi basi itakuwa ni kuhisi amani ya makri [mipango] ya Allah, na endapo dhana njema itampelekea mtu kufanya utiifu basi hiyo ndio yenye kunufaisha, na inapopungua hiyo [dhana njema] katika moyo basi maasi yatadhihiri katika viungo.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# YENYE KUTIA DOSARI TAWHIDI[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakaye mpoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha; kwani atakayemcha Mola wake Mlezi ataokoka, na atakaye upa Ukumbusho wake kisogo atapotea.

**Enyi Waisilamu:**

Saada ya mja ipo katika ukamilifu wa kumuabudu kwake Allah, na kutekeleza ibada ipasavyo kunakuwa kwa kumtakasia Allah amali na kufuata uongofu wa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie, na pindi mja atafanya amali yoyote, na asiwe ndani yake ni mwenye kumtakasia Allah basi amali yake itakuwa ni kama vumbi la kupepererushwa, [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَقَدِمْنَآ إِلَىٰ مَا عَمِلُواْ مِنْ عَمَلٍ فَجَعَلْنَٰهُ هَبَآءً مَّنثُورًا﴾

{Na tutayaendea yale waliyo yatenda katika vitendo vyao, tuvifanye kama mavumbi yaliyo tawanyika}, [Al-furqaan: 23] na pindi atakapomtakasia Allah [amali], na asiwe ni mwenye kufuata uongofu wa Nabii swala na salamu za Allah zimshukie amali yake itakuwa ni yenye kurudishwa kwake; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe ishirini na nane, mwezi wa Dhul-Qa'adah, mwaka elfu moja mia nne na ishirini na sita, katika msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

«**Yeyote atakayefanya amali yoyote isiyo na maamrisho yetu; basi itakuwa ni yenye kurudishwa**», imepokewa na Muslim, na amali itakapokuwa ni yenye kutakaswa iliyosibu [uongofu wa Mtume] basi itakuwa ni yenye kukubaliwa na kushukuriwa; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ كَانَتۡ لَهُمۡ جَنَّٰتُ ٱلۡفِرۡدَوۡسِ نُزُلًا﴾

{Hakika wale walio amini na wakatenda mema mashukio yao yatakuwa kwenye Pepo za Firdausi}. [Al-Kahf: 107].

Na Dini imesimama juu ya kukanusha na kuthibitisha, Uisilamu wa mja hausilihi ila kwa hayo mawili; kujitakasa na waabudiwa wengine na watu wake, na kuthibitisha haki ya kuabudiwa kwa Allah peke yake; [Allah] aliyetukuka na aliye juu amesema:

﴿فَمَن يَكۡفُرۡ بِٱلطَّٰغُوتِ وَيُؤۡمِنۢ بِٱللَّهِ فَقَدِ ٱسۡتَمۡسَكَ بِٱلۡعُرۡوَةِ ٱلۡوُثۡقَىٰ لَا ٱنفِصَامَ لَهَاۗ وَٱللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ﴾

{Basi anaye mkufuru Shet'ani [na kila kinachoabudiwa kinyume na Allah] na akamuamini Allah bila ya shaka amekamata kishikio madhubuti, kisicho vunjika. Na Allah ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua} [Al-Baqarah: 256]. na [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**atakayesema 'laa ilaaha illa llaah', na akakufuru kila kinachoabudiwa kinyume na Allah; mali yake na damu yake zitakuwa haramu [kuzifanyia uadui], na hesabu yake ni juu ya Allah aliye na ushindi na aliyetukuka**», imepokewa na Bukhari na Muslim.

Amri kubwa zaidi katika Uisilamu ni amri ya Tawhidi, na katazo kubwa zaidi ndani yake ni katazo la kinyume chake, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie aliulizwa:

«**Ni dhambi gani kubwa zaidi? Akasema: Ni umfanyie Allah mshirika na Yeye ndiye aliyekuumba**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea, na ulinganizi wa Mitume umeafikiana juu ya kuamrisha kumpwekesha Allah peke yake

kwa ibada, na kutahadharisha ushirikina au kuingia katika mipaka yake

﴿وَلَقَدۡ بَعَثۡنَا فِي كُلِّ أُمَّةٖ رَّسُولًا أَنِ ٱعۡبُدُواْ ٱللَّهَ وَٱجۡتَنِبُواْ ٱلطَّٰغُوتَ﴾

{Na kwa hakika kwa kila umma tuliutumia Mtume kwamba: Muabuduni Allah, na muepukeni twaghuti}, [An-Nahl: 36],

na atakaye dumu na kumuabudu Allah kama alivyoamrishwa [Allah] aliyetukuka na aliye juu atapata amani katika nafsi yake, mali yake, watoto wake, na nyumba yake, na atapata amani kaburini mwake, na siku ya kukusanywa na kuhesabiwa; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَلَمۡ يَلۡبِسُوٓاْ إِيمَٰنَهُم بِظُلۡمٍ أُوْلَٰٓئِكَ لَهُمُ ٱلۡأَمۡنُ وَهُم مُّهۡتَدُونَ﴾

{Wale ambao wameamini, na hawakuchanganya imani yao na dhuluma - hao ndio watakao pata amani na wao ndio walioongoka} [Al-an`aam: 82].

Tawhidi ya hakika ni yenye kufuta madhambi, yenye kuunguza makosa, yenye kuzuia kuingia Motoni; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Kwa hakika Allah amemuharamishia Moto yule atakaye sema 'laa ilaaha illa llaah', akikusudia hilo Uso wa Allah**», wamefikiana Bukhari na Muslim kuipokea, na atakaye tekeleza Tawhidi ya wajibu ipasavyo ataingia Peponi bila ya hesabu, na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie amehadithia sifa zao kwa kauli yake:

«**wao ni wale wasio omba kufanyiwa zunguo [ruqya], wasiojipisha moto, wasioitakidi nuksi na ni wenye kumtegemea Mola wao Mlezi**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea; nyoyo zao zimeshikamana na Allah, ni zenye kusalimisha mambo yao kwake.

Uharibifu wa shirki ni muovu; kwa kuwa inaporomosha amali na inamkasirisha Mola Mlezi; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَلَقَدۡ أُوحِيَ إِلَيۡكَ وَإِلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِكَ لَئِنۡ أَشۡرَكۡتَ لَيَحۡبَطَنَّ عَمَلُكَ
وَلَتَكُونَنَّ مِنَ ٱلۡخَٰسِرِينَ﴾

{Na kwa yakini yamefunuliwa kwako na kwa walio kuwa kabla yako: Bila ya shaka ukimshirikisha Allah amali zako zitaanguka, na lazima utakuwa miongoni mwa wenye kukhasiri} [Az-zumar: 65],

Na [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie alisema: «**atakayekufa na hali anamuomba asiyekuwa Allah mshirika ataingia Motoni**», imepokewa na Bukhari; bali hilo linawajibisha kukaa milele Motoni; kama alivyosema aliyetakasika:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ لَا يَغۡفِرُ أَن يُشۡرَكَ بِهِۦ وَيَغۡفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَآءُ﴾

{Hakika Allah hasamehe kushirikishwa Naye mwengine, na husamehe yalioduni ya hilo kwa anayemtaka}[An-Nisaa: 48],

Na kwa kuwa ushirikina unawajibisha kuangamia duniani na akhera; kipenzi cha Allah Ibrahim salamu zimshukie alimuomba Mola wake Mlezi amlinde kutokana nao, [Allah] aliyetakasika amesema akitutolea habari yake [alipoomba]:

﴿وَٱجۡنُبۡنِي وَبَنِيَّ أَن نَّعۡبُدَ ٱلۡأَصۡنَامَ﴾

{Na uniepushe mimi na wanangu na kuabudu masanamu}, Ibrahim At-Taymi Allah amrehemu alisema: "Na ni nani atakaye kuhisi amani ya balaa hii [ya ushirikina] baada ya Ibrahim [salamu zimshukie kujihofia]?!". [Ibrahim: 35],

Jambo bora zaidi atakalolingania mwenye kulingania ni Neno la Tawhidi na yanayojulishwa nalo; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema kumwambia Muaadh ibnu Jabal [alipomtuma Yemen kulingania]:

«**Hakika wewe unaiendea kaumu miongoni mwa waliopatiwa Kitabu; basi liwe la kwanza utakalo walingania ni: shahada ya 'laa ilaaha illa llaah'**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Atakaye muomba asiyekuwa Allah hakika atakuwa ameidhulumu nafsi yake

﴿وَلَا تَدۡعُ مِن دُونِ ٱللَّهِ مَا لَا يَنفَعُكَ وَلَا يَضُرُّكَۖ فَإِن فَعَلۡتَ فَإِنَّكَ إِذٗا مِّنَ ٱلظَّٰلِمِينَ﴾

{Na wala usiwaombe wasio kuwa Allah ambao hawakufai kitu wala hawakudhuru. Ukifanya hivyo basi utakuwa miongoni mwa walio dhulumu} [Yunus: 106]

na atayakaye piga goti kwa sanamu au akalinyenyekea kaburi akitarajia manufaa kutoka kwake basi ametaka yasiowezekana, na amedhani sarabi kuwa ni maji:

﴿وَمَنۡ أَضَلُّ مِمَّن يَدۡعُواْ مِن دُونِ ٱللَّهِ مَن لَّا يَسۡتَجِيبُ لَهُۥٓ إِلَىٰ يَوۡمِ ٱلۡقِيَٰمَةِ وَهُمۡ عَن دُعَآئِهِمۡ غَٰفِلُونَ * وَإِذَا حُشِرَ ٱلنَّاسُ كَانُواْ لَهُمۡ أَعۡدَآءٗ وَكَانُواْ بِعِبَادَتِهِمۡ كَٰفِرِينَ﴾

{Na nani mpotofu mkubwa kuliko hao wanao waomba badala ya Allah, ambao hawatawaitikia mpaka Siku ya Kiyama, na wala hawatambui maombi yao * Na ambao watu watakapo kusanywa watakuwa maadui zao, na wataikataa ibada yao}.

Kuwaomba maiti na kuwataka mahitaji ni mwito usiosikiwa, na majanga yasiopata faraja, [Allah] mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿وَٱلَّذِينَ تَدۡعُونَ مِن دُونِهِۦ مَا يَمۡلِكُونَ مِن قِطۡمِيرٍ * إِن تَدۡعُوهُمۡ لَا يَسۡمَعُواْ دُعَآءَكُمۡ وَلَوۡ سَمِعُواْ مَا ٱسۡتَجَابُواْ لَكُمۡۖ وَيَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِ يَكۡفُرُونَ بِشِرۡكِكُمۡۚ وَلَا يُنَبِّئُكَ مِثۡلُ خَبِيرٖ﴾

{Na hao mnao waomba badala yake [Allah] hawamiliki hata ugozi wa kokwa ya tende * Mkiwaomba hawasikii maombi yenu; na hata wakisikia hawakujibuni. Na Siku ya Kiyama watakataa ushirikina wenu. Na hapana atakaye kupa khabari vilivyo kama Yeye Mjuzi mno}. [Al-Ahqaaf: 5-6].

Kukeuka mpaka katika wafu na watu wema ndio sababu ya kukufuru binadamu na kuacha kwao Dini yao, na [Mtume] mteule amelitahadharisha hilo kwa kauli yake:

«**Ole wenu na kukeuka mipaka katika Dini, kwani kukeuka mipaka katika Dini kuliwaangamiza waliokuwa kabla yenu**», imepokewa na Nasai, na viumbe waovu zaidi ni wale waliokaa kiibada katika makaburi na wakayaomba badala ya Allah, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema kumwambia Ummu salama Allah amridhie:

«**Hao pindi anapokufa mtu mwema kwao - au mja mwema**

**- wanajenga Msikiti juu ya kaburi lake, na wakatengeneza ndani hizo sura [sura zao], hao ndio viumbe waovu zaidi mbele ya Allah**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na uchawi unazima nuru ya Imani na unavunja Uisilamu:

﴿وَلَقَدْ عَلِمُواْ لَمَنِ ٱشْتَرَىٰهُ مَا لَهُۥ فِي ٱلْأٓخِرَةِ مِنْ خَلَٰقٍ﴾

{Na hakika wanajua kwamba aliye khiari haya [kujifunza uchawi] hatakuwa na fungu lolote katika Akhera} [Al-Baqarah: 102], na kuwaendea makuhani ni uharibifu katika Dini na upungufu katika akili, [Allah] mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿قُل لَّا يَعْلَمُ مَن فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ٱلْغَيْبَ إِلَّا ٱللَّهُ﴾

{Sema: Hapana katika mbingu na ardhi ajuaye ya ghaibu isipo kuwa Allah, [An-Naml: 65], na [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Atakayemwendea kuhani au mcheza ramli, akamuuliza kitu na akamsadikisha; basi hakika [kwa hilo] ameyakufuru aliyo teremshiwa Muhammad**», imepokewa na Ahmad.

Hirizi za vikuku, nyuzi, kauri na mfano wake hazimzidishi mwenye kuzivaa ila unyonge na udhaifu katika kumtegemea Allah,

«**Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alimuona mtu katika mkono wake kuna kikuku cha shaba, akasema: Ole wako, ni nini hii? Akasema: nimevaa kutokana na maradhi ya mshipa, [Mtume] akasema: kuwa, hakika hiki hakikuzidishi ila udhaifu; itupe kando nawe, kwani wewe lau ungekufa na nacho kiko katika [mkono wako] haungefaulu milele**», imepokewa na Ahmad, na kuvaa hirizi ni kumshirikisha Allah; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**atakayefunga hirizi; hakika amefanya ushirikina**», imepokewa na Ahmad, na atakayefunga kitu basi Allah atamtegemeza kwa alichokifunga na ataangamia; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**atakayejifunga kitu atategemezwa kwacho**», imepokewa

na Tirmidhi.

Na baraka hazitarajiwi kutoka kwa miti na mawe, na kwa sababu yao, na hakika si mengine hayo ni viumbe vya Allah, havidhuru wala havinufaishi.

Kumwaga damu kwa kuchinga kurubani haifai ila kwa ajili ya Allah, na atakayechinja kwa asiyekuwa Allah atakuwa ameingia katika hali za ushirikina; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema: «Allah amemlani aliyechinjia asiyekuwa Allah», imepokewa na Muslim.

Nadhiri ni ibada; hafanyiwi asiyekuwa Allah, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**aliyeweka nadhiri ya kumtii Allah basi amtii, na aliyeweka nadhiri ya kumuasi Allah asimuasi**», imepokewa na Bukhari.

Atakayetaka ulinzi kwa Allah atamlinda, na atakayekimbilia kwa asiyekuwa Yeye atamuachilia [hatamuafikia wala kumnusuru], Nabii swala na salamu za Allah zimshukie anasema:

«**atakayeshukia sehemu, kisha akasema: *'audhu bikalimaati llaahi ttaammaati min sharri maa khalaq'*; basi hatadhurika na kitu chochote hadi aondoke sehemu yake ile**», imepokewa na Muslim.

Na yanapokushukia misiba ya maisha na majanga ya zama basi usitake uokozi kutoka kwa asiyekuwa Allah, wala usimuombe asiyekuwa Yeye, wala usimnyenyekee maiti aliye kaburini mwake, au mifupa iliyovunjika vunjika ndani ya ufuko wake, na nyanyua matakwa yako kwa aliye mbinguni; kwani huko ndiko kunaitikiwa maombi:

﴿أَمَّن يُجِيبُ ٱلۡمُضۡطَرَّ إِذَا دَعَاهُ﴾

{Au nani yule anaye mjibu mwenye shida pale anapo mwomba} [An-Naml: 62].

Wala hakuna pakuepuka mitihani:

﴿أَحَسِبَ ٱلنَّاسُ أَن يُتۡرَكُوٓاْ أَن يَقُولُوٓاْ ءَامَنَّا وَهُمۡ لَا يُفۡتَنُونَ﴾

{Je! Wanadhani watu wataachwa kwa kuwa wanasema:

Tumeamini. Nao wasijaribiwe?} [Al-Ankabuut: 2],

na pindi msiba unapokufika, basi ukabili na kuridhia na kujisalimisha [kadari ya Allah], mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿وَمَن يُؤۡمِنۢ بِٱللَّهِ يَهۡدِ قَلۡبَهُۥ﴾

{Na mwenye kumuamini Allah huuongoa moyo wake}, [At-Taghabun: 11]

Alqama Allah amrehemu amesema [kuhusu aya hii]: "huyu ni mtu anapatwa na msiba, akajua kuwa unatoka kwa Allah; basi akaridhia na akajisalimisha".

Wala usikasirikie yaliokwisha andikwa, kwani hasira haiyaondoshi, na tahadhari kujutia uchache wa hadhari [uliochukua] kabla ya kadari kutokea kwa neno "lau"; kwani [neno] hili linatoka kwa shetani, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Fanya bidii juu ya yanayokunufaisha, na taka msaada kwa Allah wala usilemae, na endapo utasibiwa na kitu basi usiseme: Lau ningefanya [kadha] ingekuwa kadha na kadha. Lakini sema: Allah amekadiria Naye hufanya alitakalo, kwani "lau" hufungua amali ya shetani**» ameipokea Muslim.

Basi salimisha mambo yako kwa Allah, na hautapata katika dunia ila kile ulichogawanyiwa:

﴿قُل لَّن يُصِيبَنَآ إِلَّا مَا كَتَبَ ٱللَّهُ لَنَا﴾

{Sema: Halitusibu ila alilo tuandikia Allah}, [At-Taubah: 51],

Ubaadata ibnu As-Swaamit Allah amridhie alisema kumwambia mwanawe: "Ewe mwanagu! Hakika hutapata ladha ya Imani hadi ujue [uyakinishe] kuwa lililokusibu halikuwa ni lenye kukukosa, na lililokukosa halikuwa ni lenye kukusibu".

Na kutegemea sababu kwa moyo [wako] na viungo ni dosari katika Tawhidi, na kubatilisha sababu kabisa ni kulemaa, na la wajibu ni kufanya sababu zinazofaa pamoja na kuufungamanisha moyo na Allah.

Na kwa kumtegemea Yeye aliyetakasika zito huwa jepesi,

riziki hukunjuliwa na janga hupata faraja.

Kuhisi amani kutokana na makri ya Allah ni ghururi:

﴿أَفَأَمِنُواْ مَكۡرَ ٱللَّهِۚ فَلَا يَأۡمَنُ مَكۡرَ ٱللَّهِ إِلَّا ٱلۡقَوۡمُ ٱلۡخَٰسِرُونَ﴾

{Je, wamejiaminisha na adhabu ya Allah, uwezo wake na kuwapatiliza wakiwa katika kughafilika? Kwani hawajiaminishi na hayo ila watu wenye kupata hasara} [Al-a`raaf: 99], na kuvunjika moyo na rehema za Allah ni kukata tamaa, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿قَالَ وَمَن يَقۡنَطُ مِن رَّحۡمَةِ رَبِّهِۦٓ إِلَّا ٱلضَّآلُّونَ﴾

{Na nani anayekata tamaa na rehema ya Mola wake Mlezi ila wale walio potea?}, [Al-Hijr: 56],

na kukusanya baina ya matarajio, hofu na mapenzi ni njia ya walio na hali ya katikati [ya sawa].

Ushirikina una milango iliyofichika, shetani anafanya bidii ili waja waiingie, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

{**Ninalowaogopea zaidi kwenu ni ushirikina mdogo, akaulizwa kuuhusu, akasema: Ni riya**», imepokewa na Ahmad,

Riya ni ugonjwa wa watendao amali, inaharibu amali, na inamughadhibisha Mola Mlezi, na inaogopewa zaidi na watu wema kuliko masihi dajali; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Nisiwajulisheni ninalowaogopea zaidi kuliko masihi dajali? Akasema [mpokezi]: Wakasema [Masahaba]: Kwani? [yaani: tujulishe], [Mtume] akasema: Ni ushirikina uliofichika: [Nayo ni] asimame mtu kuswali, aipambe swala yake kwa ajili ya kuona kuna mtu anamuangalia**», imepokewa na Ibnu Maajah.

Amali njema zinatarajiwa thawabu za Allah peke yake, wala hazikusudiwi pambo la Dunia, na atakaye ugeuza moyo wake kwa amali yake njema kuelekea pambo la Dunia; amali yake itaporomoka na atapata hasara katika akhera yake; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿مَن كَانَ يُرِيدُ ٱلۡحَيَوٰةَ ٱلدُّنۡيَا وَزِينَتَهَا نُوَفِّ إِلَيۡهِمۡ أَعۡمَٰلَهُمۡ فِيهَا وَهُمۡ فِيهَا لَا يُبۡخَسُونَ * أُوْلَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ لَيۡسَ لَهُمۡ فِي ٱلۡأٓخِرَةِ إِلَّا ٱلنَّارُۖ وَحَبِطَ مَا صَنَعُواْ فِيهَا وَبَٰطِلٞ مَّا كَانُواْ يَعۡمَلُونَ﴾

{Wanaotaka maisha ya dunia na pumbao lake tutawalipa humo vitendo vyao kamili. Na wao humo hawatopunjwa * Hao ndio ambao hawatakuwa na kitu Akhera ila Moto, na yataharibika waliyoyafanya, na yatapotea bure waliyokuwa wakiyatenda} [Huud;15-16].

Wala hakuna kipendezacho zaidi kwa Muisilamu kuliko Allah, wala hakuna kitukufu zaidi moyoni mwake kumliko Yeye aliyetukuka, basi Yeye ndiye adhimu ndani ya moyo wake, na Mkubwa ndani ya nafsi yake, naye [Muisilamu] ni mkweli katika kumpenda, haapi ila Naye peke yake, na kuapa na asiyekuwa Yeye aliyetakasika - kama vile Kaaba, Nabii, amana na walii -; ni ushirikina katika Tawhidi, [Mtme] swala na salamu zimshukie alisema: «**Atakaye apa na asiyekuwa Allah; amekufuru au ameshirikisha**», imepokewa na Tirmidhi.

Kukithirisha kuapa inapingana na kumuadhimisha Allah kifuani, basi hifadhi kiapo chako hata lau ni ukiwa mkweli, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَٱحۡفَظُوٓاْ أَيۡمَٰنَكُمۡ﴾

{na hifadhini viapo vyenu} [Al-Maa`idah: 89],

na kitahadhari [kiapo] katika urongo, kwani hicho ndicho cha kumzamisha mtu Motoni, na ni katika kumuadhimisha Allah: Kuridhia kiapo chake hata ikiwa anayesikia anajua kuwa aliyeapa ni mrongo, Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Musiape kwa mababa zenu, na atakayeapa kwa Allah basi aseme ukweli, na atakaye apiwa kwa Allah basi aridhie, na asiyeridhia kwa Allah basi si katika Allah kwa chochote**», imepokewa na Ibnu Maajah.

Na ni katika kumtukuza Allah: kutomrudisha aliyeomba kwa ajili ya Allah, [Mtume] swala na salamu za Allah zimshukie

alisema:

«**Atakaye jilinda na Allah mlindeni, na atakaye omba kwa ajili ya Allah mpeni, na aliyewaalika muitikieni**», imepokewa na Abu Daaud.

Kukejeli wakati na mabadiliko ya hali - miongoni mwa joto au baridi - ni kumuudhi Mola Mlezi wa walimwengu, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Allah mwenye ushindi na utukufu amesema: Binadamu ananiudhi, anatusi zama, na Mimi ndio zama [yaani: ndiye muendeshaji wa yanayotokea ndani ya zama], nageuza usiku na mchana**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Mbingu na ardhi zilisimama kwa ajili ya Dini, na kwa ajili yake ziliandaliwa Pepo na Moto, na kufanyia Dini au hukumu zake au watu wake walioishika shere; kunamtoa mtu katika Uisilamu; [Allah] mwenye ushindi na utukufu:

﴿وَلَئِن سَأَلْتَهُمْ لَيَقُولُنَّ إِنَّمَا كُنَّا نَخُوضُ وَنَلْعَبُ ۚ قُلْ أَبِٱللَّهِ وَءَايَٰتِهِۦ وَرَسُولِهِۦ كُنتُمْ تَسْتَهْزِءُونَ ۞ لَا تَعْتَذِرُوا۟ قَدْ كَفَرْتُم بَعْدَ إِيمَٰنِكُمْ﴾

{Na ukiwauliza, wanasema: Sisi tulikuwa tukipiga porojo na kucheza tu. Sema: Mlikuwa mkimfanyia maskhara Allah na Aya zake na Mtume wake? * Msitoe udhuru; mmekwisha kufuru baada ya kuamini kwenu!} [At-Taubah: 65-66].

Wala usimdhanie Allah dhana mbaya - kama vile kustahiki kwako zaidi ya ulivopewa au ukadharau neema iliyo katika mkono wa mwenzako ambayo Allah amempa -, hiyo ni dhana ya kijahili, kwani kila yaliyo ndani ya ulimwengu ni kwa amri yake na hekima yake:

﴿يَظُنُّونَ بِٱللَّهِ غَيْرَ ٱلْحَقِّ ظَنَّ ٱلْجَٰهِلِيَّةِ ۖ يَقُولُونَ هَل لَّنَا مِنَ ٱلْأَمْرِ مِن شَىْءٍ ۗ قُلْ إِنَّ ٱلْأَمْرَ كُلَّهُۥ لِلَّهِ﴾

{wakamdhania Allah dhana isiyo kuwa ya haki, dhana ya kijinga. Wakisema: Hivyo tuna lolote sisi katika jambo hili? Sema: Mambo yote ni ya Allah} [Aalu-Imran: 154].

Na kutengeneza/kupiga picha [ya viumbe vyenye roho] ni

katika madhambi makubwa, mwenye kufanya hilo ameahidiwa Moto; Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alisema:

«**Kila mtengeneza picha yuko Motoni, atajaaliwa kila picha aliyoitengeneza ni nafsi inamuadhibu ndani ya Moto**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Mtukuze Mola wako Mlezi haki ya kumtukuza, kwani Yeye ni Mkuu katika ufalme wake, aliyejuu ya Arshi yake, mwenye hikima katika sheria zake, basi yahifadhi aliyoyafaradhisha Allah juu yako miongoni mwa Swala za wajibu ndani ya wakati wake, na ole wako na kufanya upungufu ndani yake; kwani hizo [Swala] ndio nguzo ya Dini, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Ahadi ilio baina yetu na wao [makafiri] ni Swala, basi yeyote atakaye iacha atakuwa amekufuru**», imepokewa na Tirmidhi.

Na kuwa mwenye kuelekea kwa Mola wako Mlezi katika hali zako zote; amali zako zitasilihi.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ ٱلْعَٰلَمِينَ * 
لَا شَرِيكَ لَهُۥ ۖ وَبِذَٰلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا۠ أَوَّلُ ٱلْمُسْلِمِينَ﴾

{Sema: Hakika Swala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Allah, Mola Mlezi wa viumbe vyote * Hana mshirika naye. Na hayo ndiyo niliyo amrishwa, na mimi ni wa kwanza wa Waislamu} [Al-an`aam: 162-163].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

# HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii, enyi Waislamu:**

Dini ndio jambo bora zaidi unalomiliki, basi hifadhi Dini yako kwa kuepuka fitina, kwani hizo [fitina] zinachukua nyoyo, na zinaleta hamu ya starehe za haramu na shari, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Na atakaye jitokeza kwazo [fitina] zitamchukua**», imepokewa na Bukhari.

Na kuinamisha jicho kutokana na wanawake wa haramu kuwaona ni utakatifu wa nafsi, ni utiifu kwa Allah, na ni kunyanyuka kwa daraja, [Allah] aliyetukuka na aliyejuu amesema:

﴿قُل لِّلۡمُؤۡمِنِينَ يَغُضُّواْ مِنۡ أَبۡصَٰرِهِمۡ وَيَحۡفَظُواْ فُرُوجَهُمۡۚ ذَٰلِكَ أَزۡكَىٰ لَهُمۡ﴾

{Waambie Waumini wanaume wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao. Hili ni takaso bora kwao} [Al-an`aam: 162-163].

Mapambo ya mwanamke yako katika sitara yake, na urembo wake uko katika hijabu yake, na pambo lake liko katika kushikamana kwake na Dini yake, na wanawake wa kisahaba ni mfano wenye kuandamwa katika hijabu, sitara, na haya, [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِيُّ قُل لِّأَزۡوَٰجِكَ وَبَنَاتِكَ وَنِسَآءِ ٱلۡمُؤۡمِنِينَ يُدۡنِينَ عَلَيۡهِنَّ مِن جَلَٰبِيبِهِنَّۚ

ذَٰلِكَ أَدۡنَىٰٓ أَن يُعۡرَفۡنَ فَلَا يُؤۡذَيۡنَ﴾

{Ewe Nabii! Waambie wake zako, na binti zako, na wake za Waumini wajiteremshie nguo zao za kuwasitiri mwili mzima. Hivyo ni karibu zaidi kuweza kutambulikana wasiudhiwe} [Al-Ahzaab: 59].

Kusikiliza nyimbo ni katika maasi yenye kutia moyo giza, na yanazuia kusikiliza Qur-ani, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Watakuja watu katika umma wangu watahalalisha zinaa, hariri [kwa wanaume], ulevi, na ala za muziki**», imepokewa na Bukhari, na bora anayoyasikiliza mja ni: Maneno ya Mola Mlezi wa walimwengu, mnao ndani yake nuru, uongofu na ponyo.

Mali ya halali ni wema katika Dini, ni nguvu katika mwili, ni uongofu kwa watoto, ni baraka katika vipawa, ni sababu ya kuitikiwa maombi, na ni kuwaiga Manabii, [Allah] mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلرُّسُلُ كُلُواْ مِنَ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَٱعۡمَلُواْ صَٰلِحًا﴾

{Enyi Mitume! Kuleni vyakula vizuri na tendeni mema} [Al-Mu`minuun: 51].

Mali ya haramu yametolewa baraka, ni yenye madhara mingi, mwenye mali hayo ni mwenye majuto marefu, mwenye kukataliwa maombi.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# MAJINA YA ALLAH MAZURI ZAIDI[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakaye mpoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha; kwani atakayemcha Mola wake Mlezi ataokoka, na atakayempa kisogo atapotea.

**Enyi Waisilamu:**

Elimu ya kumjua Allah ni moja wapo wa nguzo za Imani; bali hiyo ndio asili ya nguzo hizo, na zilizobaki zinaifuata, na kujua Majina ya Allah na Sifa zake ni bora zaidi na ni wajibu zaidi kati ya yaliyochumwa na nyoyo na kudirikwa na akili; ibnul Qayyim Allah amrehemu amesema: " jambo zuri zaidi kati ya yaliyo duniani: ni kumjua Yeye aliyetakasika na kumpenda".

Qur-ani yote inawaita watu katika kutazama Majina ya Allah na Sifa zake na Matendo yake; Sheikhul Islaam ibnu Taymiyyah Allah amrehemu amesema: "Na ndani ya Qur-ani mna utajo wa Majina ya Allah na Sifa zake na Matendo yake kwa wingi zaidi kuliko kutajwa kula na kunya".

Allah anampenda mwenye kupenda kutaja Sifa zake, na Nabii swala na salamu za Allah zimshukie alimbashiria yule aliyekuwa akisoma suratu al-ikhlaas kuwa Allah anampenda, akasema:

---

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe ishirini na tatu, mwezi wa Shawwali, mwaka elfu moja mia nne na ishirini na sita hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

«**Muulizeni kwa kitu gani anafanya hivo? Wakamuuliza, akasema: Kwa sababu [sura] hii ni Sifa ya Ar-Rahmaan, na mimi napenda kuisoma, basi Nabii swala na salamu za Allah zimshukie akasema: Mpeni habari ya kuwa Allah anampenda**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na Majina yake aliyetakasika ni Majina mazuri zaidi, na Sifa zake ni Sifa zilizokamilika zaidi:

﴿لَيۡسَ كَمِثۡلِهِۦ شَيۡءٞۖ وَهُوَ ٱلسَّمِيعُ ٱلۡبَصِيرُ﴾

{Hapana kitu kama mfano wake. Naye ni Mwenye kusikia Mwenye kuona} [Ash-Shuuraa: 11].

Na inastahiki kwa kila Muisilamu kuyajua, na kufahamu maana yake.

Basi Mola wetu Mlezi aliyetukuka ni mwingi wa rehema [Ar-Rahmaan] mwenye kurehemu [Ar-Rahiim]; Rehema zake zimeenea kila kitu, na Rehema yake ndio Sifa yake iliyokunjufu zaidi, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Hakika Allah ana rehema mia moja, ameteremsha kati yazo rehema moja tu baina ya majini, binadamu, na wanyama, basi kwayo ndio wanahurumiana, na kwayo ndio wanarehemeana, na kwayo mnyama mwitu amuhurumia mwanawe, na Allah amebakisha rehema tisaini na tisa atawarehemu kwazo waja wake [wema] siku ya Kiyama**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea,

Na hakuna yeyote ila anazunguka ndani ya rehema za Allah, na kila neema unayo iona ni katika rehema za Allah, na kila adhabu iliyoepushwa ni katika athari za rehema yake, ibnul Qayyim Allah amrehemu amesema: "na kikawa kitabu hichi kilicho andikwa - yaani: «**Hakika rehema zangu zimeshinda hasira zangu**» - ni kama ahadi kutoka kwa Allah aliyetakasika kwa viumbe vyake, na lau si kitabu hichi basi viumbe wangekuwa na hali nyengine", na atakayekuwa karibu na Allah basi rehema za Allah zitakuwa aula zaidi naye.

Naye aliyetakasika ni Mfalme: Mwenye kuwapelekesha

viumbe vyake kama anavyotaka, na hatetemeki yeyote wala hatulii yeyote ila kwa elimu yake na matakwa yake, anaamrisha akikataza, anapatia ushindi na akidhalilisha bila ya kizuizi wala pingamizi, hakuna chochote ndani yake [mbingu na ardhi] kinachomshinda, basi salimisha mambo yako kwa Mfalme, hatamu za mambo zipo Mkononi mwake, na mtegemee Yeye katika hali zako zote utamkuta yupo karibu [nawe].

Naye ni Al-Qudduus; aliyetakasika na mapungufu, aliyesifika na Sifa za ukamilifu; hapana Mola apasaye kuabudiwa pamoja Naye, wala hapana walii anayeitwa pamoja Naye.

Naye ni As-Salaam: Aliyesalimika kutokana na aibu zote na sifa za upungufu, viumbe vyote vinamtakasa Mola wetu Mlezi kutokana na hayo; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿يُسَبِّحُ لِلَّهِ مَا فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِي ٱلْأَرْضِ﴾

{Viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi vinamtakasa Allah} [Al-Jumua: 1].

Naye aliyetukuka na aliye juu ni Al-Mu'min: Viumbe vyake wapo kwenye amani ya kutodhulumiwa Naye au kupunguziwa haki yao, basi jiandae na uchamngu; kwani amali zinahifadhiwa na malipo yake yanazidishwa.

Naye ni Al-Muhaymin [Mwenye kushuhudia matendo ya waja], na kuona mambo yao yaliofichana na yaliofichika vifuani mwao, basi usijiaminie makri ya Allah endapo utamuasi.

Naye 'Ash-Shahiid' mwenye kushuhudia kauli na matendo ya waja wake

﴿وَمَا ٱللَّهُ بِغَٰفِلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ﴾

{Na Allah si mwenye kughafilika na yale wanayo yatenda} [Al-Baqarah: 74].

Naye ni 'Al-Aziz': Haghilibiwi, ameshinda kila kitu akavikahiri, mazito yalidhalilika kwa ushindi wake, na yakalainika magumu kwa nguvu zake,

«**pindi Allah anapohukumu jambo mbinguni Malaika hupiga mbawa zao kuinyenyekea kauli yake [Allah], kana**

**kuwa [nguvu ya Sauti waliosikia Malaika] ni silsila ya chuma iliopigwa juu ya jiwe manga**», na atakayejikurubisha Naye kwa utiifu hupata ushindi; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿مَن كَانَ يُرِيدُ ٱلۡعِزَّةَ فَلِلَّهِ ٱلۡعِزَّةُ جَمِيعًا﴾

{Mwenye kutaka ushindi basi ushindi wote ni wa Allah} [Faatwir: 10],

na mwenye kumkabili na maasi hudhalilika, basi usiangalie maasi, lakini muangalie uliyemuasi.

Naye ni 'Al-Aliyyi' aliye juu zaidi:

﴿إِلَيۡهِ يَصۡعَدُ ٱلۡكَلِمُ ٱلطَّيِّبُ وَٱلۡعَمَلُ ٱلصَّٰلِحُ يَرۡفَعُهُۥ﴾

{Kwake Yeye hupanda neno zuri, na amali njema Yeye huinyanyua} [Faatwir: 10]

Naye ni 'Al-Jabbar': Amewalazimisha viumbe vyake anayoyataka, hakuna mmoja kati yao aweza kataa:

﴿إِنَّمَآ أَمۡرُهُۥٓ إِذَآ أَرَادَ شَيۡـًٔا أَن يَقُولَ لَهُۥ كُن فَيَكُونُ﴾

{Hakika amri yake anapotaka kitu ni kukiambia tu: Kuwa! Na kikawa} [Yaasin: 82]

alisema kuiambia mbingu na ardhi:

﴿ٱئۡتِيَا طَوۡعًا أَوۡ كَرۡهًا قَالَتَآ أَتَيۡنَا طَآئِعِينَ﴾

{Njooni, kwa khiari au kwa nguvu! Vyote viwili vikasema: Tumekuja nasi ni watiifu} [Fussilat: 11],

Naye aliyetakasika ni mwenye kuziunga nyoyo za walio wanyonge.

Naye ni 'Al-Kabiir'; kila kitu ni duni yake, wala hakuna kitu ni adhimu wala kikubwa kumliko Yeye:

﴿وَٱلۡأَرۡضُ جَمِيعًا قَبۡضَتُهُۥ يَوۡمَ ٱلۡقِيَٰمَةِ وَٱلسَّمَٰوَٰتُ مَطۡوِيَّٰتُۢ بِيَمِينِهِۦ﴾

{Na Siku ya Kiyama ardhi yote itakuwa mkononi mwake, na mbingu zitakunjwa katika mkono wake wa kuume} [Az-Zumar: 67],

«**anaziweka mbingu juu ya kidole, na ardhi juu ya kidole, na miti juu ya kidole, na maji na michanga juu ya kidole, na viumbe vyote vilivyo baki juu ya kidole**», wameafikiana

Bukhari na Muslim kuipokea.

Naye ndiye 'Al-Mutakabir' mwenye kiburi peke yake, wala kiburi hakilingani ila Naye, na atakaye kufanya kiburi kati ya viumbe vyake basi mashukio yake ni Moto wa 'Saqar'; [Allah] aliyetukuka na aliye juu amesema:

﴿أَلَيْسَ فِي جَهَنَّمَ مَثْوًى لِّلْمُتَكَبِّرِينَ﴾

{Je! Si katika Jahannamu makaazi ya wanao takabari?}, [Az-zumar: 60], na ni wajibu juu ya mja kuwa dhalili na mnyenyekevu kwa Mola wake Mlezi, na kujiweka chini kwa waja [wenzake].

Naye ni 'Al-Khaaliq'; ameuleta ulimwengu na amezusha akawashangaza wenye kuupeleleza, ni Muumbaji atengeneza madhubuti alivyoviumba:

﴿فَتَبَارَكَ ٱللَّهُ أَحْسَنُ ٱلْخَٰلِقِينَ﴾

{Basi ametukuka Allah Mbora wa waumbaji}. [Al-Mu`minuun: 15].

Naye ni 'Al-Baari-u'; ameumba viumbe kutoka kutokuweko; nyota, jua na mwezi, na viumbe vinginevyo katika anga:

﴿كُلٌّ فِي فَلَكٍ يَسْبَحُونَ﴾

{vyote katika anga vinaogelea} [Al-Anbiya`: 33], vimewapiga butwaa waliovitafakari na kizingatia.

Naye ni 'Al-Muswawwir'; amewasawirisha viumbe vyake katika sifa tofauti, na maumbile mbali mbali, anavyotaka:

﴿فَمِنْهُم مَّن يَمْشِي عَلَىٰ بَطْنِهِۦ وَمِنْهُم مَّن يَمْشِي عَلَىٰ رِجْلَيْنِ
وَمِنْهُم مَّن يَمْشِي عَلَىٰٓ أَرْبَعٍ﴾

{Wengine katika wao huenda kwa matumbo yao, na wengine huenda kwa miguu miwili, na wengine huenda kwa miguu minne} [An-Nuur: 45], na amemuumba binadamu katika sura nzuri zaidi:

﴿لَقَدْ خَلَقْنَا ٱلْإِنسَٰنَ فِيٓ أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ﴾

{Bila ya shaka tumemuumba mtu kwa umbo lilio bora kabisa}

[At-Teen: 4].

Naye ni 'Al-Muswawwir' na ameharamisha kwa waja wake kutengeneza picha, na akawakemea watengenezaji picha katika viumbe vyake; na

«**Mtume swala na salamu za Allah zimshukie alimlaani mtengenezaji picha**», imepokewa na Bukhari, na alisema:

«**kila mtengenezaji picha yumo Motoni**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Naye ni 'Al-Ghafuur'; hufuta madhambi ya aliyetubia kwake miongoni mwa waja wake hata madhambi yake yakafika ukomo wa ukubwa, aliwasamehe wachawi wa Firauni na kosa lao la kupambana na Nabii wake kwa sababu ya sijida moja tu waliomsujudia Allah iliyokuwa imefungamanishwa na toba:

﴿وَإِنِّي لَغَفَّارٌ لِّمَن تَابَ وَءَامَنَ وَعَمِلَ صَٰلِحًا ثُمَّ ٱهْتَدَىٰ﴾

{Na hakika Mimi ni Mwingi wa Kusamehe kwa anaye tubia, na akaamini, na akatenda mema, tena akaongoka} [Twaaha: 82].

Naye ni'Al-Qahhaar'; viumbe viko chini ya kahri yake na kabdhi yake, hutoa roho ya anayemtaka anapotaka, hakutokei amri yoyote katika ulimwengu ila kwa kutaka kwake, hata lau mja atafanya bidii kuitekeleza.

Naye ni 'Al-Fattaah'; anafungua milango ya riziki na rehema na sababu zake kwa waja wake, na anawafungulia yaliofungika katika mambo yao na hali zao.

Naye ni 'Ar-Razzaaq'; anamruzuku mja kutoka mbinguni na ardhini:

﴿قُلْ مَن يَرْزُقُكُم مِّنَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ۖ قُلِ ٱللَّهُ﴾

{Sema: Ni nani anaye kuruzukuni kutoka mbinguni na kwenye ardhi? Sema: Allah!} [Saba : 24],

amekienea kila kitu kwa riziki yake; hakuna kiumbe ardhini ila ni juu ya Allah kukiruzuku, amewaruzuku watoto ndani ya matumbo ya kina mama, na amewaruzuku wanyama mwitu katika majangwa makavu, na ndege vitundu vilivyo juu, na samaki chini ya bahari.

Naye ni 'Al-Wahhab'; humpa amtakaye anachokitaka, zipo Mkononi mwake hazina za mbinguni na ardhini, amewaruzuku Manabii kizazi chema baada yao kufikia ukongwe katika uzee, na Suleiman salamu zimshukie alimuomba Mola wake Mlezi 'Al-Wahhab' ufalme asiopasa kuwa nao yeyote baada yake, akampatia alama na mazingatio katika vipawa; upepo, majini, na mto wa shaba iliyoyayushwa, [yote ni] yenye kuendeshwa na amri yake.

Naye ni 'Al-‘Aliim'; anajua siri na yaliofichamana, haifichamani kwake kauli wala kitendo katika wanayoyachuma waja:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ بِكُلِّ شَيۡءٍ عَلِيمٌ﴾

{Hakika Allah ni Mjuzi wa kila kitu} [Al-Anfaal: 45].

Naye ni 'As-Samiiu'; anasikia minong'ono na yaliotangazwa, na siri na yaliofichana, ukijahirisha kauli yako anaisikia, na ukiisema kwa siri kwa mwenzako anaisikia [pia], na ukiificha ndani ya nafsi yako anaijua.

Naye ni 'Al-Baswiir'; anaona mambo yaliofichana hata yakiwa madogo, hapana kinacho fichikana kwake hata chenye uzito wa chembe mdogo kabisa hata lau kitafichana [kwa waja], anaona katika giza la usiku yaliochini ya mchanga, na anaona chini ya bahari ndani ya giza.

Naye ni 'Adh-dhwaahir' na 'Al-Baatwin'; haifichiki kwake mwendo wa chungu mweusi juu ya jiwe manga katika usiku wa giza, utakapo tenda tendo la dhahiri atakuona, na utakapo fanya kwa siri hata lau ni ndani ya nyumba yako atakuona:

﴿إِنَّ رَبَّكَ لَبِٱلۡمِرۡصَادِ﴾

{Hakika Mola wako Mlezi yupo kwenye mavizio anawavizia} [Al-Fajr: 14],

na atakayejua kuwa Allah anamuona; ataona haya amuone akiwa juu ya maasi.

Naye ni 'Al-Hakiim'; katika hukumu zake na sheria zake hakuingii kasoro wala teleza, wala hakuna yeyote mwenye

uwezo wa kuzidadisi hukumu zake wala kuzivunja au kuzijadili:

﴿وَٱللَّهُ يَحۡكُمُ لَا مُعَقِّبَ لِحُكۡمِهِۦ﴾

{Na Allah huhukumu, na hapana wa kupinga hukumu yake} [Ar-Ra`ad: 41],

bali la wajibu ni kujisalimisha na kunyenyekea mbele ya hukumu zake na kuziandama:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ يَحۡكُمُ مَا يُرِيدُ﴾

{hakika Allah huhukumu analotaka} [Al-Maaidah: 1], wala hasilihi kwa waja wake ila sheria yake iliyotwahirishwa, na mwenye kufanyia maskhara Dini yake au sheria yake basi Allah humdhalilisha.

Naye ni 'Al-Latwiif'; anawafanyia upole waja wake, anawaletea riziki bila wao kuhisi.

Naye ni 'Al-Khabiir' Mjuzi wa mambo ya waja wake, hakifichamani kwake chochote, ni mwenye kuona hakika ya kila jambo:

﴿فَسۡـَٔلۡ بِهِۦ خَبِيرٗا﴾

{Uliza khabari zake [Allah] kwa amjuaye [yaani Yeye mwenyewe]} [Al-Furqaan: 59],

Naye ni 'Al-Haliim'; haharakishi adhabu ya madhambi kwa waja wake, wala hazuii neema zake na fadhila zake kwao kwa sababu ya makosa yao, wanamuasi na anawaruzuku, wanafanya dhambi na anawapa muda, wanadhihirisha na anawasitiria; basi usighurike na upole wa Allah na ukarimu wake, huenda adhabu ikakujia ghafla:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلۡإِنسَٰنُ مَا غَرَّكَ بِرَبِّكَ ٱلۡكَرِيمِ﴾

{Ewe mwanadamu! Nini kilicho kughuri na Mola wako Mlezi Mkarimu? [Ukafanya kasoro katika haki zake na ukawa jasiri katika kufanya yenye kumkasirisha!]}. [Al-Infitwar: 6].

Naye ni 'Al-Adhwiim'; anapozungumza wahyi mbingu zinafikwa na mtetemeko mkali sana kwa kumuogopa Allah, na pindi wanaoishi mbinguni wanaposikia hayo wanazimia na

wanaanguka kumsujudia Allah.

Naye ni 'Ash-Shakuur'; anatoa [malipo] mengi kwa amali chache, na anasamehe teleza nyingi, basi usidharau amali njema yoyote hata ikiwa chache, kwani mema huzidishwa maradufu; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَمَن يَقۡتَرِفۡ حَسَنَةٗ نَّزِدۡ لَهُۥ فِيهَا حُسۡنًاۚ إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٞ شَكُورٌ﴾

{Na anaye fanya wema tutamzidishia wema. Hakika Allah ni Msamehevu Mwenye shukrani} [Ash-shuuraa: 23].

Naye ni 'Al-Hafiidh'; anahifadhi amali za waja na anadhibiti kauli zao:

﴿لَّا يَضِلُّ رَبِّي وَلَا يَنسَى﴾

{Mola wangu Mlezi hapotei wala hasahau} [Twaaha: 52],

na anawahifadhi waja wake kutokana na maangamivu; alimuhifadhi Yunus salamu zimshukie akiwa ndani ya tumbo la samaki katika mashimo ya bahari, na alimuhifadhi Musa salamu zimshukie naye bado mchanga wa kunyonya akiwa katika Mto [alipotupwa na mamake kwa hofu ya kumuogopea firauni]; basi mtegemee Allah katika kuhifadhi nafsi yako na wanao, wala usichukue mazunguo ya kishirikina wala hirizi wala usiwaendee wachawi wala makuhani.

Naye ni 'Al-Qawiyyu'; hashindwi na kitu chochote, ni mwenye nguvu katika kushambulia kwake, ibnu Jariir Allah amrehemu amesema: "anapokishambulia kitu hukiangamiza", alimuamrisha Jibrili salamu zimshukie kukigeuza juu chini kijiji kilichopindukia katika machafu - kaumu ya Luut - akakiinua kwa incha ya mbawa yake kisha akakigeuza na waliomo ndani yake, na akakijalia [kijiji hicho] kuwa alama kwa wenye kuzingatia kwa karne zilizokuja:

﴿وَإِنَّكُمۡ لَتَمُرُّونَ عَلَيۡهِم مُّصۡبِحِينَ * وَبِٱلَّيۡلِۚ أَفَلَا تَعۡقِلُونَ﴾

{Na hakika nyinyi mnawapitia [kaumu ya Luut] wakati wa asubuhi * Na usiku. Basi je! Hamyatii akilini?} [As-Swaaffaat: 137-138], na atakayetaamali nguvu za anayemuasi ataacha maasi.

Naye aliyetakasika ni 'Ash-Shaafi'; anaponya na kuafu maradhi:

﴿وَإِذَا مَرِضْتُ فَهُوَ يَشْفِينِ﴾

{Na ninapo ugua ni Yeye ndiye anaye niponesha} [Ash-shu`araa`: 80],

na dawa ni sababu haipasi moyo kishikamana nazo.

Naye ni 'Al-Mannaani'; huanza kutoa kabla kuombwa, na Allah aliyetakasika ni 'Al-Muhsin'; amewafunika viumbe na ihsani yake na fadhila zake.

Naye ni 'Al-Kariim'; anatoa na anakithirisha vipawa, hakuna pazia baina yake na baina ya waja wake, basi muombe Mola wako Mlezi Mkarimu sana, na anapoifungua riziki kwa mja wake basi hakuna yeyote atamnyima; [Allah] aliyetakasika:

﴿مَّا يَفْتَحِ ٱللَّهُ لِلنَّاسِ مِن رَّحْمَةٍ فَلَا مُمْسِكَ لَهَا﴾

{Rehema ambayo Allah anawafungulia watu hapana wa kuizuia} [Faatwir: 2],

Naye ni 'Hayiyun'; «**anamuonea haya mja wake anaponyanyua mikono kwake - mja wake akamuomba kitu - airudishe mitupu**», imepokewa na Abu Daaud.

Naye ni 'Ar-Raqiib'; haghafiliki na waja wake wala hawapotei,

﴿وَمَا كُنَّا عَنِ ٱلْخَلْقِ غَٰفِلِينَ﴾

{Nasi hatukuwa wenye kughafilika na viumbe} [Al-Mu`minuun: 17],

anaona yaliofichwa na dhamiri zao, Al-Hasan Al-Basri Allah amrehemu amesema: "Allah amrehemu mja aliyesimama katika hamu yake; ikiwa ni kwa ajili ya Allah analifanya, na ikiwa ni kwa ajili ya mwengine huliacha", basi simama kisimamo cha kutaamali katika kila amali, ikiwa ni kwa ajili ya Allah basi songa, na ikiwa ni kwa ajili ya mwengine achana.

Naye ni Mwenye Mapenzi kwa waja wake wema, anawapenda wenye Subira miongoni mwao na wenye kumtegemea.

Naye ni 'Al-Waduud'; anajipendekeza kwa waja wake kwa

neema na kuacha uasi, na atakayeacha kitu kwa ajili yake humpatia ziada. Naye ni mwenye mapenzi ya waja wake wema, anawapenda wenye kutubia sana na wenye kumtegemea na wenye kusubiri.

Naye ni 'Al-Majiid', mwenye utukufu na sifa tukufu, hakuna utukufu ila wake, na kila utukufu wa asiyekuwa Yeye hakika si mengine ila ni kipawa na fadhila kutoka kwake aliyetakasika.

Naye ni 'Al-Hamiid'; anastahiki kusifiwa kwa matendo yake, anahimidi katika furaha na misiba, na kumhimdi ni katika amali bora zaidi, [Mtume] swala na salamu zimshukie amesema:

«**na [dhikri ya] 'al-hamdu lillah' inajaza mizani [ya kupima thawabu], na 'sub-haana llah wal hamdu lillah' zinajaza baina ya mbingu na ardhi**», imepokewa na Muslim.

Naye aliyetakasika 'Al-Hayyul Qayyuum'; mwenye kusimamia mambo ya viumbe wote:

﴿يَسۡـَٔلُهُۥ مَن فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضِۚ كُلَّ يَوۡمٍ هُوَ فِي شَأۡنٖ﴾

{Vinamwomba Yeye vilivyomo katika mbingu na ardhi. Kila siku Yeye yumo katika mambo} [Ar-Rahman: 29].

Naye ni 'Ahad'; hajaacha kuwa peke yake, wala hakuwa naye mwengine, na amepwekeka na aina zote za ukamilifu, hashirikiani naye katika hayo mshirika yeyote.

Naye ni 'As-Swamad'; viumbe vinamkusudia katika mahitaji yao, na vinatoa kwake mashtaka yao, na vinaweka mbele yake misiba yao.

Naye ni 'As-Sayyid'; pakukimbilia wakati wa shida na majanga ni kwake peke yake.

Naye ni 'Al-Qadiir'; mwenye uwezo uliotimia na mwenye kupitisha kila kitu; aliuambia moto wa kuchoma:

﴿كُونِي بَرۡدٗا وَسَلَٰمًا عَلَىٰٓ إِبۡرَٰهِيمَ﴾

{Sisi tukasema: Ewe moto! Kuwa baridi na salama kwa Ibrahim!} [Al-Anbiya`: 69],

basi ukawa kama alivyoamrisha, na aliamrisha bahari iliyojaa

mawimbi iwe njia kavu kwa Musa [salamu zimshukie], kisha bahari ikarudi katika hali [yake] kamili.

Naye ni 'Al-Barru'; anawafanyia ihsani waja wake na anatengeneza hali zao, mwenye kumtenda wema mtiifu katika kuwazidishia ujira, na mwenye kumtenda wema mkosa katika kumsamehe na kumuafu:

﴿إِنَّهُۥ هُوَ ٱلۡبَرُّ ٱلرَّحِيمُ﴾

{Hakika Yeye ndiye Mwema [Mtenda wema] Mwenye kurehemu} [At-Tuur: 28].

Naye ni 'At-Tawwaabu', hamrudishi mwenye kutubia, atakayemjia [kutubia] usiku au mchana humkubali bali humpenda:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلتَّوَّٰبِينَ﴾

{Hakika Allah huwapenda wanao tubu} [Al-Baqarah: 222].

Naye ni 'Al-‘Afuw'; mja atakavojifanyia israfu nafsi yake kwa maasi kisha akatubu humsamehe madhambi yake.

Naye ni 'Ar-Rauuf' anayehurumia viumbe vyake, anawajazia riziki hata wakimuasi:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ بِٱلنَّاسِ لَرَءُوفٞ رَّحِيمٞ﴾

{Kwani Allah ni Mwingi wa huruma kwa watu na Mwenye kuwarehemu} [Al-Baqarah: 143].

Naye ni 'Al-Ghaniy'; hana mahitaji kwa waja wake, Mkono wake umejaa «haupungui kwa kutoa, ni mtoaji sana usiku na mchana», [Nabii] swala na salamu zimshukie anasema katika aliyoyapokea kutoka kwa Mola wake Mlezi:

«**Enyi waja wangu! Lau wa mwanzo wenu na wa mwisho wenu, na binadamu wenu na majini wenu, watasimama katika uwanja mmoja, wakaniomba; nami nikampa kila mtu maombi yake, hilo halitapunguza chochote katika yalio kwangu, ila kama inavyopunguza sindano inapoingizwa katika bahari**», imepokewa na Muslim.

**Na baada ya haya, enyi Waisilamu:**

Allah aliyetukuka huombwa kwa Majina yake yalio mazuri zaidi, na asifiwa kwayo na kwa Sifa zake za juu, na Allah anampenda mwenye kumuomba na kumsifu, na mtu aliyekamili zaidi katika ibada ni mwenye kumuabudu kwa Majina yake yote na Sifa zake zote, na Majina yake hayadhibitiki [kwa wingi wake], miongoni mwayo ni Majina tisaini na tisa ambayo atakaye yahifadhi - kwa kuyajua maana yake, na kutenda kwa mujibu wake - ataingia Peponi.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿وَلِلَّهِ ٱلۡأَسۡمَآءُ ٱلۡحُسۡنَىٰ فَٱدۡعُوهُ بِهَاۖ وَذَرُواْ ٱلَّذِينَ يُلۡحِدُونَ فِيٓ أَسۡمَٰٓئِهِۦۚ

سَيُجۡزَوۡنَ مَا كَانُواْ يَعۡمَلُونَ﴾

{Na Allah ana Majina mazuri kabisa, basi muombeni kwa hayo. Na waacheni wale wanao haribu utakatifu wa Majina yake. Hao watakuja lipwa waliyo kuwa wakiyatenda} [Al-a`raaf: 180].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii, enyi Waislamu:**

Ufunguo wa ulinganizi wa Mitume na johari ya ujumbe wao: ni kumjua Muabudiwa kwa Majina yake na Sifa zake na Matendo yake.

Na kumjua Allah na anayostahiki miongoni mwa Majina yaliyo Mazuri zaidi na Sifa za juu; linalazimisha kumtukuza, kumuadhimisha, kumcha, kumuogopa, kumpenda, kumtarajia, kumtegemea, kuridhia kadari yake, na kusubiri mtihani wake, na kumuadhimisha Mola Mlezi katika moyo kunakuwa kwa kadri ya kumjua.

Mtu anayemjua zaidi Yeye ndio huwa mwingi zaidi wa kumuadhimisha na kumtukuza, na aliyejua Majina ya Allah na Sifa zake hujua kwa yakini kuwa machukivu yanayo msibu na misiba inayomshukia mna aina ya maslahi ndani yake asiyoweza kuyadhibiti kwa elimu yake, na Allah anapenda mujibu wa Majina yake na Sifa zake, basi Yeye ni Mkarimu [Kariim] anapenda ukarimu, mwenye busara [Haliim] awapenda watu wa busara, Mjuzi [Aliim] awapenda wenye elimu, mwenye kushukuru [Shakuur] awapenda wenye kushukuru.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# JINA LA ALLAH: 'AL-HAKIIM'[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakaye mpoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha, na kamateni Uislamu katika kishiko madhubuti kabisa.

**Enyi Waislamu:**

Maumbile yameshuhudia ya kwamba ulimwengu una Mola Mlezi aliyekamilika katika dhati yake na Sifa zake, aliyesifika na Sifa za ukamilifu, utukufu na uzuri, ni zake Sifa zote na himdi zote, na ni katika kumuadhimisha Allah kumthibitishia Sifa za ukamilifu na za utukufu.

﴿سَبَّحَ لِلَّهِ مَا فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضِۖ وَهُوَ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡحَكِيمُ﴾

{Kinamsabihi kumtakasa Allah kila kiliomo ndani ya mbingu na ardhi. Na Yeye ndiye 'Al-Aziiz' Mwenye nguvu, 'Al-Hakiim' Mwenye hekima} [Al-Hadeed: 1].

Naye aliyetakasika ni Mwenye hekima anaabudiwa mbinguni na ardhini:

﴿وَهُوَ ٱلَّذِي فِي ٱلسَّمَآءِ إِلَٰهٞ وَفِي ٱلۡأَرۡضِ إِلَٰهٞۚ وَهُوَ ٱلۡحَكِيمُ ٱلۡعَلِيمُ﴾

{Na Yeye ndiye Muabudiwa mbinguni, na ndiye Muabudiwa katika ardhi. Naye ndiye Mwenye hekima, Mwenye elimu} [Az-Zukhruf: 84], alijihimidi Nafsi yake; kwa kuwa Yeye ni Mwenye

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, mwezi wa Shawwali, mwaka elfu moja mia nne na arubaini na moja hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu za Allah zimshukie.

hekima, akasema:

﴿ٱلۡحَمۡدُ لِلَّهِ ٱلَّذِي لَهُۥ مَا فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِي ٱلۡأَرۡضِ وَلَهُ ٱلۡحَمۡدُ فِي ٱلۡأٓخِرَةِۚ وَهُوَ ٱلۡحَكِيمُ ٱلۡخَبِيرُ﴾

{Sifa njema zote ni za Allah, ambaye ni vyake vyote viliyomo mbinguni na ardhini. Na sifa ni zake Yeye katika Akhera. Naye ni Mwenye hikima, Mwenye ujuzi [Saba`: 1], na Allah alijisifu mwenyewe aliyetakasika kwa kuwa Yeye ni Mwenye kiburi, na akaihitimisha aya [kwa kueleza] kuwa Yeye ni Mwenye hekima:

﴿وَلَهُ ٱلۡكِبۡرِيَآءُ فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضِۖ وَهُوَ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡحَكِيمُ﴾

{Na ukubwa ni wake Yeye tu mbinguni na katika ardhi, naye ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima} [Al-Jaathiyah: 37].

Anao [Allah] aliyetakasika jeshi mbinguni na ardhini anaendesha anavotaka, na ni Mwenye hekima:

﴿وَلِلَّهِ جُنُودُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضِۚ وَكَانَ ٱللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا﴾

{Na Allah ndiye mwenye majeshi ya mbingu na ardhi. Na Allah ni Mwenye elimu, Mwenye hekima}, na Mola wetu Mlezi alimnadi Musa salamu zimshukie na akamtambulisha Dhati yake kuwa Yeye ni Mwenye hekima: [Al-fat`h: 7],

﴿يَٰمُوسَىٰٓ إِنَّهُۥٓ أَنَا ٱللَّهُ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡحَكِيمُ﴾

{Ewe Musa! Hakika Mimi ndiye Allah, Mwenye nguvu, Mwenye hekima} [An-Naml: 9].

Na Allah alikisifu Kitabu chake kuwa kimetoka kwa Mola Mlezi Mwenye hekima, kinaweka kila kitu pahali pake, na kinakiweka katika cheo chake, basi kikawa Kitabu madhubuti kilichokusanya hekima iliyotimia; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿كِتَٰبٌ أُحۡكِمَتۡ ءَايَٰتُهُۥ ثُمَّ فُصِّلَتۡ مِن لَّدُنۡ حَكِيمٍ خَبِيرٍ﴾

{Hiki ni Kitabu ambacho Aya zake zimewekwa wazi, kisha zikapambanuliwa, kilichotoka kwa Mwenye Hikima na Mwenye Khabari} [Huud: 1].

Naye aliyetakasika hufungua riziki zake na kuzizuilia kwa hekima yake:

﴿مَّا يَفْتَحِ ٱللَّهُ لِلنَّاسِ مِن رَّحْمَةٍ فَلَا مُمْسِكَ لَهَا ۖ وَمَا يُمْسِكْ فَلَا مُرْسِلَ لَهُۥ مِنۢ بَعْدِهِۦ ۚ وَهُوَ ٱلْعَزِيزُ ٱلْحَكِيمُ﴾

{Rehema ambayo Allah anawafungulia watu hapana wa kuizuia. Na anayo izuia hapana wa kuipeleka isipokuwa Yeye. Naye ndiye Mwenye nguvu Mwenye hekima} [Faatwir: 2].

Malaika walipokuwa sehemu ya kukiri kutoweza kwao walikiri elimu ya Allah na hekima yake na wakajisalimisha kwa amri yake:

﴿قَالُوا۟ سُبْحَـٰنَكَ لَا عِلْمَ لَنَآ إِلَّا مَا عَلَّمْتَنَآ ۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلْعَلِيمُ ٱلْحَكِيمُ﴾

{Wakasema: Subhanaka, Wewe umetakasika! Hatuna ujuzi isipokuwa kwa uliyo tufunza Wewe. Hakika Wewe ndiye Mjuzi Mwenye hekima} [Al-Baqarah: 32],

na Malaika wa kubeba Arshi na walio mbavuni zake wanawaombea waumini msamaha na Pepo za neema, na wakahitimisha maombi yao kwa Jina lake aliyetakasika 'Al-Hakiim':

﴿رَبَّنَا وَأَدْخِلْهُمْ جَنَّـٰتِ عَدْنٍ ٱلَّتِى وَعَدتَّهُمْ وَمَن صَلَحَ مِنْ ءَابَآئِهِمْ وَأَزْوَٰجِهِمْ وَذُرِّيَّـٰتِهِمْ ۚ إِنَّكَ أَنتَ ٱلْعَزِيزُ ٱلْحَكِيمُ﴾

{Mola wetu Mlezi! Na waingize katika Pepo za Milele ulizo waahidi. Na uwape haya pia wale walio fanya mema miongoni mwa wazee wao na wake zao na vizazi vyao. Hakika Wewe ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima} [Ghaafir: 8].

Na ufunuo uliowateremkia Mitume unatoka kwa Mwenye hekima:

﴿كَذَٰلِكَ يُوحِىٓ إِلَيْكَ وَإِلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِكَ ٱللَّهُ ٱلْعَزِيزُ ٱلْحَكِيمُ﴾

{Hivi ndivyo Allah Mwenye nguvu na Mwenye hekima anavyo kuletea Wahyi wewe na walio kabla yako} [Ash-shuuraa: 3],

na Manabii salamu ziwashukie walikuwa wakimuomba Allah atekeleze matarajio yao na matamanio yao kupitia kwa Jina lake aliyetakasika 'Al-Hakiim' Mwenye hekima, basi Ibrahim salamu zimshukie alimuomba Mola wake Mlezi kupitia Jina lake 'Al-

Hakiim' atutumilizie sisi [umma wa mwisho] Nabii atakayetufundisha Qur-ani na Dini:

﴿رَبَّنَا وَٱبۡعَثۡ فِيهِمۡ رَسُولٗا مِّنۡهُمۡ يَتۡلُواْ عَلَيۡهِمۡ ءَايَٰتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ ٱلۡكِتَٰبَ وَٱلۡحِكۡمَةَ وَيُزَكِّيهِمۡۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡحَكِيمُ﴾

{Ewe Mola Mlezi wetu! Waletee Mtume anaye tokana na wao, awasomee Aya zako, na awafundishe Kitabu na hekima na awatakase. Hakika Wewe ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hekima} [Al-Baqarah: 129], na Ibrahim salamu zimshukie aliacha mji wake na akahamia kwa Allah [yaani sehemu ambayo atamuabudu Allah vizuri bila pingamizi] na akasema: Hakika Mola wangu Mlezi ni Mwenye hekima:

﴿وَقَالَ إِنِّي مُهَاجِرٌ إِلَىٰ رَبِّيٓۖ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡحَكِيمُ﴾

{na akasema: Mimi nahamia kwa Mola wangu Mlezi. Hakika Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hikima} [Al-Ankabuut: 26], na Ibrahim salamu zimshukie alikaa umri mrefu bila ya kupata mtoto, Malaika wakambashiria mkewe mtoto na hali yeye [mke] ni mkongwe tena tasa, basi akastajabu na hilo, Malaika wakamwambia: Hakika Allah ni Mwenye elimu Mwenye hekima:

﴿قَالُواْ كَذَٰلِكِ قَالَ رَبُّكِۖ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلۡحَكِيمُ ٱلۡعَلِيمُ﴾

{Wakasema: Ndivyo vivyo hivyo alivyo sema Mola wako Mlezi. Hakika Yeye ni Mwenye hekima na Mwenye elimu} [Adh-dhariyaat: 30].

Yakub salamu zimshukie pamoja kusubiri kwake na kungojea kwake faraja baada kuwakosa [wanawe] Yusuf [salamu zimshukie] na ndugu yake; alithibitisha elimu ya Allah katika kuchagua zama zinazolingana zaidi na faraja anayoitarajia, na akayakinisha hekima ya Allah katika kutayarisha sababu za kuleta faraja ya hamu yake, basi akaelekea kwa Allah na matarajio yake na kumuomba kwa Jina lake 'Al-Hakiim':

﴿عَسَى ٱللَّهُ أَن يَأۡتِيَنِي بِهِمۡ جَمِيعًاۚ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلۡعَلِيمُ ٱلۡحَكِيمُ﴾

{Subira ni njema! Asaa Allah akaniletea wote pamoja. Hakika Yeye ni Mjuzi Mwenye hekima} [Yusuf: 83],

na baada ya ghamu kumuondokea Yusuf salamu zimshukie baada ya misiba ya mda na mazito alioyapata, alizungumzia neema za Allah na fadhila zake, na akathibitisha hekima ya Allah ndani ya hayo:

﴿وَقَدْ أَحْسَنَ بِيٓ إِذْ أَخْرَجَنِي مِنَ ٱلسِّجْنِ وَجَآءَ بِكُم مِّنَ ٱلْبَدْوِ مِنۢ بَعْدِ أَن نَّزَغَ ٱلشَّيْطَٰنُ بَيْنِي وَبَيْنَ إِخْوَتِيٓۚ إِنَّ رَبِّي لَطِيفٞ لِّمَا يَشَآءُۚ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلْعَلِيمُ ٱلْحَكِيمُ﴾

{Na [Allah] amenifanyia wema kunitoa gerezani, na kukuleteni kutoka jangwani baada ya Shet'ani kuchochea baina yangu na ndugu zangu. Hakika Mola wangu Mlezi ni Mpole kwa alitakalo. Bila ya shaka Yeye ni Mjuzi Mwenye hikima} [Yusuf: 100].

Jina lake aliyetakasika 'Al-Hakiim limekusanya maana ya hekima yake katika uumbaji wake na amri yake katika matakwa yake ya kidini na kiulimwengu, ibnul Qayyim Allah amrehemu amesema: "kwa sifa ya' izza' ushindi kunakuwa na ukamilifu wa uwezo, na kwa 'hikma' hekima kunakuwa na ukamilifu wa elimu, na kwa Sifa hizi mbili [Allah] aliyetakasika hupitisha alitakalo, huamrisha na kukataza, na hutoa thawabu na huadhibu, basi Sifa hizi mbili ndio chanzo cha kuumba na kuamrisha".

Na kwa hekima yake aliyetakasika ameumba viumbe vyote katika nidhamu iliyo nzuri kabisa, na akaipangilia katika utaratibu ulio mzuri kabisa, amefanya uzuri zaidi uendeshaji na kadari ndani yake, na akakipatia kila kiumbe maumbile yanayolingana nacho; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿أَعْطَىٰ كُلَّ شَيْءٍ خَلْقَهُۥ ثُمَّ هَدَىٰ﴾

{amekipa kila kitu umbo lake, kisha akakiongoa} [Twaaha: 50],

na ametoa changamoto kwa viumbe wapate katika uumbaji wake kasoro au upuzi:

﴿فَٱرْجِعِ ٱلْبَصَرَ هَلْ تَرَىٰ مِن فُطُورٖ * ثُمَّ ٱرْجِعِ ٱلْبَصَرَ كَرَّتَيْنِ يَنقَلِبْ إِلَيْكَ ٱلْبَصَرُ خَاسِئٗا وَهُوَ حَسِيرٞ﴾

{Hebu rudisha nadhari! Unaona kosa lolote? * Tena rudisha nadhari mara mbili, nadhari yako itakurejea mwenyewe hali ya kuwa imehizika nayo imechoka} [Al-mulk: 3-4].

Lau akili za viumbe zitakusanyika ili walete mfano wa kiumbe cha 'Ar-Rahmaan' au ikurubiane na yale aliyopatia viumbe miongoni mwa uzuri, utaratibu, na umadhubuti basi watashindwa; ndio Allah akaamrisha kutosheka na kutaamali hekima aliyoziweka katika viumbe vyake, na kuona baadhi ya yaliomo ndani yake miongoni mwa uzuri na umadhubuti, akasema:

﴿قُلِ ٱنظُرُواْ مَاذَا فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلۡأَرۡضِ﴾

{Sema: Angalieni yaliomo mbinguni na kwenye ardhi!} [Yunus: 101].

Kwa hekima yake aliyetakasika aliwatambulisha waja wake Dhati yake takatifu, Uisilamu, amri zake na makatazo yake, na akateremsha Kitabu chake, na akabainisha ndani yake kuwa Yeye hutuwafikia kutubu na akaikubali toba, na kuwa hakuna kutengea mambo ya duniani ila kupitia Dini, baadhi ya Salaf wamesema: "lau haingekuwa katika amri yake na sheria yake ila hekima hii adhimu, ambayo ndio msingi wa heri, na ladha kamili zaidi, basi ingekuwa ni yenye kutosha.

Naye aliyetakasika ni Mwenye hekima katika amri yake ya kilimwengu; anawatahini waja wake kwa machukivu ili awatengeze na anyanyue daraja zao, na mja ameamrishwa kuamini na kuridhia kadari za Allah na kufanya sababu zinazojuzu ili kujiondolea [machukivu], basi ajikinge na kadari za Allah kwa kadari za Allah, na asilokuwa na uwezo wa kuliondoa - kama kufa mtu wa karibu na mfano wake -; basi ataridhia na ajisalimishe, na ashuhudie ushindi wa Allah katika hukumu yake, na uadilifu wake katika kadari yake, na hekima yake katika kupitiwa [na kadari hiyo], na kuwa yaliomsibu hayakuwa ni yenye kumkosa, na yaliomkosa hayakuwa ni yenye kumsibu, na kuwa hilo limewajibishwa na uadilifu wa Allah na

hekima yake.

Allah mwenye ushindi na utukufu huenda akadhihirisha baadhi ya hekima zake kwa waja wake, akatupa habari yakuwa hekima ya kuteremsha Qur-ani ni kuwatia imara waumini, na ni uongofu na bishara kwao; akasema:

﴿قُلۡ نَزَّلَهُۥ رُوحُ ٱلۡقُدُسِ مِن رَّبِّكَ بِٱلۡحَقِّ لِيُثَبِّتَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَهُدٗى وَبُشۡرَىٰ لِلۡمُسۡلِمِينَ﴾

{Sema: Ameiteremsha hii Roho takatifu [Jibrili] kutoka kwa Mola wako Mlezi kwa haki, ili awathibitishe wale walio amini, na kuwa ni uwongofu, na ni bishara kwa Waislamu} [An-Nahl: 102]

na amewatuma Mitume ili asibaki yeyote kuwa na hoja ya kuwa haijui Dini:

﴿رُّسُلٗا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى ٱللَّهِ حُجَّةُۢ بَعۡدَ ٱلرُّسُلِ﴾

{Mitume hao ni wabashiri na waonyaji, ili watu wasiwe na hoja juu ya Allah baada ya kuletewa Mitume} [An-Nisa`: 165],

na akatupa habari kuwa hekima ya kutahini watu ni ajue [adhihirishe] ukweli wa Waumini na subira yao;

﴿أَحَسِبَ ٱلنَّاسُ أَن يُتۡرَكُوٓاْ أَن يَقُولُوٓاْ ءَامَنَّا وَهُمۡ لَا يُفۡتَنُونَ *
وَلَقَدۡ فَتَنَّا ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِهِمۡۖ فَلَيَعۡلَمَنَّ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ صَدَقُواْ وَلَيَعۡلَمَنَّ ٱلۡكَٰذِبِينَ﴾

{Je! Wanadhani watu wataachwa kwa kuwa wanasema: Tumeamini. Nao wasijaribiwe? * Hakika tuliwajaribu walio kuwa kabla yao, na kwa yakini Allah atawatambulisha walio wa kweli na atawatambulisha walio waongo} [Al-Ankabuut: 2-3],

na kwa hekima yake aliyetakasika ameificha elimu ya ghaibu kwa viumbe vyake na akaihusu nayo Nafsi yake; akasema:

﴿عَٰلِمُ ٱلۡغَيۡبِ وَٱلشَّهَٰدَةِۚ وَهُوَ ٱلۡحَكِيمُ ٱلۡخَبِيرُ﴾

{Mwenye kujua ghaibu na dhaahiri, Mwenye nguvu, Mwenye hekima} [Al-an`aam: 73].

**Na baada ya himdi hii, enyi Waisilamu:**

Basi uumbaji na amri ni za Allah peke yake, anafanya katika ulimwengu wake anavotaka, na anafanya katika sheria yake

anayoyataka, haelekezewi swali, wala hakuna makala ya kukejeli hukumu yake, amesema aliyetukuka:

﴿لَا يُسۡـَٔلُ عَمَّا يَفۡعَلُ وَهُمۡ يُسۡـَٔلُونَ﴾

{Haulizwi anayoyafanya, na wao ndio wanaoulizwa} [Al-Anbiya`: 23].

na mja ameamrishwa kuabudu kwa mujibu wa maana ya Jina lake 'Al-Hakiim', na pindi atakapo yakinisha hekima ya Allah katika kila kitu atapumbazwa na uumbaji wa Allah wenye nguvu, na utengezaji wake ulio mathubuti na atatafakari ndani yake, ataiadhimisha sheria ya Allah na atamuogopa aliyetukuka, atayaonea haya madhambi yake, atajisalimisha mbele ya amri zake [Allah] na makatazo yake, na furaha yake itazidi, kwa kuwa Allah amemuongoza katika Dini hii kwa hekima aliomtakia, na kuwa sheria imekuja kutoka kwa Mwenye hekima ili kuwapa binadamu maisha bora, na endapo balaa itamshukia ataridhia hukumu ya Allah na kadari yake, na atajisalimisha, kuwa mnao ndani ya aliyoyakadiria Allah kwake wema na heri:

﴿وَعَسَىٰٓ أَن تَكۡرَهُواْ شَيۡـٔٗا وَهُوَ خَيۡرٞ لَّكُمۡۖ﴾

{na huenda mkachukia kitu nacho ni heri kwenu} [Al-Baqarah: 216],

na atayakinisha kuwa mnao nyuma ya hilo hekima ambayo yeye haijui, na kuwa yeye anageuka geuka katika neema za Allah, [sawa] katika mazito [yanaomsibu] na ya furaha; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Ajabu ya jambo la Muumini! Hakika jambo lake lote ni heri kwake, na hana hali hiyo ila Muumini, akifikwa na ya furaha hushukuru ikawa ni heri kwake; na akifikwa na ya kudhuru husubiri ikawa ni heri kwake**», imepokewa na Muslim.

Basi ishi vizuri maishani kwa yale aliyoyaumba Allah na aliyoyataka kisheria na kilimwengu, na salimisha mambo yako kwa Mwenye hekima, atakupa zaidi unayoyatamani.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿شَهِدَ ٱللَّهُ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ وَٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ وَأُوْلُواْ ٱلۡعِلۡمِ قَآئِمَۢا بِٱلۡقِسۡطِۚ

لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡحَكِيمُ﴾

{Allah, na Malaika, na wenye elimu, wameshuhudia kuwa hakika hapana apasaye kuabudiwa ila Yeye, ndiye Mwenye kusimamisha uadilifu; hapana apasaye kuabudiwa ila Yeye Mwenye nguvu na Mwenye hikima} [Aalu-Imran: 18].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi Waisilamu:**

Allah amewajulisha waja wake maana makubwa ya uumbaji wake na amri yake pasina yale madogo (ya undani) na uchambuzi wake, na yanayofichika kwa waja miongoni mwa maana ya hekima ya Allah katika uumbaji wake, utendaji wake mzuri, amri yake, sheria yake, hukumu yake na kadari yake: inawatosha wao katika haya kuyajua kiujumla kuwa yanayo ndani yake hekima kubwa, hata wasipojua uchambuzi wake, na kuwa hilo ni katika elimu ya ghaibu ambayo Allah amepwekeka nayo.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# GHADHABU ZA MOLA MLEZI[1]

Sifa za ukamilifu zote ni za Allah, tunamhimidi, tunamuomba msaada, tunamuomba msamaha, na tunajilinda na Allah kutokana na shari za nafsi zetu, na kutokana na amali zetu mbovu, yule ataongozwa na Allah, basi hakuna wa kumpoteza, na atakaye mpoteza hakuna wa kumuongoza, nashuhudia ya kwamba hapana apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake, hana mshirika, na nashuhudia kuwa Nabii wetu Muhammad ni mja wake na mtume wake, swala na salamu za Allah nyingi zimshukie yeye, watu wake, na masahaba wake.

**Ama baada ya himdi hii:**

Mcheni Allah - enyi waja wa Allah - kama ipasavyo kumcha; kwani atakayemcha Mola wake Mlezi ataokoka, na atakayempa kisogo atapotea.

**Enyi Waisilamu:**

Allah amejitambulisha kwa viumbe vyake kwa yale yaliyokuja katika Kitabu chake na kupitia kwa ulimi wa Mtume wake swala na salamu za Allah zimshukie, na anao Allah aliyetukuka Sifa za juu katika Majina yake na Sifa zake, na kuzizingatia Sifa na kumuabudu nazo: ni njia ya [kupata] Mapenzi yake na Pepo yake, na ni njia ya kuamiliana Naye kwa matunda yake [ya Majina yake na Sifa zake] miongoni mwa hofu, matarajio, mapenzi, kumtegemea na mengineo.

Itikadi ya wema wa umma huu: ni kuthibitisha yaliozungumzwa na Kitabu na Sunnah miongoni mwa Majina na Sifa za Allah, na miongoni mwa Sifa za Allah zenye kuwajibisha kumuogopa aliyetakasika na aliyetukuka: ni Sifa ya Ghadhabu; Allah hughadhibika na huridhia si kama mmoja wapo wa viumbe, na kila Sifa kati ya Sifa zake aliyetakasika ina athari yake katika viumbe, na ni katika athari ya Sifa ya ghadhabu ya

[1] Imetolewa siku ya ijumaa, tarehe tisa, mwezi wa Dhul-Qaadah, mwaka elfu moja mia nne na arubaini hijria, katika Msikiti wa Mtume swala na salamu zimshukie.

Allah: adhabu za dunia za jumla na balaa zake; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَمَن يَحۡلِلۡ عَلَيۡهِ غَضَبِي فَقَدۡ هَوَىٰ﴾

{Na inaye mshukia ghadhabu yangu basi huyo ameangamia} [Twaaha: 81];

Sufyaan ibnu Uyayna amesema: "Ghadhabu za Allah ni ugonjwa usio na dawa".

Na huenda Hasira za Allah zikasababisha kuporomoka amali za mja; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمُ ٱتَّبَعُواْ مَآ أَسۡخَطَ ٱللَّهَ وَكَرِهُواْ رِضۡوَٰنَهُۥ فَأَحۡبَطَ أَعۡمَٰلَهُمۡ﴾

{Hayo ni kwa sababu wao waliyafuata yaliyo mkasirisha Allah na wakachukia yanayo mridhisha, basi akaviangusha vitendo vyao} [Muhammad: 28].

na pindi Allah atawakasirikia watu basi huwaadhibu; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿فَلَمَّآ ءَاسَفُونَا ٱنتَقَمۡنَا مِنۡهُمۡ﴾

{Walipo tukasirisha tuliwapatiliza} [Az-Zukhruf: 55]

ibnul Qayyim Allah amrehemu amesema: «na adhabu inakuwa kutokana na Sifa ya Ghadhabu zake, na Moto haukuwashwa ila na Ghadhabu zake»

Allah awaadhibu nayo [Ghadhabu yake] watu, na akatutajia habari zao ili tutahadhari maasi walioyafanya, [Allah] Mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿ضُرِبَتۡ عَلَيۡهِمُ ٱلذِّلَّةُ أَيۡنَ مَا ثُقِفُوٓاْ إِلَّا بِحَبۡلٍ مِّنَ ٱللَّهِ وَحَبۡلٍ مِّنَ ٱلنَّاسِ وَبَآءُو بِغَضَبٍ مِّنَ ٱللَّهِ﴾

{Wamepigwa na udhalili popote wanapo kutikana, isipokuwa wakishika kamba ya Allah na kamba ya watu. Na wakastahiki ghadhabu ya Allah} [Aalu-Imran: 112],

na ilikufuru kaumu aya za Allah baada kuwajia wakastahiki adhabu juu ya adhabu, na Allah aliwakasirikia watu akawageuza sura, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Allah aliwakasirikia kabila katika wana wa israili akawageuza wanyama wanatembea katika ardhi**», imepokewa na Muslim.

Na hakuna Nabii yeyote ila aliitahadharisha kaumu yake adhabu ya Allah; Musa salamu zimshukie aliiambia kaumu yake:

﴿أَمۡ أَرَدتُّمۡ أَن يَحِلَّ عَلَيۡكُمۡ غَضَبٌ مِّن رَّبِّكُمۡ﴾

{au mmetaka ikushukieni ghadhabu ya Mola wenu Mlezi} [Twaaha: 86].

Na wenye umbile liliosalimika waliziogopea nafsi zao, alitoka Zaid ibnu Amr ibnu Nufail kabla ya kutumilizwa [kwa Mtume] ili kuuliza kuhusu Dini, akakutana na mwanachuoni wa kiyahudi, akamuuliza kuhusu Dini yao, akasema:

«**Hauwezi kuwa juu ya Dini yetu hadi uchukue sehemu yako katika ghadhabu za Allah, Zaid akasema: Mimi sikimbii ila ghadhabu za Allah, wala sitabeba chochote katika ghadhabu za Allah kabisa, na vipi nitaliweza hilo?!**», imepokewa na Bukhari.

Muisilamu hukimbilia kwa Allah akitarajia rehema zake na radhi zake, na akihofia ghadhabu zake na hasira zake, na kumshirikisha Allah ndio jambo kubwa zaidi lenye kuwajibisha ghadhabu za Mola Mlezi na adhabu yake; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ ٱتَّخَذُواْ ٱلۡعِجۡلَ سَيَنَالُهُمۡ غَضَبٌ مِّن رَّبِّهِمۡ وَذِلَّةٌ فِي ٱلۡحَيَوٰةِ ٱلدُّنۡيَا﴾

{Hakika wale walio muabudu ndama, itawapata ghadhabu ya Mola wao Mlezi na madhila katika maisha ya dunia} [Al-a`raaf: 152].

na kuswali katika makaburi na kuswali kuyaelekea ni sababu ya kupelekea hilo [la ushirikina], [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Zimekuwa kali ghadhabu za Allah juu ya watu waliofanya makaburi ya Manabii wao kuwa Misikiti**», imepokewa na Maalik, na atakayeshindana na Allah katika Sifa zake ataadhibiwa na kinyume cha makusudio yake, [Mtume]

swala na salamu zimshukie alisema:

«**Zimekuwa kali ghadhabu za Allah juu ya mtu aliyejiita Mfalme wa wafalme**», imepokewa na Ahmad.

Allah ni Mkarimu anapenda kutoka kwa waja wake wamuombe, na humkasirikia mwenye kufanya kiburi kwa hilo [akakataa kumuomba]; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**ambaye hatamuomba Allah atamkasirikia**», imepokewa na Tirmidhi.

[Allah] haupendi ukafiri wala hauridhii, na mja atakapoufanya [Allah] humkasirikia; [Allah] Mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿مَّن شَرَحَ بِٱلۡكُفۡرِ صَدۡرٗا فَعَلَيۡهِمۡ غَضَبٞ مِّنَ ٱللَّهِ وَلَهُمۡ عَذَابٌ عَظِيمٞ﴾

{lakini aliyeufungulia kifua chake ukafiri - basi hao ghadhabu ya Allah ipo juu yao, na wao watapata adhabu kubwa} [An-Nahl: 106].

Wema wa jamii uko katika kusilihi kwa siri na dhahiri [kwa watu], na atakaye ficha uovu na akadhihirisha kinyume chake hakika amekuwa na dhana mbaya kwa Allah na amepatwa na ghadhabu ya Allah; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَيُعَذِّبَ ٱلۡمُنَٰفِقِينَ وَٱلۡمُنَٰفِقَٰتِ وَٱلۡمُشۡرِكِينَ وَٱلۡمُشۡرِكَٰتِ ٱلظَّآنِّينَ بِٱللَّهِ ظَنَّ ٱلسَّوۡءِۚ عَلَيۡهِمۡ دَآئِرَةُ ٱلسَّوۡءِۖ وَغَضِبَ ٱللَّهُ عَلَيۡهِمۡ وَلَعَنَهُمۡ وَأَعَدَّ لَهُمۡ جَهَنَّمَۖ وَسَآءَتۡ مَصِيرٗا﴾

{Na awape adhabu wanafiki wanaume na wanafiki wanawake, na washirikina wanaume na washirikina wanawake, wanao mdhania Allah dhana mbaya. Utawafikia mgeuko mbaya, na Allah awakasirikie, na awalaani, na awaandalie Jahannamu. Na hayo ni marudio maovu kabisa} [Al-fat`h: 6].

Mitume salamu ziwashukie ni wateule wa viumbe, na anayewaudhi anastahiki ghadhabu za Allah kali zaidi; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**imekuwa kali ghadhabu ya Allah kwa watu walioutoa damu uso wa Nabii wa Allah**», imepokewa na Bukhari, na

atakayeuliwa na Nabii ni katika viumbe waovu zaidi; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**imekuwa kali ghadhabu ya Allah kwa aliyeuwa Nabii**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Atakaye wakasirisha vipenzi vya Allah na waja wake wema Allah atamkasirikia, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**ukiwa umewakasirisha - yaani: kikundi cha Masahaba - basi hakika umemkasirisha Mola wako Mlezi**», imepokewa na Muslim.

Kutosubiri katika misiba hakurudishi kadari, na malipo ya mwenye hilo ni jinsi ya tendo lake, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**na atakayekasirika - yaani: kuikasirikia kadari - basi atapata hasira**», imepokewa na Tirmidhi.

Kuzuia watu na Allah kwa kauli au amali kunawajibisha adhabu ya Allah; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَٱلَّذِينَ يُحَآجُّونَ فِي ٱللَّهِ مِنۢ بَعۡدِ مَا ٱسۡتُجِيبَ لَهُۥ حُجَّتُهُمۡ دَاحِضَةٌ عِندَ رَبِّهِمۡ وَعَلَيۡهِمۡ غَضَبٞ وَلَهُمۡ عَذَابٞ شَدِيدٌ﴾

{Na wanao hojiana juu ya Allah baada ya kuitikiwa [Allah], hoja zao ni baatili mbele ya Mola wao Mlezi, na juu yao ipo ghadhabu, na itakuwa kwao adhabu kali}, [Ash-shuuraa: 16].

Ibnu Abbaas Allah amridhie amesema: "waliwajadili Waumini baada ya wao kumuitikia Allah na Mtume wake; ili wawazuie na uongofu, na wakatamani ujahili urudi".

Na ambaye hakufanyia kazi aliyoyajua basi yeye ni katika waliokasirikiwa - ambao Waisilamu wameamrishwa kumuomba Allah katika kila rakaa awaepushe njia yao -, na Allah ameadhimisha haki ya Wazazi wawili kwa ajili ya cheo chao, na akajaalia radhi zake zimo katika radhi zao, na hasira zake zimo katika hasira zao, Abdallah ibnu Umar Allah amridhie yeye na babake:

"Radhi za Mola Mlezi zimo katika radhi za mzazi, na hasira

za Mola Mlezi zimo katika hasira za mzazi", imepokewa na Tirmidhi.

Muisilamu amelindwa damu yake, na atakaye muuwa Muisilamu atapata ghadhabu ya Allah na laana yake; [Allah] Mwenye ushindi na utukufu amesema:

﴿وَمَن يَقْتُلْ مُؤْمِنًا مُّتَعَمِّدًا فَجَزَآؤُهُۥ جَهَنَّمُ خَٰلِدًا فِيهَا وَغَضِبَ ٱللَّهُ عَلَيْهِ وَلَعَنَهُۥ وَأَعَدَّ لَهُۥ عَذَابًا عَظِيمًا﴾

{Na mwenye kumuuwa Muumini kwa kukusudia, basi malipo yake ni Jahannamu humo atadumu, na Allah amemkasirikia, na amemlaani, na amemuandalia adhabu kubwa}, [An-Nisaa: 93].

Mali ya Waisilamu yamelindwa, na atakayefanyia uadui mali ya mtu Muisilamu atastahiki makemeo makali; [Mtume] swala na salamu zimshukie amesema:

«**Atakayeapa kiapo cha kukusudia ili akate nacho mali ya Muisilamu, na hali yeye ni muovu [katika kiapo kile]; atakutana na Allah na hali Yeye amemkasirikia**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

Na pindi mwanamke anapomfanyia mumewe kiapo cha kulaaniana - na hali yeye ni mrongo - basi hataacha kuwa katika ghadhabu za Allah; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَٱلْخَٰمِسَةَ أَنَّ غَضَبَ ٱللَّهِ عَلَيْهَآ إِن كَانَ مِنَ ٱلصَّٰدِقِينَ﴾

{Na mara ya tano ya kwamba ghadhabu ya Allah iwe juu yake kama mumewe yu miongoni mwa wanao sema kweli} [An-Nuur: 9].

Atakaye saidia dhuluma Allah atamkasirikia; [Mtume] swala na salamu zimshukie amesema:

«**Atakaye saidia mzozo kwa dhuluma - au akasaidia kudhulumu -; hataacha kuwa katika hasira za Allah hadi aache**», imepokewa na ibnu Maajah.

Ulimi ni katika mizani za waja, neno moja huenda likawa sababu ya kufaulu kwa mja au kuangamia; [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Hakika mmoja wenu huenda akasema neno katika hasira za Allah, asidhanie kuwa litafikia pale lilipofikia, basi Allah amuandikie kwa ajili yake hasira zake hadi siku atakutana Naye**», imepokewa na Tirmidhi.

Kukimbia vitani wakati wa kukutana na adui ni jambo la kuwajibisha ghadhabu za Allah; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَمَن يُوَلِّهِمۡ يَوۡمَئِذٖ دُبُرَهُۥٓ إِلَّا مُتَحَرِّفٗا لِّقِتَالٍ أَوۡ مُتَحَيِّزًا إِلَىٰ فِئَةٖ فَقَدۡ بَآءَ بِغَضَبٖ مِّنَ ٱللَّهِ وَمَأۡوَىٰهُ جَهَنَّمُۖ وَبِئۡسَ ٱلۡمَصِيرُ﴾

{Na atakaye wageuzia mgongo wake siku hiyo - isipo kuwa kwa mbinu za vita au kuungana na kikosi - basi atakuwa amestahiki ghadhabu ya Allah. Na pahala pake ni Jahannamu, na huo ni mwisho muovu}, [Al-anfaal: 16].

Haki ya neema ni kuishukuru, na adhabu ya kufanya kiburi ndani yake na kumsahau aliyekuneemesha nayo inaharakishwa [hapa ulimwenguni kabla ya akhera]; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿كُلُواْ مِن طَيِّبَٰتِ مَا رَزَقۡنَٰكُمۡ وَلَا تَطۡغَوۡاْ فِيهِ فَيَحِلَّ عَلَيۡكُمۡ غَضَبِي﴾

{Kuleni katika vitu vizuri hivyo tulivyo kuruzukuni, wala msiruke mipaka katika hayo, isije ikakushukieni ghadhabu yangu} [Twaaha: 81], na atakayefanya ya kumughadhibisha Allah ni wajibu kumchukia na ni haramu kumpenda na kumnusuru; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَتَوَلَّوۡاْ قَوۡمًا غَضِبَ ٱللَّهُ عَلَيۡهِمۡ﴾

{Enyi mlio amini! Msiwafanye vipenzi vyenu watu ambao Allah amewakasirikia} [Al-mumtahinah: 13].

Ni juu ya waja wafanye amali kwa ajili ya maisha ya baada ya mauti na wajiandae kwa hilo; kwani ghadhabu za Allah kali zaidi juu ya waja wake ni siku ya kukusanywa [kwa hesabu siku ya kiyama]; kwa hilo ndio Manabii salamu ziwashukie - Adam, Nuuh, Ibrahim, Musa na Isa - watasema katika kisimamo hicho adhimu:

«**Hakika Mola wangu Mlezi leo hii ameghadhibika ghadhabu ambayo hajawahi kukasirika mfano wake kabla yake, wala hataghadhibika mfano wake baada yake**», wameafikiana Bukhari na Muslim kuipokea.

**Na baada ya haya, enyi Waislamu:**

Allah ni 'Al-aqawiyyu' Al-Matiinu Mwenye nguvu, aliye Thabiti na amewatahadharisha waja wake kutokana na Hasira zake; [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَيُحَذِّرُكُمُ ٱللَّهُ نَفۡسَهُۥ﴾

{Na Allah anakuhadharisheni Nafsi yake} [Aalu- Imraan: 28], na ni juu ya waja wasighurike na Upole wa Allah kwao, kwani Yeye aliyetakasika anapoghadhibika na akaidhinisha adhabu basi hakuna wa kurudisha aliyoyapitisha, na endapo waja watafanya maasi na Allah akawamiminia neema basi hilo ni Allah kuwavuta [katika adhabu], [Allah] aliyetakasika amesema:

﴿وَأُمۡلِي لَهُمۡۚ إِنَّ كَيۡدِي مَتِينٌ﴾

{Nami nitawapa muda. Hakika mpango wangu ni madhubuti} [Al-Kalam: 45], na waja watakaporudi kwa Mola wao Mlezi Allah huwafungulia milango ya toba na heri nyingi na huwaridhia.

***'Audhu billaahi mina sh-shaitwaani rrajiim'***

﴿أَفَمَنِ ٱتَّبَعَ رِضۡوَٰنَ ٱللَّهِ كَمَنۢ بَآءَ بِسَخَطٖ مِّنَ ٱللَّهِ وَمَأۡوَىٰهُ جَهَنَّمُۖ وَبِئۡسَ ٱلۡمَصِيرُ﴾

{Je! Aliye yafuata ya kumridhisha Allah ni kama yule aliye stahiki ghadhabu ya Allah, na makaazi yake yakawa Jahannamu? Napo ni mahala pabaya pa kurejea} [Aalu-Imran: 162].

Allah anibarikie mimi na nyinyi katika Qur-ani tukufu...

## HOTUBA YA PILI

Sifa njema zote anastahili Allah kwa wema Wake [kwetu], na shukrani zote anastahili Yeye kwa kutuafikia na kutuneemesha, na nashuhudia ya kwamba hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah peke yake hana mshirika; ili kuadhimisha shani yake, na nashuhudia ya kwamba Nabii wetu Muhammad ni mja Wake [Allah] na Mtume wake, swala na salamu nyingi za Allah zimshukie yeye, watu wa nyumba yake na Masahaba wake.

**Enyi Waislamu:**

Utiifu unaleta Radhi za Ar-Rahmaan, na kwalo ndio mja hupata Rehema zake; [Allah] aliyetukuka amesema:

﴿وَرَحْمَتِي وَسِعَتْ كُلَّ شَيْءٍ ۚ فَسَأَكْتُبُهَا لِلَّذِينَ يَتَّقُونَ وَيُؤْتُونَ ٱلزَّكَوٰةَ وَٱلَّذِينَ هُم بِـَٔايَـٰتِنَا يُؤْمِنُونَ﴾

{Na rehema yangu imeenea kila kitu. Lakini nitawaandikia khasa wanao mchamngu, na wanao toa Zaka, na wale ambao wanaziamini Ishara zetu} [Al-A`raaf: 156], na katika ukunjufu wa Rehema ni kuwa zinashinda Ghadhabu zake, [Mtume] swala na salamu zimshukie alisema:

«**Hakika Allah ameandika Kitabu kabla hajaumba viumbe: Hakika Rehema zangu zimeshinda Ghadhabu zangu, nacho kimeandikwa kwake juu ya 'Arshi'**», imepokewa na Bukhari.

Kujilinda na ghadhabu za Allah linakukinga na Yeye kwa idhini yake aliyetukuka, na miongoni mwa Dua za Nabii swala na salamu za Allah zimshukie:

«**Ewe Allah, najilinda kwa Radhi zako kutokana na Hasira zako**», imepokewa na Muslim, na Muisilamu mwerevu hufanya bidii kutekeleza yenye kumpatisha Radhi za Allah, na huizuia nafsi yake kutokana na yenye kumghadhibisha Allah.

Kisha jueni kuwa Allah amewaamrisha kumswalia na kumsalimia Nabii wake...

# FAHARISI


UTANGULIZI ....................................................................5
UMUHIMU WA TAWHIDI.........................................................6
KUSHIKAMANA NA TAWHIDI...............................................14
MATUNDA YA TAWHIDI ........................................................27
UBORA WA NENO LA TAWHIDI.............................................37
AMALI INAYOPENDEZA ZAIDI KWA ALLAH.................................53
UTUKUFU WA ALLAH...........................................................63
KUMUADHIMISHA ALLAH.......................................................73
MJA KUMTAMBUA MOLA MLEZI.............................................86
ITIKADI YA MUISILAMU .........................................................97
KUWA NA DHANA NJEMA KWA ALLAH ..................................104
YENYE KUTIA DOSARI TAWHIDI. ............................................119
MAJINA YA ALLAH MAZURI ZAIDI ..........................................133
JINA LA ALLAH: 'AL-HAKIIM' ..................................................147
GHADHABU ZA MOLA MLEZI .................................................157
FAHARISI .............................................................................166


**TAASISI YA TWALIBUL ILM YA KUNUSHURU NA KUGAWA**
**00966506090448**




## VITABU VYA MTUNZI VILIVYOTOKA


SILSILA YA HOTUBA ZA AL-MASJID AN-NABAWI




**NGUZO ZA IMANI**

**NGUZO ZA UISILAMU**







**AL-AKHLAAQ**
**[TABIA]**

**NABII ﷺ**
**NA MASAHABA ZAKE ALLAH AWARIDHIE**